# Nipashe


Alhamisi Juni 13, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579943

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

## Mtoto aliyekaa miezi minne ICU Muhimbili aruhusiwa

UKURASA 3





UKURASA 13

# Raia awatuhumu polisi kumpora zaidi ya mil.1/-

**MCHEZO** ulianzia kwa wakala M-Pesa, aomba msaada wa IGP Sirro kurejeshewa fedha zake...*Endelea ukurasa wa 2*





## MACHO, MASIKIO YOTE DODOMA BAJETI KUU

UKURASA 2



IGP Sirro

## YALIYOMO


**UKURASA WA 2**

**RAIS TSHISEKEDI KUJA NCHINI LEO**
RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Felix Tshisekedi, anatarajia kuwasili nchini leo na kufanya mazungumzo na mwenyeji wake, Rais John Magufuli, Ikulu jijini Dar...

**UKURASA WA 3**

**MARAIS 16 KUHUDHURIA MKUTANO WA SADC**
MARAIS wa nchi 16 wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) pamoja na viongozi mbalimbali zaidi ya 1,000, wanatarajia...

**UKURASA WA 5**

**MALI ZA UHALIFU ZA BIL. 90/- ZATAIFISHWA**
MAKAMU wa Rais , Samia Hassan, amesema Serikali imetaifisha mali mbalimbali zilizotokana na uhalifu wa kupangwa wa kuvuka mipaka zenye thamani...


## Kakunda afunguka mazito kwa mrithi wake

UKURASA 3

MICHEZO KICHUYA, BANDA WATEMWA STARS UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

## Rais Tshisekedi kuwasili nchini leo

**Na Romana Mallya**

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo , Felix Tshisekedi, anatarajia kuwasili leo nchini na kufanya mazungumzo na mwenyeji wake, Rais John Magufuli, Ikulu jijini Dar es Salaam.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa mkutano baina ya Waziri wa Mambo ya nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, na wamiliki wa vyombo vya habari, wakurugenzi na waandishi wa habari.

Akizungumza kwenye mkutano huo uliolenga kuzungumzia mkutano wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Makonda alisema leo Rais wa Congo, Tshisekedi atawasili na kupokelewa na mwenyeji wake Rais, John Magufuli ikiwa ni ziara yake ya siku mbili.

"Rais Magufuli atampokea Rais wa Congo kesho (leo) uwanja ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere na ninawaomba wananchi wa Dar es Salaam kwa umoja wenu mjitokeze kwa wingi kumpokea Rais wa Congo ambaye atakua na ziara ya kikazi kwa siku mbili," alisema.

Makonda alisema baada ya Rais huyo kuwasili, atakwenda moja kwa moja Ikulu ambako atafanya mazungumzo na Rais Magufuli kuhusu mambo mbalimbali, ikiwamo namna ya kuimarisha uchumi na maendeleo.

"Ugeni wa viongozi mbalimbali kuja Tanzania ni matokeo ya uongozi imara na thabiti wa Rais Magufuli katika usimamizi wa amani, usalama, maendeleo na uwapo wa diplomasia imara," alisema.

# Awatuhumu polisi kumpora zaidi ya mil.1/-

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa Dar es Salaam, Nixon Moshi, amewatuhumu baadhi ya askari polisi Mkoa wa Mwanza kumpora Sh. 1,188,000, wakati akiwa mkoani humo kuhani msiba.

Katika barua yake ya wazi kwenda kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP), Simon Sirro, aliyoomba ichapishwe kwenye gazeti la Nipashe ni kutaka asaidiwe kurudishiwa fedha zake pamoja na usumbufu.

Alidai kulipwa kiasi cha Sh. 990,000 alichotumia wakati akiwa mkoani humo akisubiri upelelezi wa madai yake ambao aliambiwa unaendelea.

Alipotafutwa na gazeti hili kupitia namba yake ya simu aliyoandika kwenye barua hiyo, Moshi aliwatuhumu askari polisi hao kuchukua fedha zake Sh. 1,188,000 na kumuomba IGP amsaidie.

Alidai Mei 14, mwaka huu akiwa mkoani humo alikwenda kwa wakala wa M- Pesa akiwa na Sh. 1,630,000 kwa ajili ya kuwekewa fedha hizo kwenye simu, lakini mhudumu alimwambia kuwa ana Sh. 600,000 peke kwenye simu yake.

"Nilimkabidhi mhudumu wa M-Pesa Sh. 600,000 akadai bado Sh. 5,000, nilipompa kabla hajaniwekea fedha kwenye simu yangu alitoka nje ya duka na aliporudi alikuwa ameambatana na mlinzi wa benki ambaye ni Suma JKT na mhudumu akasema mimi ni mwizi nataka kumwibia nimempa fedha pungufu."

Aidha, alidai mhudumu huyo alipiga simu polisi na walifika askari watatu na kumchukua kuelekea kituoni.

"Palepale askari waliniuliza nina shilingi ngapi, nikawajibu jumla nina Sh. 1,630,000 na nikitoa nilizomkabidhi mhudumu wa M-Pesa, nilizonazo mfukoni ni Sh. 1,030,000."

Alidai kuwa waliondoka na askari hao ambao walijitambulisha kwa majina, mmoja alijitambulisha kwa jina la Lyimo wakati jina lake halisi ni Novatus na mwingine alijitambulisha kama Dula wakati jina lake halisi ni Abdalah na watatu hakujitambulisha.

"Askari hawa hawakunipeleka mapokezi kituo cha polisi waliniingiza kwenye vyumba ambako ni karibu na kituo cha polisi vilivyopakana na ofisi ya Mkuu wa Upelelezi Mkoa (RCO), walinipekuwa, hawakuandika maelezo ili isijulikane kiasi nilichokuwa nacho."

"Walichukua maelezo na baadaye wakaniambia Mkuu wa Polisi Wilaya (OCD) anazitaka fedha. Wakanirudishia Sh. 442,000. Hawakunifungulia kesi yoyote wakaniambia nijidhamini kwa Sh. 500,000 ya maneno, wakaniruhusu niondoke."

Moshi alidai kuwa Mei 15, aliamua kuwasiliana na Kamanda wa Polisi wa Mkoa huo pamoja na RCO ili wamsaidie kuhusu suala lake na kumwambia aende kwa OCD.

"Nilikwenda kwa OCD na askari wale walipatikana na RCO akasema ufanyike uchunguzi na kazi hiyo alipewa askari Sajenti Christopher (ametaja namba yake ya simu),

INAENDELEA UK. 8



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, akizungumza na wamiliki na wakuu wa vyombo vya habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kuanza kwa maandalizi ya mkutano wa 39 wa SADC utakaofanyika jijini humo mwezi Agosti 17/18. Kulia ni Katibu Mtendaji wa chama cha wamiliki wa vyombo vya habari (MOAT), Henry Muhanika, Mwenyekiti wa kamati ya maandalizi, Agnes Kayola na Msemaji wa Serikali Dk. Hassan Abbas. **PICHA: JOHN BADI**

# Macho, masikio bungeni Bajeti Kuu

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MACHO na masikio yanatarajiwa kuelekezwa bungeni jijini Dodoma leo wakati serikali itakapowasilisha makadirio ya bajeti yake kwa mwaka ujao wa fedha.

Mpango wa Maendeleo ya Taifa na ukomo wa bajeti ya mwaka 2019/20, unaonyesha bajeti hiyo ya nne kwa serikali ya awamu ya tano, inatarajiwa kuwa Sh. trilioni 33.1.

Kwa mujibu wa mpango huo, mapato ya ndani yakijumuisha yatokanayo na halmashauri yanatarajiwa kuwa Sh. trilioni 23. Serikali Kuu inatarajia kukusanya Sh. trilioni 22.2. Kati yake, mapato yatokanayo na kodi Sh. trilioni 19.1 na mapato yasiyo ya kodi Sh. trilioni 3.1.

Vilevile, mpango huo unabainisha kuwa mapato ya halmashauri yanatarajiwa kuwa Sh. bilioni 765.4, mikopo ya ndani na nje Sh. trilioni 7.27 (yenye masharti ya kibiashara Sh. trilioni 2.3) na misaada na mikopo yenye masharti nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo Sh. trilioni 2.7.

Katika bajeti hiyo, kunatarajiwa kuwa na ongezeko na punguzo la tozo katika bidhaa mbalimbali zinazozalishwa ndani na nje ya nchi kama ilivyokuwa katika bajeti zilizopita.

Bidhaa zinazotarajiwa kuguswa ni pamoja na vinywaji baridi (soda, maji na juisi), sigara, mvinyo, pombe na pombe kali.

Maeneo mengine muhimu yanayotarajiwa kuguswa ni unafuu wa kodi kwenye sekta ya viwanda, kilimo, mifugo, madini na huduma muhimu za kijamii kwa lengo la kudhibiti mfumuko wa bei na kulinda viwanda vya ndani.

Serikali pia inatarajiwa kuondoa migongano ya sheria, kanuni na taratibu zinazotumiwa na mamlaka mbalimbali katika utozaji kodi na gharama kubwa za kuanzisha na kuendesha biashara kutokana na wingi wa kodi, ada na tozo zinazoambatana na taratibu zenye urasimu.

Vilevile, serikali inatarajiwa kuwasilisha bajeti yenye mikakati ya kuondoa mianya na mazingira ya rushwa na muingiliano wa majukumu na wingi wa mamlaka za udhibiti katika kuidhinisha na kutoa hati, vibali na vyeti kwenye shughuli za uwekezaji na biashara.

**UTITIRI WA MAMLAKA, TOZO**

Wiki iliyopita wafanyabiashara walikutana na Rais John Magufuli jijini Dar es Salaam na moja ya malalamiko yao ni utitiri wa mamlaka zinazohusika na biashara.

Bajeti ya nne ya awamu tano inatarajiwa kuwa na marekebisho na kufutwa kwa baadhi ya tozo za kibiashara.

Marekebisho hayo pia yanatarajiwa kwenda sambamba na ama kufutwa au kuunganishwa kwa mamlaka za udhibiti, taasisi na mashirika ya umma.

Tayari serikali ya awamu ya tano imeshaziunganisha baadhi ya mamlaka, taasisi na mashirika ya umma na imeshaweka wazi kwamba mchakato wa kupitia miundo ya kiutendaji ya mashirika na taasisi zote za umma unaendelea.

Taasisi na mashirika ya umma yanayounganishwa ni pamoja na yale yanayoonekana kuingiliana kimajukumu, ingawa uamuzi huo pia huenda ukawa na athari kwenye upatikanaji wa ajira.

Mamlaka ambazo huenda zikaunganishwa ni pamoja na Shirika la Viwango (TBS) ambalo majukumu yake yanaonekana kufanana na yale yanayotekelezwa na Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) na Tume ya Ushindani (FCC).

**MAJIBU YA HOJA SITA**

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti tangu Jumatatu ya wiki iliyopita ilikuwa katika mazungumzo na serikali kuhusu hoja za msingi sita ambazo Bunge halikufikia mwafaka na serikali wakati wa mijadala ya kisekta.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, George Simbachawene, aliambia Nipashe mwanzoni mwa wiki kuwa majadiliano na serikali

INAENDELEA UK.8

## HABARI KITAIFA



Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Dar es Salaam, Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu maadhimisho ya walei na jubilei ya miaka 50, yatakayofanyika Msimbazi Centre Jumapili ijayo. Kushoto ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Walei Taifa, Gasper Makiluli. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Waziri aliyetumbuliwa na Magufuli afunguka

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

ALIYEKUWA Waziri wa Viwanda na Biashara, Joseph Kakunda, amefunguka na kudai kuwa kwa muda ambao amekuwa Waziri amejifunza mengi ikiwamo umuhimu wa Wizara hiyo, kulaumiwa na kusifiwa na kila mtu.

Pamoja na hayo, amemsihi Waziri mpya, Innocent Bashungwa, kuhakikisha ahadi aliyoitoa kwa Rais John Magufuli kwamba hatamuangusha aisimamie.

Kakunda alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akimkabidhi ofisi Waziri Bashungwa, katika ofisi zao zilizopo mji wa serikali, jijini hapa.

Alimpongeza Bashungwa kwa dhamana aliyopewa huku akimwambia kuwa ana jukumu kubwa ambalo Rais amelikasimisha kwake.

"Wizara hii ya viwanda inabeba ajenda ya maendeleo ya nchi kwa sasa, mimi nikwambie sasa katika muda mfupi niliokaa hapa wizarani nimejifunza umuhimu wa hii wizara,kwa sababu wizara hii kutokana na umuhimu wake kila mtu anailaumu na kila mtu anaisifu kwa hiyo huwezi kushangaa Rais ana matarajio makubwa sana na wizara hii," alisema.

Aidha, alisema matarajio ya Rais ni kigezo kimoja wapo cha Waziri mpya kujipima

INAENDELEA UK.8

# Mtoto aliyekaa miezi minne ICU atoka hospitali

**Na Beatrice Shayo**

KATIKA hali isiyo ya kawadia mwanafunzi, Hilary Plasdius (8), aliyekaa Chumba cha Uangalizi Maalumu (ICU) kwa miezi minne huku akipumulia mashine kwa miezi mitatu baada ya kuugua ugonjwa wa kupooza, jana ameruhusiwa kutoka hospitali.

Mwanafunzi huyo alilazwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Mloganzila kuanzia Oktoba 27, mwaka jana akipatiwa matibabu.

Akizungumzia ugonjwa huo, Daktari Bingwa wa watoto, Mwanaidi Amiri, alisema mtoto huyo alikuwa na shida ya kupooza mwili.

"Hilary alikuja akiwa na shida ya kupooza mwili kuanzia miguuni hadi kwenye shingo mpaka akawa anapata shida ya kupumua, ni ugonjwa unawatokea watu wazima na watoto."

Aliongeza:" Mara nyingi ugonjwa huo unatokea baada ya mtu kupataka maambukizi ya bakteria kupitia mfumo wa kifua au mtoto akiharisha, mwili wake ukiwa unashambulia mishipa ya fahamu na kusababisha mishipa yake kukosa nguvu na kujikuta anashindwa kunyanyua miguu," alisema.

Alisema mtoto huyo alivyopata ugonjwa huo ulienda kwa haraka sana na siku waliyompokea hakuwa anaweza kupumua.

"Kwa sababu alikuwa anashindwa kupumua tulimpeleka ICU maana mishipa yake ilikuwa dhaifu ambako alikaa miezi minne na mpaka sasa ana miezi minane hapa hospitalini," alisema.

Dk. Amiri alisema kwa sasa amepata nafuu na anaweza kunyanyua miguu na mikono hali iliyowafanya waridhike na kuamua kumruhusu kurudi nyumbani.

Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa hospitali huyo, Dk. Julieth Magandi, alisema wanafuraha kwa mtoto huyo kuruhusiwa kwa kuwa alikuwa ICU muda mrefu.

INAENDELEA UK.8

# Marais nchi 16 kuhudhuria mkutano wa SADC Dar

**Na Romana Mallya**

MARAIS wa nchi 16 wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) pamoja na viongozi mbalimbali zaidi ya 1,000 wanatarajia kuja nchini kuhudhuria mkutano wa 39 wa Jumuiya hiyo utakaofanyika Agosti 17, jijini Dar es Salaam.

Mkutano wa mwisho wa SADC kufanyika Tanzania ulikuwa mwaka 2003, chini ya uongozi wa Rais wa awamu ya tatu, Benjamin Mkapa, miaka 16 iliyopita.

Waziri wa Mambo ya nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, alitoa taarifa hiyo katika mkutano wake na wamiliki wa vyombo vya habari, wahariri, wakurugenzi na waandishi wa habari.

Mkutano huo ulilenga kuzungumzia mkutano wa SADC unaotarajia kufanyika kwa siku mbili kuanzia Agosti 17, vyombo vya habari vikitakiwa kuwa na uzalendo katika kuhabarisha umma habari zinazohusu mkutano huo kuanzia sasa na baada ya mkutano huo.

Kabudi alisema mkutano huo utatanguliwa na vikao vya awali vya kazi vya makatibu wakuu na mawaziri wa jumuiya hiyo vitakavyoanza Agosti 9 hadi 16.

Aidha, kutakuwa na maonyesho ya awamu ya nne ya wiki ya viwanda kwa nchi za SADC yatakayofanyika katika ukumbi wa Mlimani City kuanzia Julai 22 hadi 26.

"Mkutano huu utahudhuriwa na wakuu wa nchi wanachama 16 watakaoambatana na viongozi na maofisa waandamizi mbalimbali takribani 1000."

"Ndugu zangu wamiliki wa vyombo vya habari na wakurugenzi hii ni heshima kwetu kama taifa ya kuwa mwenyeji wa mkutano huu wa SADC na Rais John Magufuli ambaye sasa ni Makamu Mwenyekiti atakuwa mwenyekiti wa Jumuiya hiyo muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi kwa nchi wanachama kwa mwaka mmoja mpaka Agosti 2020," alisema.

Pia alisema Waziri wa Mambo ya Nje ambaye ni yeye,

INAENDELEA UK.8

CAPITAL RADIO

POPOTE ULIPO SIKILIZA CAPITAL RADIO KATIKA MASAFA YAFUATAYO




www.capitalradioco.tz @capitalradiotanzania @CapitalRadiotz capitalradiotz

## HABARI KITAIFA

# Mali za uhalifu za bil. 90/- zataifishwa

**Na Elizabeth Zaya**

MAKAMU wa Rais , Samia Hassan, amesema Serikali imetaifisha mali mbalimbali zilizotokana na uhalifu wa kupangwa wa kuvuka mipaka zenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 90 katika sekta mbalimbali. Sekta hizo ni madini, maliasili, fedha hususani katika maeneo ya upatu (DECI) na maeneo mengine.

Akizungumza katika maadhimisho ya miaka 10 na mkutano mkuu wa Umoja wa urejeshaji wa mali zinazohusiana na uhalifu kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara (ARINSA), Makamu wa Rais alisema mafanikio hayo yametokana na Tanzania kufanya marekebisho makubwa katika sheria ya utaifishaji wa mali zitokanazo na uhalifu pamoja na sheria ya kuzuia utakatishaji wa fedha haramu.

Alisema lengo la kufanya maboresho hayo ni kuhakikisha zinakuwa na ufanisi unaotakiwa katika kupambana na mbinu mpya za kihalifu, hasa katika makosa ya uhalifu wa kupangwa na mengine yanayovuka mipaka.

Pia alisema mafanikio hayo yametokana na dhamira ya dhati ya nchi wanachama katika kuhakikisha kuwa malengo ya msingi ya Umoja huo yanafanikiwa ambayo pia yanaunga mkono jitihada zinazofanywa na serikali ya Rais John Magufuli ya kupambana na rushwa na ufisadi.

"Nchi wanachama wa ARINSA wamesaini na kuridhia mkataba wa Kimataifa wa kupambana na makosa ya kupangwa pamoja na mikataba mingine ya kimataifa na kikanda inayohusiana na mapambano dhidi ya uhalifu.," alisema Makamu wa Rais na kuongeza:

"Mkataba wa kupambana na makosa ya kupangwa una vipengele ambavyo vinazitaka nchi wanachama kuweka mikakati yenye lengo la kuhakikisha kuwa uhalifu wa kupangwa unatokomezwa."

Aliongeza: "Kwa mfano ibara ya 6 ya mkataba huo unazitaka nchi hizo kushughulika na wahalifu wanaojihusisha na utakatishaji wa mali zitokanazo na uhalifu, na ndiyo maana baadhi ya nchi wanachama zimeshatunga sheria za uzuiaji utakatishaji fedha haramu. Rai yangu ni kwa zile nchi ambazo hazijatunga sheria hiyo kuhakikisha kwamba sheria hiyo inatungwa."

Makamu wa Rais alisema ibara ya 19 na 27 pamoja na mkataba wa kupambana na makosa ya kupangwa unahimiza umuhimu wa vyombo vya uchunguzi katika nchi wanachama kufanya upelelezi kwa pamoja kwa lengo la kuhakikisha kuna ufanisi katika matokeo ya upelelezi husika na kupata mafanikio katika uendeshaji wa kesi hizo zifikapo mahakamani.

Alisemza bado kuna idadi ndogo ya wapelelezi na waendesha mashtaka ikilinganishwa na wingi wa mashauri yanayohusiana na utaifishaji na urejeshaji wa mali zinazohusiana na uhalifu.

Pia Makamu wa Rais alisema atahakikisha anapambana na uhalifu unaotumia mkaa kama kiongozi mwenye dhamana ya mazingira nchini.

"Jana nilikuwa na mazungumzo kidogo na DPP, lakini katika mazungumzo hayo nilikuwa nashangaa kwamba misitu inachangiaje kwenye uhalifu , lakini alinieleza kwamba mkaa tunaotumia kupikia na wenyewe una mchango wake katika uhalifu kwa sababu ni mkaa huo huo ambao unasafirishwa, unauzwa nje kutoka Tanzania na fedha zinaingia katika makundi maovu, kwa hiyo hilo nalo ni eneo jingine ambalo mimi kama msimamizi wa mazingira wa nchi hii, lazima nisimame kulishughulikia, kwa kuhakikisha miti haikatwi na kutengeneza mikaa ambayo inaenda kuingia kwenye uhalifu," alisema Makamu wa Rais.

Kwa upande wake Rais wa ARINSA, Biswalo Mganga, alisema kuanzia mwaka 2013 hadi mwaka huu umoja huo umetaifisha mali zenye thamani ya dola za Marekani bilioni 1.406.

Rais huyo ambaye pia ni Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP), alisema mwaka huu pekee walitaifisha mali zenye thamani ya dola za Marekani milioni 700 na mali zinazoshikiliwa mpaka sasa zina thamani ya Dola za Marekani 594.23, na kwamba maombi ya kutaifisha mali waliyonayo mpaka sasa ni 142.

# Aliyekumbwa vyefi feki adaiwa kutoweka na GPS ya wilaya

**Na Yasmine Protace,** KIBITI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kibiti mkoani Pwani inamsaka aliyekuwa Ofisa Ardhi wa Wilaya hiyo, kwa madai ya kuondoka na kipimo cha kupimia ramani (GPS).

Ofisa huyo anadaiwa aliondoka na kifaa hicho baada ya kuacha kazi kutokana na kukumbwa kwenye sakata la wenye vyeti feki.

Hayo yalisemwa jana na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Khatibu Chaulembo, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Chaulembo alimtaja mtuhumiwa huyo kuwa ni Salehe Shekimwa.

"Huu ni mwezi wa sita sasa tangu aondoke na kipimo hicho, na tumemtafuta hatujafanikiwa kumpata, aliacha kazi kwa notisi ya saa 24 na muda mfupi tu akagundulika kwenye vyeti feki" alisema.

Alisema halmashauri itamchukulia hatua kama asiporudisha kipimo hicho, na jitihada za kumtafuta kokote aliko zinaendelea.

Aliongeza kuwa halmashauri imekinunua kifaa hicho kwa ajili ya matumizi ya kupimia kutokana na kuchukuliwa kipimo hicho, wanafanya kazi katika mazingira magumu, ikiwamo kukodisha kifaa hicho.


| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 41 | 761/32 | SAMORA/OHIO | 101 | 915.92 | Biashara |
| 42 | 761/32 | SAMORA/OHIO | 201 | 915.92 | Biashara |
| 43 | 761/32 | SAMORA/OHIO | 309 | 79.00 | Biashara |
| 44 | 761/32 | SAMORA/OHIO | 301 | 915.92 | Biashara |
| 45 | 761/32 | SAMORA/OHIO | 000 | 915.92 | Biashara |
| 46 | 761/32 | SAMORA/OHIO | 403 | 30.67 | Biashara |
| 47 | 2203-5/32 | PAMBA/SOKOINE | 017 | 69.35 | Biashara |
| 48 | 2203-5/32 | PAMBA/SOKOINE | 102 | 254.05 | Biashara |
| 49 | 2203-5/32 | PAMBA/SOKOINE | 201 | 473.60 | Biashara |
| 50 | 2203-5/32 | PAMBA/SOKOINE | 203 | 209.56 | Biashara |
| 51 | 2203-5/32 | PAMBA/SOKOINE | 302 | 308.00 | Biashara |
| 52 | 2203-5/32 | PAMBA/SOKOINE | 303 | 70.00 | Biashara |
| 53 | 2203-5/32 | PAMBA/SOKOINE | 401 | 212.44 | Biashara |
| 54 | 2273-4/32 | AZIKWE/SAMORA | 102 | 320.00 | Biashara |
| 55 | 2273-4/32 | AZIKWE/SAMORA | 111 | 44.50 | Biashara |
| 56 | 2273-4/32 | AZIKWE/SAMORA | 204 | 209.53 | Biashara |
| 57 | 2273-4/32 | AZIKWE/SAMORA | 311 | 15.38 | Biashara |
| 58 | 2273-4/32 | AZIKWE/SAMORA | 312 | 3.28 | Biashara |
| 59 | 331/36 | MKWEPU | 103 | 28.00 | Biashara |
| 60 | 331/36 | MKWEPU | 104 | 26.40 | Biashara |
| 61 | 331/36 | MKWEPU | 105 | 34.13 | Biashara |
| 62 | 331/36 | MKWEPU | 106 | 37.65 | Biashara |
| 63 | 331/36 | MKWEPU | 201 | 28.00 | Biashara |
| 64 | 331/36 | MKWEPU | 202 | 12.00 | Biashara |
| 65 | 331/36 | MKWEPU | 206 | 20.12 | Biashara |
| 66 | 2229/41 | ZANAKI | 102 | 12.39 | Biashara |
| 67 | 2229/41 | ZANAKI | 103 | 31.43 | Biashara |
| 68 | 2229/41 | ZANAKI | 104 | 31.43 | Biashara |
| 69 | 2229/41 | ZANAKI | 204 | 83.93 | Biashara |
| 70 | 2229/41 | ZANAKI | 208 | 54.00 | Biashara |
| 71 | 2229/41 | ZANAKI | 209 | 43.81 | Biashara |
| 72 | 2229/41 | ZANAKI | 210 | 25.27 | Biashara |
| 73 | 2229/41 | ZANAKI | 211 | 40.68 | Biashara |
| 74 | 2229/41 | ZANAKI | 304 | 22.18 | Biashara |
| 75 | 567/48 | SAMORA/MOROGORO ROAD | 102 | 51.00 | Biashara |
| 76 | 567/48 | SAMORA/MOROGORO ROAD | 103 | 17.28 | Biashara |
| 77 | 567/48 | SAMORA/MOROGORO ROAD | 104 | 14.70 | Biashara |
| 78 | 567/48 | SAMORA/MOROGORO ROAD | 109 | 15.80 | Biashara |
| 79 | 567/48 | SAMORA/MOROGORO ROAD | 111 | 21.10 | Biashara |
| 80 | 567/48 | SAMORA/MOROGORO ROAD | 113 | 11.00 | Biashara |
| 81 | 568/48 | SAMORA/MANSFIELD | 005 | 76.86 | Biashara |
| 82 | 568/48 | SAMORA/MANSFIELD | 009 | 50.45 | Biashara |
| 83 | 568/48 | SAMORA/MANSFIELD | 012 | 20.80 | Biashara |
| 84 | 568/48 | SAMORA/MANSFIELD | 107 | 20.10 | Biashara |
| 85 | 114/49 | SAMORA | 101 | 35.00 | Biashara |
| 86 | 114/49 | SAMORA | 403 | 26.00 | Biashara |
| 87 | 114/49 | SAMORA | 404 | 21.18 | Biashara |
| 88 | 232/59 | MOROGORO RD | 102 | 30.00 | Biashara |
| 89 | 636/59 | SAMORA | 105 | 46.00 | Biashara |
| 90 | 2311/8 | SAMORA | 121 | 22.84 | Biashara |
| 91 | 2311/8 | SAMORA | 123 | 25.00 | Biashara |
| 92 | 175/3 | JAMHURI | 006 | 22.58 | Biashara |
| 93 | 175/3 | JAMHURI | 007 | 45.27 | Biashara |
| 94 | 175/3 | JAMHURI | 009 | 23.76 | Biashara |
| 95 | 291&230/59 | SAMORA/MOROGORO ROAD | 001 | 98.32 | Biashara |
| 96 | 291&230/59 | SAMORA/MOROGORO ROAD | 103M | 20.88 | Biashara |
| 97 | 148,123&125/50 | SAMORA/BRIDGE | 1101 | 1,742.11 | Makazi |
| 98 | 26/00 | MKWEPU | 501 | 110.37 | Biashara |
| 99 | 26/00 | MKWEPU | 801 | 110.37 | Biashara |
| 100 | 1429/21 | SEWA | 004 | 54.57 | Biashara |
| 101 | 106/27 | A.H.MWINYI | 405 | 29.67 | Biashara |
| 102 | 1465/71 | ZANAKI | 002 | 98.00 | Biashara |
| 103 | 1465/71 | ZANAKI | 004 | 20.25 | Biashara |
| 104 | 1314/78 | MALI/ASIA | 006 | 37.50 | Biashara |
| 105 | 2171/82 | JAMHURI | 102 | 17.49 | Biashara |
| 106 | 1278/84 | ZANAKI | 001 | 61.20 | Biashara |
| 107 | 1278/84 | ZANAKI | 002 | 39.67 | Makazi |
| 108 | 1278/84 | ZANAKI | 005 | 52.20 | Biashara |
| 109 | 139/00 | MAGORE | 003 | 110.00 | Biashara |
| 110 | 308/00 | A.H.MWINYI | 002 | 160.50 | Makazi |
| 111 | 880-883/00 | FIRE | 009 | 119.40 | Biashara |
| 112 | 2109/5 | SEA VIEW | 003 | 100.65 | Biashara |
| 113 | 37/00 | A.H.MWINYI | 001 | 611.22 | Biashara |

Kwa Mawasiliano zaidi:
Upanga: +255 22 2128305

Temeke: +255 22 2851207 / 2850396
Kinondoni: +255 22 2667150
Ilala: +255 22 2203138
OFISI YA MAWASILIANO NA HUDUMA KWA JAMII

NHC-MAKAO MAKUU

215271602

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Karibu bajeti 2019/20, uzalendo wahitajika

**MAKADIRIO** ya bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha yanatarajiwa kuwasilishwa bungeni jijini Dodoma baadaye leo jioni. Mpango wa Maendeleo ya Taifa na ukomo wa bajeti ya mwaka 2019/20, unaonyesha bajeti hiyo ya nne kwa serikali ya awamu ya tano, inatarajiwa kuwa Sh. trilioni 33.1. Kwa mujibu wa mpango huo, mapato ya ndani yakijumuisha yatokanayo na halmashauri yanatarajiwa kuwa Sh. trilioni 23.

Mpango huo unabainisha kuwa Serikali Kuu inatarajia kukusanya Sh. trilioni 22.2. Kati yake, mapato yatokanayo na kodi Sh. trilioni 19.1 na mapato yasiyo ya kodi Sh. trilioni 3.1.

Nipashe tunaipongeza serikali kwa jitihada zake katika kuongeza makusanyo na kudhibiti mianya ya ufujaji wa fedha za umma kwa lengo la kutekeleza miradi ya maendeleo.

Takwimu za makusanyo zinazotolewa na Mamlaka ya Mapato (TRA), zinaonyesha serikali ya awamu ya tano imefanikiwa kuongeza makusanyo kwa wastani Sh. bilioni 450 kwa mwezi.

Takwimu hizo zinaonyesha kuwa serikali ya awamu ya tano imeongeza makusanyo kutoka wastani wa Sh. bilioni 850 kabla ya Novemba 2015 hadi kufikia Sh. trilioni 1.3 kwa mwezi.

Hata hivyo, pamoja na jitihada zinazofanywa na serikali kuimarisha makusanyo ya nchi kwa kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato, taarifa za kamati mbalimbali za Bunge na ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), zinaonyesha utekelezaji usioridhisha wa miradi ya maendeleo kutokana na ukosefu wa fedha.

Hii inatokana na ukweli kwamba kiwango kikubwa cha makusanyo kinatumika kulipa Deni la Taifa na mishahara ya watumishi wa umma.

Kwa mujibu wa Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, serikali inatumia wastani wa Sh. bilioni 600 kulipa Deni la Taifa na Sh. bilioni 550 kwa mishahara ya watumishi wa umma kila mwezi, hivyo katika makusanyo yake ya Sh. trilioni 1.3, hubakiwa na Sh. bilioni 150 pekee.

Ni kutokana na hali hii, Nipashe tunaona ipo haja kuongeza juhudi zaidi katika ukusanyaji wa mapato ya nchi ili kutekeleza miradi muhimu kwa manufaa ya kizazi kilichopo na kijacho.

Tunapoelekea kufunga mwaka wa fedha 2018/19 siku 18 zijazo, mamlaka zinazohusika na ukusanyaji wa mapato, zinapaswa kujipanga kuhakikisha zinatatua changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka huu ili zisijirudie mwakani.

Tunaamini hatua kali zitaendelea kuchukuliwa dhidi ya wanaojihusisha na kadhia ya ukwepaji kodi na uhujumu uchumi kwa ujumla.

Baadhi ya nchi za Amerika, kosa la kukwepa kodi halina faini. Yeyote anayepatikana na hatia hiyo hulazimika kutumikia kifungo gerezani.

Hata Tanzania, wanaohukumiwa kifungo kwa makosa ya ukwepaji kodi, wamekuwa hawajumuishwi kwenye utaratibu wa msamaha wa Rais. Yote haya yanaonyesha jinsi suala la ulipaji kodi lilivyo muhimu kwa maendeleo ya nchi.

Tanzania ina takribani watu milioni 50 sasa, lakini takwimu za ulipaji wa kodi zinaonyesha walipakodi hawafiki hata robo ya watu wote waliopo nchini. Tunaamini hamasa na elimu ya ulipaji wa kodi itaisaidia nchi kuongeza mapato yake na hatimaye kutekeleza miradi muhimu kwa fedha za ndani badala ya kutegemea misaada na mikopo kutoka nje.

Hatupingi utaratibu wa serikali kukopa kwa lengo la kutekeleza miradi ya maendeleo, lakini tunaona ni muhimu wananchi wakahamasishwa zaidi kulipa kodi na kusaidia jitihada hizo za serikali kuimarisha uchumi wa nchi. Tunaamini huo ndiyo uzalendo unaohitajika kutimiza ndoto za kuijenga Tanzania yenye uchumi wa kati kufikia mwaka 2025.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Tabia ya kubana haja ndogo safarini hatari 'kote kote'

Na Sabato Kasika

**KATIKA** maisha ya kila siku, imekuwa ni jambo la kawaida kwa baadhi ya watu kukaa na haja ndogo kwa muda mrefu bila kwenda kujisaidia kutokana na sababu mbalimbali, hali ambayo inaelezwa kuwa ina madhara kiafya.

Mtu anaweza kuwa safarini, lakini hashuki katika magari kwenda kujisaidia pale kondakta anapotangaza kwamba sasa ni 'wakati wa kuchimba dawa'.

Vilevile, wapo watu ambao wakiwa wanafanya shughuli zao au kama wanafuatilia jambo fulani, huwa hawataki kuliacha hata pale wanapobanwa na haja ndogo huendelea nalo kana kwamba hawajabana haja ndogo.

Lakini wataalamu wa afya wanakumbusha kuwa mtu kujibana na kupuuzia kwenda haja ndogo, kuna madhara makubwa kiafya ikiwamo uwezo wa kibofu cha mkojo kujitawala kupotea.

Hivyo wale wanaofanya hivyo aidha kwa kutojua au wawe wanaojua, ni vyema wakatambua kuwa kitendo cha mtu kubanwa na haja ndogo siyo cha hiyari, bali ni lazima kwa ajili ya kulinda afya zao.

Inaelezwa, kila mtu anatakiwa kwenda haja ndogo kila baada ya saa nne hadi sita, hivyo kama ataendelea kukaa na haja ndogo kwa muda mrefu zaidi atakuwa umejiweka katika hatari kukumbwa na matatizo mbalimbali ya kiafya.

Goodluck Maiga ni mtaalamu wa mambo ya mkojo, anasema mtu anapaswa kufikiria kibofu chake kama puto lililojazwa maji kupitiliza na kwamba puto hilo likatanuka hadi mwisho wake na kuwa zito.

Kwamba kadiri mtu atakavyoendelea kubana haja ndogo ndivyo itakavyokuwa vigumu kwake kutembea hadi msalani kabla hujajikojolea, itakuwa aibu kwa mtu mzima kujikojolea.

Anakumbusha kuwa, kuna misuli inayoitwa 'pelvic' ambayo kazi yake ni kuzuia mkojo usitoke au kuuruhusu utoke katika kibofu cha mkono na kwamba mtu akiwa na mtindo wa kubana haja ndogo kwa muda mrefu, misuli hiyo inachoka na kushindwa kufanya kazi inavyotakiwa.

Kwa mantiki hiyo, anaweka wazi kuwa watu wanatakiwa kuacha kuharibu misuli hiyo kwa kubana haja ndogo bila kuwa na sababu za msingi za kuwafanya wafikie hatua hiyo ili kulinda afya zao.

Mtaalamu huyo anafafanua kuwa kwa kawaida mtu anapokaa na haja ndogo kwenye kibofu kwa muda mrefu, huwa anapata maumivu makali, ambayo huwa yanaisha mara tu pale anapokwenda kujisaidia.

Anakumbusha kwamba maumivu hayo yanaweza yakawa ndio mfumo wa maisha ya mtu mwenye mtindo wa kubana haja ndogo na kama hakuchukua hatua za kuachana na mtindo huo anaweza kuwa kwenye hatari.

Kwa upande wa tatizo la kutanuka kibofu kutokana na kubana haja ndogo mara kwa mara, anasema mwili utakuwa haumpi mtu taarifa kuwa anatakiwa kujisaidia, kwa vile umbo la kibofu limeongezeka.

Mtaalamu huyo anasema kwamba taarifa hizo, ambazo kwa kawaida hutolewa na ubongo wakati kibofu kimejaa, ni muhimu sana, lakini kibofu cha mkojo kinapotanuka humfanya mhusika asiweze kupata taarifa.

Anasema kibofu cha mkojo huwa kinafanya kazi kwa mfumo wa kujiendesha wenyewe na iwapo mtu hatakwenda kujisaidia kwa wakati anaweza kusababisha ubongo wake upate usumbufu wa taarifa za kujaa kwa kibofu.

Anasema ubongo ndio unaotuma taarifa katika kibofu na kusema mkojo uendelee kushikiliwa hadi muda fulani utakapotimia, na kwamba inaweza kufikia hatua uwezo wa ubongo kutoa taarifa hizo na pia uwezo wa vigunduzi asili ambavyo viko katika kibofu cha mkojo kupoteza uwezo wa kufanya kazi.

Kwa maelezo hayo ya kitaalam, ni wazi kwamba wale wote ambao walikuwa na mazoea ya kubana haja ndogo kwa muda mrefu watakuwa wamepata cha kujifunza ili kuepuka madhara kiafya.

Inawezekana mtu akabanwa na haja ndogo katika mazingira ambayo hawezi kupata sehemu ya kujisaidia, lakini kwa wale ambao wamekuwa na mtindo wa kujibana, ni vyema wakaachana nao.

Maana yake ni kwamba, mara mtu anapobanwa na haja ndogo kama yuko mazingira ambayo anaweza kuitoa, basi asiendelee na mambo mengine bali aitoe kwanza ndipo aendelee na kile anachofanya.

Kama anavyosema mtaalamu kwamba kubana haja ndogo siyo kitendo cha hiyari, basi hilo lichukuliwe kama lilivyo na tena kwa uzito wake kwani linaweza kumuweka mtu salama zaidi kuliko kufanya mambo kwa mazoea.

## Mbunge ataka waraka wa viwanda 100 kila mkoa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum, Sophia Mwakagenda (Chadema), amehoji bungeni uliko waraka wa serikali kuhusu mpango wa ujenzi wa viwanda 100 kila mkoa nchini.

Mwakagenda alihoji kuhusu suala hilo alipouliza swali la msingi wakati wa kipindi cha 'maswali' bungeni jijini Dodoma jana, akieleza kuwa katika kujenga Tanzania ya viwanda, Wizara ya Viwanda na Biashara imekuwa na mikakati ya muda mrefu.

"Je, mkakati wa Ofisi ya Rais - Tamisemi (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa) kujenga viwanda 100 kwa kila mkoa ni sehemu ya mkakati wa kuijenga Tanzania ya viwanda na umeainishwa kwenye waraka gani wa serikali ili kuwapa wananchi rejea ya pamoja ya kitaifa?" Alihoji.

Akimjibu mbunge huyo, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - Tamisemi, Mwita Waitara, alisema mkakati wa kujenga viwanda 100 kila mkoa ni sehemu ya mikakati mbalimbali inayotekelezwa na serikali ya awamu ya tano kujenga uchumi wa viwanda uliofungamanishwa na maendeleo ya watu.

Alisema Ofisi ya Rais Tamisemi imeandaa mwongozo wa kubainisha majukumu ya mikoa na mamlaka za serikali za mitaa katika utekelezaji wa Sera ya Viwanda.

Tangu ilipoingia madarakani Novemba 5, 2015, serikali ya awamu ya tano imekuwa ikitilia mkazo ujenzi wa viwanda nchini kwa lengo la kutoa ajira na kujenga Tanzania yenye uchumi wa kati kufikia mwaka 2025.

## KESI YA NIDA

# Korti yahoji Jamhuri siku ya kusoma maelezo mashahidi

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imeagiza upande wa Jamhuri kupeleka taarifa ya lini washtakiwa wanaokabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi akiwamo Mkurugenzi Mkuu wa zamani wa Mamlaka ya Vitambulisho (NIDA), Dickson Maimu na wenzake watasomewa maelezo ya mashahidi.

Aidha, mahakama hiyo imesema upelelezi wa kesi hiyo ulikamilika tangu Januari 29, mwaka huu na miezi sita sasa Jamhuri inapiga danadana kuwasomewa washtakiwa maelezo hayo.

Kesi hiyo inayomkabili Maimu na wenzake dhidi ya mashtaka 100 ikiwamo kutakatisha fedha na kuisababishia serikali hasara ya Sh. bilioni 1.16, ilitajwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Salum Ally.

Upande wa Jamhuri ukiongozwa na Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Leonard Swai.

Swai alidai kuwa kesi hiyo imepangwa kwa ajili ya kutajwa na mchakato wa kuandaa maelezo ya mashahidi bado haujakamilika.

Hata hivyo, upande wa Jamhuri ulidai kuwa ni mara ya nne upande wa Jamhuri unaeleza kwamba uko katika mchakato.

"Mheshimiwa hakimu, hatujui sababu zinazofanya wasimalize, waseme mahakamani ugumu wa kuwasomea washtakiwa maelezo ya awali uko wapi?" Ulidai upande wa utetezi.

Akijibu hoja za utetezi, Swai alidai kuwa kutokana na tuhuma zinazowakabili washtakiwa inachukua muda kuandaa maelezo hayo, aliomba mahakama kupanga tarehe nyingine ya kutajwa.

Hakimu alisema kesi hiyo imekamilika upelelezi miezi sita iliyopita na kila inapopangwa kutajwa Jamhuri inadai wako kwenye mchakato na kuhoji kwanini inachukua muda mrefu.

"Kwanini huo mchakato unachukua muda mrefu haukamiliki, nataka upande wa Jamhuri muwe makini ukizingatia washtakiwa wako mahabusu na kesi hii haina dhamana," alisema Hakimu Ally.

Alisema tarehe ijayo upande wa Jamhuri upeleke taarifa ya mchakato huo umefikia wapi.

Hakimu Ally alisema kesi hiyo itatajwa Juni 25, mwaka huu na washtakiwa wataendelea kukaa mahabusu.

Mbali na Maimu na Kayombo, washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Meneja Biashara wa NIDA, Aveln Momburi, Mkurugenzi wa Kampuni ya Aste Insurance Brokers, Astery Ndege, Ofisa Usafirishaji, George Ntalima na Mkurugenzi wa Sheria, Sabina Raymond.

Awali washtakiwa hao walikuwa wakikabiliwa na mashtaka 26 likiwamo la uhujumu uchumi, Januari 28, 2019 waliachiwa huru na mahakama hiyo baada ya Mkurugenzi wa Mashitaka (DPP) kusema hana nia ya kuendeleza mashtaka dhidi yao.

Hata hivyo, baada ya washtakiwa kuondolewa mashtaka hayo na kuachiwa huru walikamatwa tena na kufikishwa katika mahakama hiyo kisha kusomewa mashtaka mapya 100 yakiwamo 25 ya utakatishaji fedha.

Washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka 22 ya kughushi, mashtaka 43 ya kutumia nyaraka kwa lengo la kumdanganya mwajiri, mashtaka mawili ya kula njama, 25 ya kutakatisha fedha na matano ya kuisababishia hasara NIDA.

Pia washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka mawili ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na shtaka moja la matumizi mabaya ya madaraka, lipo moja ambalo linamkabili Maimu na Sabina.

Katika shtaka ya kwanza la kula njama, Maimu, Ndege na Ntalima wanadaiwa, kati ya Julai 19, 2011 na Agosti 31, 2015 wakiwa maeneo tofauti ndani ya Jiji la Dar es Salaam, walikula njama ya kufanya udanganyifu wa Sh. bilioni 1.175 dhidi ya NIDA.



Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan akifungua maadhimisho ya miaka 10 na Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Umoja wa Urejeshaji wa mali zinazohusiana na Uhalifu (ARINSA), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: OMR**

# Polisi waua watuhumiwa ujambazi, mmoja akutwa na bunduki ya kivita

**Na Allan Isack,** ARUSHA

JEAHI la Polisi mkoani Arusha kwa kushirikiana na kikosi maalumu wamewaua watu wawili wakituhumiwa kuwa majambazi sugu.

Watu hao waliuawa katika majibizano ya kurushiana risasi na askari polisi katika Milima ya Digodigo, Kata ya Digodigo Wilayani Ngorongoro.

Kamanda wa Polisi mkoani Arusha, Jonathan Shana, alisema tukio hilo lilitokea Juni 11, mwaka huu, majira ya usiku, na kuwa waliuawa baada ya polisi kuwazidi nguvu.

Alisema walikuwa wakitafutwa kwa muda mrefu kwa tuhuma za unyang'anyi, utekaji wa watalii, wafanyabiashara na wachuuzi wa mifugo wa ndani na nje ya nchi.

Alisema kuwa watu hao walikuwa wakifanya uhalifu kwenye maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Ngorongoro.

Shana alisema katika ukio la majibizano ya risasi kati yao na polisi lilichukua takribani dakika 75 hadi walipowaua.

Alisema katika mapambano hayo, jambazi mmoja alifanikiwa kutoroka huku akiwa na majeraha mengi mwilini.

Aidha alisema katika upekuzi wa kina mmoja aliyefariki alikutwa na bunduki moja aina ya AK 47, ikiwa na magazini 20.

Alieleza kuwa majambazi hao walitambuliwa kwa majina ya Kulima Albert maarufu kwa jina la Ndemesha na Hashimu Nginodya maarufu kwa jina la Morinyo wote ni wakazi wa Kijiji cha Digodigo.

## Mtoto aliyekaa ICU

INATOKA UK. 3

Alisema gharama za matibabu ni zaidi ya Sh. milioni 17 ambazo hospitali imezilipa kwa mtoto huyo.

"Sio kwamba bibi yake ameweza kulipa hizo gharama sisi tuliangalia kumtibu kwanza na hospitali imetoa msamaha wa gharama za matibabu. Matibabu yake yalikuwa ni makubwa kwa upande wa dawa ambayo dozi moja ni Sh 700,000 kwa siku utaona matibabu ya ICU yalivyo na gharama kubwa," alisema.

Pia alisema hospitali hiyo imempatia msaada wa kiti mwendo kwa ajili ya kumsaidia kutembelea chenye gharama ya Sh. 450,000.

Mkuu wa ICU, Baraka Elisha, alisema wakati wanampokea mtoto huyo mwili wake ulikuwa hauna nguvu huku akishindwa kupumua na walimwekea mashine ya kumsaidia kupumua.

Alisema baada ya kupita miezi mitatu alitolewa katika mashine hiyo na kuendelea na matibabu mengine ikiwamo kufanyishwa mazoezi na kuhamishiwa katika wodi ya kawaida.

Bibi wa mtoto huyo, Patricia Hilary, alishukuru hospitali hiyo kwa msaada mkubwa waliompatia kwa kuwa madaktari walijitahidi kupambana na afya ya mtoto huyo na hatimaye kuruhusiwa kutoka.

Alisema wapo ambao walimkatisha tamaa kwa madai kuwa mtoto huyo hawezi kupona, hivyo anamshukuru Mungu aliyewatumia madaktari hao kumponya mjukuu wake.

Bibi huyo alijikuta anatokwa na machozi kila mara baada ya kusikia amesamehewa deni lake pamoja na kupatiwa msaada wa kiti cha kutembelea mtoto huyo.

## Awatuhumu polisi kumpora zaidi ya mil.1/-

INATOKA UK. 2

baada ya uchunguzi RCO akaamua kuwa askari hao wasirudishe fedha na akachukua simu yangu kuwa wanaifanyia uchunguzi, nilisubiri majibu kila nikipiga simu kwa Christopher hapokei."

Alidai kuwa kutokana na hali hiyo aliamua kurudi Dar es Salaam na kuomba vyombo husika kufuatilia ili arudishiwe fedha zake Sh. 1,188,000 pamoja na alizotumia kusubiri wakati wote kiasi cha Sh. 990,000.

Kamanda wa Polisi mkoani humo, Jumanne Muliro, alipopigiwa simu na Nipashe kuhusu madai hayo, alisema kama mtu huyo ameona njia sahihi ya kuwasilisha malalamiko yake ni vyombo vya habari, wanasubiri barua hiyo ili waijibu."Malalamiko ni haki ya mwananchi, amefungua kesi amepewa RCO, lakini ameamua kumwandikia barua IGP, tutamjibu," alisema Kamanda Muliro.

Hata hivyo, Kamanda Muliro alisema hafahamu kama aliwahi kuwasiliana na mtu huyo kwa sababu kwa siku anapigiwa simu na watu wengi siyo rahisi kuwakumbuka wote.

"Kama anadai nilimkabidhi wa RCO, inawezekana ikawa kweli au siyo kweli kwasababu ninaongea na watu wengi, ila kama ni kweli sijajua ni hatua gani za kiuchunguzi zimefikia," alisema.

Nipashe ilipomtafuta Sajenti Christopher ili kujua kama anafahamu suala hilo, alisema hafahamu tukio hilo wala mtu huyo na kumuomba aende Mwanza ili wakutane amuone.

"Yeye anasema alikuwa Mwanza akaondoka, aje Mwanza sizijui habari hizi unazoniambia kama kulikuwa na mkwamo kwa nini asirudi kwa RPC, simfahamu wala kesi siifahamu," alisema.

## Marais nchi 16 kuhudhuria SADC

INATOKA UK. 3

atakuwa Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri wa nchi za nje kwa kipindi hicho.

Prof. Kabudi alisema mkutano huo utakuwa mwanzo wa mingine itakayokuwa ikifanyika mfululizo Tanzania ikihusisha sekta mbalimbali hadi kukamilika kwa uenyekiti wa Rais Magufuli.

"Mkutano mwingine kama huu utafanyika tena Tanzania miaka 16 ijayo. Ndio maana tukio kama hili la kihistoria huwezi kulifanya bila kushirikiana kikamilifu na vyombo vya habari, tutakuwa na semina mbalimbali za waandishi wa habari watakao ripoti mkutano," alisema.

Pia alilishukuru Shirika la Maendeleo la Ujerumani kwa kukubali kutoa fedha za kuendesha semina hizo zitakazofanyika nchini.

"Ninajua ndani ya taaluma hii wapo wabobezi, magwiji wapo ambao naamini watatoa mada ili tuweze kuwahabarisha Watanzania mkiwa mmefahamu mambo ya SADC," alisema.

Prof. Kabudi alisema Tanzania kuwa mwenyekiti wa mkutano huo ni jambo kubwa hasa kwa sababu historia inaonyesha kabla na baada ya uhuru, nchi ilibeba jukumu la kusaidia nchi za Afrika Mashariki, Afrika ya Kati na Kusini mwa Afrika katika harakati za kupigania uhuru na ukombozi.

"Mkutano huu una umuhimu mkubwa kwa nchi hizi kwa sababu zinarudi katika nchi iliyowasaidia kupigania ukombozi wa nchi zao na kuwarejeshea heshima. Mwenyekiti wa sasa wa SADC ni Rais wa Namibia, Hage Geingob ambaye ameanza Agosti 2018 hadi Agosti mwaka huu," alisema.

Pia alisema kwa sababu Tanzania ni miongoni mwa waasisi wa SADC, nchi za Kusini mwa Afrika zimependekeza wakati wa shughuli hiyo wafanye kumbukizi ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere na miongoni mwao sasa ni wazee. Prof. Kabudi aliomba vyombo vya habari visaidie kuhamasisha kuhusu SADC, kuelimisha wafanyabiashara kuchangamkia fursa zitakazotokana vikao hivyo.

Kadhalika, alisema wapo baadhi ya viongozi wa Afrika ambao walikaa Tanzania na amewaomba waandishi wa habari, kutafuta nyumba walizokaa kipindi hicho ili kuwakumbusha waafrika.

Kuhusu lugha ya Kiswahili, Prof Kabudi aliwataka waandishi wa habari kupendelea kusoma kamusi kwa sababu kumekuwa na Kiswahili cha ukakasi kilichopungukiwa utajiri.

Mkurugenzi wa Idara ya Habari (Maelezo), Dk. Hassan Abbasi, ambaye pia ni Msemaji Mkuu wa Serikali alisema wanahabari wapo tayari kutangaza yote yanayohusu SADC kwa sababu wanawajibu kitaaluma.

Katibu Mtendaji wa Wamiliki wa Vyombo vya Habari nchini (MOAT), Henry Muhanika, alisema inapotokea fursa ya matangazo vyombo vya habari binafsi navyo vipewe.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, aliwaomba wakazi wa Dar es Salaam kuongeza kazi ya kampeni za usafi ambazo zimekuwa zinafanyika.

## Waziri aliyetumbuliwa afunguka

INATOKA UK. 3

nchi kutekeleza ajenda ya viwanda na biashara.

"Mheshimiwa Waziri hii ni dhamana kubwa jukumu kubwa limekasimiwa kwako na Rais na Watanzania maana ndio waliomchagua Rais na kwa sababu Watanzania wana mategemeo makubwa na Rais na Rais ana mategemeo makubwa na hii wizara kwa kweli kama ulivyosema Ikulu na wewe ulikuwepo ulitoa ahadi kwa Watanzania kuwa hutawaangusha,"alisema.

Aliwataka kusimamia ahadi hiyo kwa kuwa Rais na Watanzania wote wana mategemeo na wizara hiyo.

"Katibu Mkuu, wakuu wa idara na wafanyakazi wa wizara hii msijisahau nyinyi mnaandika historia ya nchi hii kwa hiyo msijisahau, msaidie Waziri aweze kutimiza matarajio ya Rais," alisisitiza.

Aliongeza: "Jitahidini mpeni 'briefing' pale anapotaka msimpangie kwamba tutakupa 'briefing' kesho, siku ina saa 24 msiseme muda wa leo wa kazi umeisha akihitaji saa kumi 'briefing' mpeni 'briefing' ili aweze kutaraji aweze kutimiza matarajio ya Watanzania na matarajio ya Rais."



Joseph Kakunda

"Mimi ni Mbunge wa Sikonge, Katibu mkuu hapa anamung'unya maneno, Waziri mstaafu hakuna cheo cha Waziri mstaafu kwa kuwa sisi hatustaafu unapewa uwaziri na unaondolewa huwa hakuna kustaafu, kwa hiyo mimi unaweza kuniita Waziri wa zamani," "Mimi ni Mbunge kupitia CCM najivunia hilo kwenye mkutano mkuu napata nafasi ya kuihoji serikali, Baraza la Madiwani, napata nafasi ya kuihoji serikali, bungeni pia napata nafasi ya kuihoji na kuishauri serikali nzima."

Kadhalika, Kakunda alisema wafanyakazi wa wizara hiyo ni watu watulivu sio walalamikaji wala wapiga kelele.

"Nilivyofika hapa gari la Katibu Mkuu lilikuwa haliwezi kufika Dar es Salaam bila ya kupata hitilafu njiani, yaani mpaka Katibu Mkuu alikuwa akiishi katika mazingira magumu ya kazi, kwa hiyo hapa katika wizara hii yapo yaliyofanyika kwa kushirikiana na serikali kuyaweka vizuri ndio maana hata gari lako Waziri ni gari jipya," alisema.

Alisisitiza suala la utawala bora na kuwataka kuwahudumia wananchi bila kuwambia njoo kesho

### BASHUNGWA ATAJA MIKAKATI YAKE

Alisema haamini katika kushindwa na kuwataka watumishi wake kuhakikisha hamuangushi Rais Magufuli na Watanzania kwenye kufikia uchumi wa kati.

"Hili deni kubwa sana Rais na Watanzania na Rais alisema nakupa pole sio kukupongeza, sasa na mimi ile presha niliyopata nashusha kwenu ninachoweza kusema 'team work' ndio key ya kumsaidia Rais na kufika uchumi wa viwanda na kipato cha kati,"alisema.

Aliongeza "Tuchapa kazi hakuna linaloshindikana ,Tanzania inawezakana kuwa net doner badala ya kuwa dependent na misaada... Shukrani Mheshimiwa Kakunda umefanya jambo la kiungwana umenikabidhi ofisi kwa upendo umenipa ushauri ,na nyaraka ulizonipa nitasoma nikuhakikishie ushauri wako nitaufanyia kazi, sina cha kukupa zaidi ya kusema umenisaidia kuanza vizuri."

## Macho, bungeni

INATOKA UK. 2

kuhusu hoja hizo yalikuwa yanaendelea kabla ya kuwasilishwa kwa makadirio ya bajeti ya mwaka ujao.

Alizitaja hoja hizo kuwa ni pamoja na changamoto zilizojitokeza katika ugawaji wa vitambulisho vya wajasiriamali na malimbikizo ya madeni kwa watumishi wa umma, makandarasi na watoa huduma, utoaji taulo za kike shuleni bila malipo.

Hoja nyingine ni kudorora kwa biashara ya ngozi nchini na pendekezo la kupunguza Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa viwanda vya ndani.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, anatarajiwa kujibu hoja hizo leo atakapowasilisha bungeni makadirio ya bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha.

MAONI YA WABUNGE

Mbunge wa Busega, Raphael Chegeni (CCM), alisema anatarajia kuona serikali ikija na mkakati wa kuongeza idadi ya walipakodi nchini.

Alisema Tanzania ina zaidi ya watu milioni 50, lakini walipa kodi ni milioni 2.4 tu, jambo linalotoa ishara kwamba hakuna mwamko wa wananchi katika ulipaji kodi.

Mbunge wa Mlalo, Rashid Shangazi (CCM), pia alizungumzia suala hilo, akieleza kuwa anatarajia Mamlaka ya Mapato (TRA) itaachana na mfumo wa kikoloni wa kukusanya kodi kwa mtutu na kujikita katika kutoa elimu kwa umma juu ya umuhimu wa kulipa kodi.

Mbunge wa Manonga, Seif Gulamali (CCM), alisema anatarajia kuona bajeti ya nne ya serikali ya awamu ya tano ikijikita katika utekelezaji wa miradi muhimu kwa wananchi ikiwa ni pamoja na ujenzi wa barabara, ufuaji wa umeme wa maji katika Mto Rufiji, maarufu Stiegler's Gorge na miradi ya maji.

Mbunge wa Momba, David Silinde (Chadema), alisema anatarajia serikali itawasilisha bajeti yenye mikakati ya kuongeza ajira na uzalishaji ambao anaamini utaongeza makusanyo.

Silinde ambaye pia ni Waziri Kivuli wa Fedha na Mipango, alisema asilimia 60 ya makusanyo ya kodi nchini yanatokana na Kodi ya Lipa Kadri Unavyopata (PAYE) ambayo wafanyakazi wanakatwa kwenye mishahara yao.

"Tukitengeneza mazingira ya kuongeza uzalishaji, tutazalisha ajira nyingi na hao watakaoajiriwa watalipa kodi kwa serikali," alisema.

Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mara, Agnes Marwa (CCM), alisema anatarajia bajeti mwaka ujao wa fedha itajikita katika kutekeleza ahadi ya serikali ya kumtua mama ndoo kichwani kwa kutekeleza miradi ya maji.

Marwa pia aliomba serikali kukamilisha mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara ambao umesimama kwa muda mrefu.

# Waziri amwagiza mhandisi mshauri bandarini D'Salaam

**Na Enock Charles.**

WAZIRI wa Ujenzi , Uchukuzi na Mawasiliano , Mhandisi Isaack Kamwele, ametoa maagizo kwa mhandisi mshauri wa bandari ya Dar es Salaam kufanya manunuzi ya haraka ya vifaa vya kupakulia mizigo katika meli zinazoingia katika Bandari ya Dar es Salaam.

"Upakuaji wa meli unatakiwa pia kuwapo na vyombo, yale makreni ya kushusha mizigo na kuhakikisha kwamba tunakuwa na efficiency (ufanisi) wa kuitoa mizigo katika bandari yetu kwenda kwenye maeneo inakotakiwa " Kamwele alisema Akizungumza katika uzinduzi wa gati namba moja kati ya nane ambazo zinaendelea na ujenzi katika bandari ya Dar es Salaam, Waziri Kamwelwe alisema lengo la Serikali ni kuondoa vikwazo ili kuwavutia wawekezaji wa ndani na nchi jirani kuitumia bandari hiyo.

"Na mimi kazi yangu ndugu zangu ni kuhakikisha naondoa vikwazo vyote vikiwamo vya kodi isiyo na msingi ndiyo maana delivery order fee nimeitoa," alisema na kuongeza: "Kontena mtu alikuwa analipa dola 70 hadi 150, kodi ambayo wala haiingii kwenye Serikali, Striping fee nimeitoa ,escot fee nimeitoa na bado naendelea na kodi zingine." Gati hilo lenye urefu wa mita 191 na kina cha mita 15 limeelezwa kuwa na uwezo wa kupokea meli kubwa yenye kontena 4,000 hadi 6,000, hivyo kuwezesha bandari hiyo kupokea meli nyingi na zenye mzigo mkubwa.

Mradi huo wa ukarabati wa magati nane katika bandari hiyo umegharimu Sh. bilioni 968 na unatarajiwa kukamilika Juni mwakani ambapo mpaka sasa zimeshatumika Sh. bilioni 337, na fedha hizo pia zitatumika kununua vifaa vitakavyotumika kushusha na kupakia mizigo katika meli.



Mwenyekiti wa Kamati ya Usajili ya Klabu ya Simba, Zakaria HansPope na viongozi wa klabu ya Simba SC, Evans Aveva na Godfrey Nyange (Kaburu), wakiwa chini ya ulizi wa askari magereza katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam jana, kusikiliza kesi inayowakabili. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Majaliwa akaribisha wawekezaji wa Rwanda

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewakaribisha wawekezaji kutoka Rwanda waje wawekeze katika sekta mbalimbali na kwamba serikali itawapa ushirikiano wa kutosha.

Aliyasema hayo alipokutana na kufanya mazungumzo na Spika wa Bunge la Rwanda, Donatille Mukabalisa, ofisini kwake bungeni jijini Dodoma.

Alisema serikali ipo tayari kuwapokea wawekezaji kutoka katika nchi hiyo, ili waje kuwekeza katika sekta mbalimbali zikiwamo za viwanda, kilimo, madini na utalii.

Kadhalika, Waziri Mkuu alisema Tanzania na Rwanda ni nchi zenye uhusiano mzuri, hivyo alimwakikishia Spika Donatille kwamba serikali itauimarisha uhusiano huo.

Majaliwa alisema serikali inatekeleza mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) ambao utarajiwa kusaidia katika usafirishaji wa mizigo kwenda hadi Rwanda.

Naye, Spika Donatille alishukuru Serikali ya Tanzania kwa ushirikiano mkubwa inaoutoa kwa Serikali ya Rwanda, hivyo kumhakikishia Waziri Mkuu kwamba watauendeleza.

Spika huyo alisema ushirikiano wa Tanzania na Rwanda ni muhimu katika uchumi kwa kuwa wanatumia Bandari ya Dar es Salaam katika kusafirisha asilimia kubwa ya mizigo yao.

# Ashauri shoroba ziwe hifadhi za taifa

**Na Salome Kitomari**

KAMISHNA wa Uhifadhi katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCA), Dk. Freddy Manonga, amesema upo umuhimu wa maeneo ya mapito ya wanyama kuwa chini ya mamlaka za uhifadhi kwa ulinzi zaidi.

Aidha, alisema yakiachwa kama yalivyosasa upo uwezekano wa kutoweka kabisa na ifikapo 2030, wanyama watashindwa kupita kutoka hifadhi moja kwenda nyingine na maeneo ya mtawanyiko.

"Ningeshauri yawe Hifadhi za Taifa, chini ya NCA au Mamlaka ya Usimamizi wa wanyamapori (Tawa) kama maeneo yaliyohifadhiwa," alishauri.

Kamishna huyo alizungumza na waandishi wa habari wa Tanzania na Thailand, walio kwenye programu maalum iliyoandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira (Jet) kwa ufadhili wa Shirika la Misaada la Marekani (USAID).

Kwa mujibu wa Dk. Manonga, tathmini ya hivi karibuni iliyofanywa na NCA, ilibaini kuwa maeneo ambayo kwa kiasi kikubwa bado yanatunzwa vizuri ni hifadhi za taifa.

"Nadhani kama tunataka kulinda shoroba kwa ukuaji endelevu wa hifadhi na wanyama, tuzibadilishe ziwe hifadhi za taifa, hata chini ya NCA ambao wameweza kulinda vizuri," alisema.

Alibainisha kuwa shoroba nyingi ni za Tawa na kwamba zipo ambazo zipo ndani ya hifadhi hivyo zipandishwe hadhi ziwe 'Game Reserve'.

Aidha, alisema idadi ya watu inavyoongezeka mahitaji ya ardhi ni makubwa na kwamba miaka 30 ijayo maeneo yaliyohifadhiwa yatakuwa yamezibwa na hakutakuwa na shoroba.

"Ninavyoona tunavyokwenda, idadi ya binadamu na mahitaji ya ardhi miaka miaka 30 ijayo naona hifadhi za taifa, maeneo yaliyohifadhiwa na NCA hazitakuwapo na nyingine kuwekewa uzio kama Afrika Kusini na Botswana," alifafanua.

Alisema ni lazima kuchukua hatua za haraka kama Tanzania inataka kuwa na shoroba na maeneo ya mtawanyiko wa wanyama.

Aidha, alisema serikali inafikiria uwezekano wa kuendelea kuyalinda maeneo ya 'Game Control Area' na ndiyo maana eneo la Loliondo litaingizwa ndani ya NCA.

Alisema kuna eneo la Ziwa Natron ambalo serikali inataka kulifanya kuwa oevu linalolindwa pamoja na Kilombero Game Controlled Area ambalo sehemu yake watapewa wananchi ili kuweka ulinzi imara. Utafiti uliofanywa na Tawa mwaka 2009, uvamizi wa shoroba umesababisha wanyama kuuawa, uwindaji haramu na kusambaa kwa magonjwa ya wanyamapori kwenda kwa wanyama wa kufugwa na kinyume chake.

Shoroba zilizo hatarini kutoweka ni Manyara hadi Ngorongoro inayojulikana kama Kitete-Salela inayoziunganisha hifadhi za Serengeti, Ngorongoro, Ziwa Manyara na Tarangire ambako wanyama huelekea hadi Ziwa Natron.

Kwa mujibu wa utafiti wa mwaka 2009, shoroba hiyo ilibakiza chini ya miaka miwili kufunga na wanyama kuacha kupita kutokana na shughuli za kibinadamu kama kilimo na makazi.

Shoroba ya Udzungwa hadi Mikumi inayounganisha maeneo yaliyohifadhiwa ya mapori ya Akiba ya Muhesi, Kizigo, Rungwa, Ruaha, Usangu, Rukwa na Katavi iligundulika kuwa na hali mbaya na ingefungwa.

Shoroba ya Tarangire hadi Manyara, maarufu kama Kwakuchinja, iliyounganisha wanyama wa hifadhi ya Tarangire na mapori ya Akiba, iligundulika kuwa katika hali mbaya ikibakiza miaka miwili kufa na sababu kubwa ni shughuli za kibinadamu na uwindaji.

Utafiti pia ulibaini shoroba ya Tarangire-Simanjiro, inayounganisha wanyama kutoka maeneo yaliyohifadhiwa ya Tarangire, Loikisale, Emboret, Mkungunero na Simanjiro (ambako wanyama huzaliana), ilikuwa na hali mbaya na iwapo shughuli za kibinadamu zingeendelea kwa kasi hiyo ingefungwa 2011.

Nyingine zilizokuwa katika tishio ni Kilimanjaro - Amboseli, maarufu kama Kitendeni, inayounganisha wanyama kutoka hifadhi ya taifa nchini Kenya ya Amboseli na kuingia hifadhi za taifa za Kinapa, Arusha hadi Pori la Tengefu la Loliondo.



Spika wa Bunge, Job Ndugai (kushoto), akiagana na Spika wa Bunge la Rwanda, Mukabalisa Donatille, wakati akisafiri kurudi nchini kwake, Rwanda, katika kiwanja cha ndege, jijini Dodoma jana, baada ya kumaliza ziara ya kikazi ya siku tatu jijini humo, ambapo alitembelea sehemu mbalimbali ikiwamo Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Chuo Kikuu cha Dodoma. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Bil. 83/- kutumika uchaguzi wa mitaa

BUNGE limeelezwa kuwa kiasi cha Sh. bilioni 82.9 kimetengwa kwa ajili ya kuendesha uchaguzi wa serikali za mitaa na kwa sasa maandalizi ya ununuzi wa vifaa vya uchaguzi yanaendelea.

Hayo yalielezwa jana bungeni na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa(TAMISEMI), Mwita Waitara, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mtambale (CUF), Masoud Abdallah Salim.

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema mwaka 2019 utafanyika uchaguzi wa serikali za mitaa kwa mujibu wa sheria na kuhoji serikali ina mkakati gani unaoendelea katika maandalizi ya mchakato wa uchaguzi huo.

Waitara akijibu swali hilo, alisema tayari serikali imehakiki maeneo ya utawala na kufanya mafunzo na mikutano kwa wadau wa uchaguzi huo.

"Ili kuhakikisha uchaguzi huu unafanyika kwa ufanisi Serikali imekamilisha maandalizi ya kanuni za uchaguzi zitakazotumika kuendesha uchaguzi huo," alisema.

Alieleza kuwa kanuni hizo zimetangazwa katika gazeti la serikali Aprili 26, mwaka huu kwa kupewa namba 372 na kwamba kanuni za uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mtaa na wajumbe wa kamati ya mtaa katika mamlaka za miji.

Alifafanua kuwa tangazo Namba 371 linalohusu kanuni za uchaguzi wa Mwenyekiti wa kitongoji katika mamlaka za miji midogo, Tangazo Namba 373 linalohusu kanuni za uchaguzi wa Mwenyekiti wa kijiji, wajumbe wa halmashauri ya kijiji na mwenyekiti wa kitongoji katika mamlaka za wilaya.

"Tangazo namba 374 linahusu kanuni za uchaguzi wa mwenyekiti wa kijiji, wajumbe wa halmashauri ya kijiji na mwenyekiti katika mamlaka za miji," alisema.

# Ndalichako: Kiingereza bado lugha ya kufundishia

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imesema bado inatumia lugha ya Kiingereza katika kufundishia na kujifunzia katika ngazi ya elimu ya sekondari, vyuo vya kati na vikuu.

Sababu ya kutumia lugha hiyo inalenga kuwajengea ufahamu na umahiri wa lugha kwenye masuala ya kitaifa, kikanda na kimataifa kwa mawasiliano na biashara.


Kauli hiyo ilitolewa jana bungeni na Waziri wa Wizara hiyo, Prof.Joyce Ndalichako, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Tabora Kaskazini (CCM), Almas Maige, ambaye katika swali lake alisema miaka iliyopita Serikali ilikuwa na nia ya kutumia Kiswahili kama lugha ya kufundishia katika shule za msingi na upili. Alihoji nini kilitokea kwa serikali kutekeleza nia yake hiyo nzuri.

"Je, ni lini itaanza kutumia kiswahili kama lugha ya kufundishia katika shule za msingi na upili ili kukuza uelewa wa wanafunzi katika masomo yao?"alihoji.

Akijibu maswali hayo, Prof. Ndalichako alibainisha kuwa suala la matumizi ya lugha ya kufundishia na kujifunzia ni la kisheria kama sheria ya elimu sura 353 inavyoelekeza.

"Sheria hii inabainisha matumizi ya lugha mbili za kufundishia na kujifunzia ambazo ni Kiswahili na Kingereza na kwa sasa lugha ya Kiswahili inatumika kufundishia katika ngazi ya elimu ya awali na msingi, vyuo vya ualimu ngazi ya cheti na vyuo vya ufundi," alisema.

Prof. Ndalichako alisisitiza serikali bado inatumia lugha ya Kiingereza katika kufundishia na kujifunzia katika ngazi ya elimu ya sekondari, vyuo vya kati na vikuu.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA

# 'Biashara ya upatu bandia'

NAIBU Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, amesema biashara ya upatu 'Pyramid Scheme' sio biashara halali, hivyo hakuna mtu au taasisi yoyote yenye leseni ya kufanya biashara hiyo.

Kutokana na hilo, kampuni au watu binafsi wanaojihusisha na biashara hiyo wanavunja sheria na watakapobainika hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Dk. Kijaji alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Munira Mustapha Khatib, ambaye alisema kumekuwa na biashara haramu za mitandao maarufu kama Pyramid Schemes ambazo zimeshamiri sana miji ya Arusha, Dar es Salaam na Mwanza.

Mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani kudhibiti biashara hizo ambazo zimekuwa na athari kubwa kwa uchumi wa taifa, ni kampuni ngapi za aina hiyo zimeingia nchini na kupata kibali cha kuziendesha.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri huyo alisema kwa mujibu wa Sheria ya Makosa ya jinai sura namba 16, kifungu cha 171A, 171B na 171C, biashara hiyo ni haramu na huendeshwa kinyume na sheria na taratibu za nchi.

Alieleza kuwa katika kudhibiti biashara hiyo serikali huchukua hatua dhidi ya wahusika kama ilivyofanya kwa taasisi ya DECI na serikali itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu ubaya na madhara ya biashara ya upatu.

"Juni 14 mwaka 2017 Benki Kuu ya Tanzania(BOT) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), ilitoa taarifa kwa umma kuhusu madhara ya biashara hiyo ili kuhimiza wananchi kutoa taarifa kwenye vyombo vinavyohusika pindi wanapopata taarifa ya baadhi ya watu au taasisi kujihusisha na biashara ya upatu," alisema.

Katika swali la nyongeza, Mbunge huyo alisema pamoja na serikali kudhibiti biashara hiyo bado kuna wanaoendelea.

"Je, Serikali ina mpango gani kuwasaidia waathirika wakuu ambao ni kinamama na vijana na Serikali ina mpango gani kuwapa mikopo yenye riba nafuu ili waachane na biashara hiyo," alihoji.

Dk. Kijaji akijibu maswali hayo, alisema washiriki wa biashara hiyo haramu wote wana makosa na hawatakiwi kusaidiwa zaidi ya kupata adhabu na tayari kanuni za kuwasaidia kinamama kwa kuwapa mikopo yenye riba nafuu zitakamilika Julai mosi mwaka huu ili kuanza kutumika.

Naibu Waziri huyo aliwaasa kinamama na vijana wanaojihusisha na biashara hiyo ya upatu waache na badala yake wachukue mikopo yenye riba nafuu ili kuendesha maisha yao.

# Mamia vijana waunganishwa fursa za ajira

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

ZAIDI ya vijana 100 kutoka mikoa mbalimbali wameunganishwa na fursa za ajira katika kampuni, viwanda, na mashirika mbalimbali na kujikwamua kiuchumi kulikowakabili muda mrefu kutokana na ukosefu wa ajira.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi wa Shirika la JIVITA Foundation, Raymond Mashambo, ambaye shirika lake linalofanya kazi na vijana walioko shuleni na wasiokuwa shuleni katika kutatua changamoto zinazowakabili hususan katika suala la ajira, wakati wa mafunzo ya siku mbili yaliyolenga kuwajengea uwezo vijana namna ya kujiajiri kupitia fursa mbalimbali za ajira zilizopo.

Mashambo alisema vijana hao wamenufaika na fursa hiyo ya ajira tangu kuanzishwa kwa shirika hilo mwaka 2011, ambapo vijana hao walikuwa wamemaliza vyuo mbalimbali, huku wakikosa ajira.

Aliongeza kuwa, wametoa mafunzo mbalimbali yakiwamo ya ujasiriamali, stadi za kazi kwa vijana zaidi ya 500, huku kati ya hao vijana 80 wamejiajiri wenyewe katika sekta mbalimbali ikiwamo ufundi, usafirishaji na shughuli nyingine ambazo zimewawezesha kujipatia kipato badala ya kukaa vijiweni bila shughuli zozote.

"Vijana wengi wanaomaliza vyuo vikuu wamekuwa wakilalamikia changamoto ya ajira wanapohitimu masomo yao na kuishia kukaa mtaani bila shughuli yoyote, hivyo sisi tumekuwa tukiwaunganisha vijana hao na fursa mbalimbali za ajira kulingana na kile walichokisomea na tumewasaidia vijana wengi sana lengo kubwa likiwa ni kuona kila kijana anajipatia kipato mwenyewe," alisema Mashambo.

Alisema vijana hao wamekuwa wakiwezeshwa na mradi wa "mwendo kasi "uliopo chini ya shirika hilo kupitia kampeni ya "ongea na mimi "katika kuangalia fursa zilizopo katika maeneo mbalimbali na kuwawezesha vijana kuajiriwa ama kujiajiri wenyewe.

Nao baadhi ya vijana wakizungumzia changamoto zilizopo katika kupata ajira, Jonas Mollel kutoka Sakina, alisema changamoto kubwa iliyopo ni kuwapo kwa elimu ndogo kwa vijana hali inayopelekea kufanya mambo mbalimbali kwa kukurupuka bila kupata muongozo wowote.

Aidha, waliomba wadau na serikali kuwatambua vijana kwa kuwapatia semina mbalimbali jinsi ya kujiajiri pamoja na kuanzishwa kwa vikundi vya vijana ambavyo vitawezeshwa na wadau hao ili kuondokana na changamoto.

Naye Rebecca John kutoka Tengeru, alisema changamoto kubwa iliyopo kwa vijana wengi ni kusubiria kuajiriwa huku wengi wao hawataki kujiajiri.



Kiongozi wa Mbio za Mwenge Kitaifa, Mzee Mkongea Ally, akiwa na Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro (kulia), wakipitia moja ya jalada la Mradi wa Maji wa Majengo wenye thamani ya Sh. milioni 754, ambao ulipaswa kuwekewa jiwe la msingi, wilayani humo juzi, lakini halikuwekwa kutokana na kutoridhishwa na thamani halisi ya pesa. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Watumishi wa umma wafundwa kuhusu matumizi ya mitandao

**Na Woinde Shizza ,**
ARUSHA

WATUMISHI wa umma wameombwa kutumia mitandao ya kijamii vizuri, ili kujenga taifa bora lenye uadilifu na kuonya wanaotumia mitandao hiyo kuchafua viongozi wao na kuvuruga amani.

Hayo yamesemwa jana na Kiongozi wa mbio za Mwenge kitaifa 2019, Mzee Mkongea Ali, wakati akihitimisha ziara ya Mwenge wa Uhuru katika Halmashauri ya Arusha DC wilayani Arumeru, ambapo jumla ya miradi nane ilikaguliwa.

"Nawaomba wafanyakazi wa serikali muache kutumia mitandao ya kijamii vibaya, badala yake tumieni vizuri kuelimisha watu wanaowazunguka, mambo mema yenye maadili na kunufaisha taifa letu," alisisitiza.

Alisema baadhi ya watumishi wa serikali wanaonywa na viongozi wao, lakini badala ya kubadilika wanaanza kumuandikia vijembe kwenye status pamoja na mitandao mingine ya kijamii, kitu ambacho sio kizuri.

Aidha, alisema miradi yote iliyotembelewa na Mwenge wa Uhuru katika halmashauri hiyo imekidhi vigezo vinavyotakiwa ambapo pia ametoa maelekezo na ushauri wa namna bora ya kuboresha miradi hiyo ili ilete tija zaidi inayokusudiwa.

Aliipongeza halmashauri hiyo pamoja na viongozi wake wakiongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, kwa jinsi wanavyoisimamia miradi hiyo kwa weledi na aliwasihi waendelee hivyo hivyo .

Miradi nane iliyotembelewa katika halmashauri hiyo ni miradi wa ufugaji nyuki, maji, shule na ufunguzi wa kiwanda cha mbegu na dawa .

# Waziri atoa neno magonjwa mlipuko

**Na Zanura Mollel,** ARUSHA

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, amewataka wananchi kutoa taarifa kwa wakati juu ya magonjwa ya mlipuko yanapoingia katika maeneo yao ili serikali ichukue hatua haraka.

Alisema hayo kwenye uzinduzi wa majaribio ya kudhibiti magonjwa ya mlipuko uliofanyika juzi katika mpaka wa Namanga kati ya Tanzania na Kenya hususani.

"Magonjwa haya wananchi ndio wadau wakubwa wa kutoa taarifa kwa wahusika, hakuna kiongozi anaweza kubaini kuwapo kwa ugonjwa pasipo mwananchi kutoka ndani ya jamii kutoa taarifa," alisema Ummy.

Alisema kupitia zoezi hilo la maandalizi juu ya kudhibiti magonjwa ya mlipuko, wanachokiangalia ni kujitathmini kama kuna vifaa tiba vya kutosha, kuwapo kwa wataalamu wanaoweza kuwahudumia magonjwa pindi magonjwa hayo yanapotokea.

Alieleza kuwa zoezi hilo litaleta picha halisi ya namna nchi hizo mbili zilivyojipanga huku akitolea mfano wa kuwapo kwa ugonjwa wa ebola katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) ambao umeleta athari kwa wananchi na kusababisha mporomoko wa kiuchumi.

"Kama tunavyofahamu nchi ya Kongo ambayo ni jirani na Tanzania kuna mlipuko wa ugonjwa wa ebola, na sisi tunajipanga kuhakikisha tutapambana na magonjwa haya," alisema.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alisema kuwa Wizara yake imejipanga vizuri dhidi ya magonjwa ya mlipuko kwa wanyama na wamefanikiwa kudhibiti ugonjwa wa kimeta ambao una athari kwa mifugo, wanyamapori na binadamu.

Alifafanua kuwa kuna wataalamu wa kutosha wanaoshughulikia magonjwa haya yanapotokea chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu inayohusika na maafa na kueleza kuwa mifugo ya Tanzania ni salama kwani inapatiwa chanjo mara kwa mara.

Alisema mifugo mingi ya Tanzania inauzwa Kenya na kuwataka kuondoa hofu juu ya mifugo hiyo kwa kuwa kabla haijapelekwa huko kibiashara inafanyiwa ukaguzi na vipimo mbali mbali na wataalamu na ikibainika kuwa na ugonjwa haiwezi kusafirishwa kibiashara kwenda nchi nyingine.







Mafundi wakiendelea na ujenzi wa barabara za juu (Ubungo Interchange), katika eneo la Ubungo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Wakulima wanavyopata hasara kwa kukosa elimu

**Na Mary Mosha,** MOSHI

UKOSEFU wa elimu juu ya matumizi bora ya viuatilifu ni chanzo cha ukosefu wa mavuno yenye tija katika Mji mdogo wa Himo, Kata ya Makuyuni, wilayani Moshi.

Haya yameelezwa juzi kwenye mafunzo na Taasisi ya Udhibiti wa Viuatilifu na Utunzaji wa Mazingira (TPRI) juu ya matumizi bora ya viuatilifu.

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Udhibiti wa Viuatilifu na Utunzaji wa Mazingira, Mwema Felix, alisema wamebaini uwapo wa wakulima wengi kushindwa kutumia kanuni bora za viuatilifu kwenye mazao yao.

"Tumebaini ya kuwa wakulima wengi hawana elimu juu ya viuatilifu na njia bora za unyunyiziaji wa viuatilifu, hali inayosababisha kuchanganya viuatilifu baadhi vinapoteza nguvu yake kwenye mimea,"alisema.

Mkulima Johnson Mmanyi alisema kutokana na kutofahamu matumizi bora ya viuatilifu imewasababishia wakulima kupata hasara kwa kutumia viuatilifu vingi hivyo kupata mazao machache.

David Lyimo kwa upande wake alisema ili kuondokana na hasara zinazowakabili wakulima ni vyema serikali ichukue jukumu la kutoa elimu kwa wananchi mara kwa mara kwa kuwatumia wataalamu.

"Leo tumepewa elimu na kubaini jinsi ambavyo tunapata hasara kwa matumizi yasiyo sahihi ya viwatilifu, hivyo tunaiomba serikali kuangalia suala hili kwa makini ili kunusuru hali ya wakulima,"alisema Anna Kimaro. Alisema wakulima wengi wamekuwa wakikabiliwa na changamoto ya kuuziwa viuatilifu vilivyoharibika kutoka kwa baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu.

"Kutokana na kukosa fedha tasilimu za kununua viuatilifu tumekuwa tukikopeshwa na baadhi ya wafanyabiashara, ambapo wakati mwingine wamekuwa wakitupa zilizopitwa muda matumizi, tunaiomba serikali kuangalia uwezekano wa kutusaidia elimu pamoja na viuatilifu kwa bei nafuu vyenye uhakika,"alisema Anna.

Ofisa Kilimo Mji wa Himo, Magreth Elia, alisema uwepo wa gharama kubwa ya pembejeo za kilimo umechangia wakulima kutofuata kanuni bora za kilimo ili kupata mazao bora.

Alisema wakulima hao wanakabiliwa na ukosefu wa elimu juu ya matumizi sahihi ya viuatilifu, wataalamu wapo wachache na wanakabiliwa na uhaba wa vitendea kazi hali inayowafanya kushindwa kufika kwa wakulima ipasavyo.

# Rotary yajitosa kuondoa uhaba maji

**Na Mary Mosha,** MWANGA

TATIZO la uhaba wa maji lililokuwa linawakabili wananchi wa kata mbili za Mwanga na Lembeni katika Wilaya ya Mwanga linatafutiwa ufumbuzi baada klabu ya Rotary wilayani humo kuanza ujenzi wa kisima kikubwa cha maji chenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 500.

Maji yatakayopatikana katika kisima hicho yanatarajiwa kusambazwa kwenye taasisi za elimu, taasisi za dini na kwa wananchi ili kukabiliana na uhaba wa maji unayozikabili wilaya hizo.

Baadhi ya wananchi waliozungumza na Nipashe walieleza kuwa wanalazimika kutembea umbali mrefu kutafuta maji kwa kutumia punda maeneo ya Kisangara jambo ambalo linawalazimu wengi wao kutumia maji yasiyo safi na salama.

"Inatulazimika kutembea umbali mrefu kutafuta maji safi na salama, hali ambayo inasababisha muda mwingi kupotea njiani huku shughuli za uzalishaji zikisimama," alisema Aisha Mzava.

Edrisha Mchome alisema wanalazimika kununua maji ndoo moja yenye ujazo lita 20 kwa Sh. 500 na kwamba wengi wao wanashindwa kumudu gharama hizo kutokana na hali ya uchumi ilivyo.

Alisema wengi wa wananchi hutegemea maji ya kuvuna ya mvua, ambayo yamekuwa hayatoshelezi kutokana na uhaba wa mvua maeneo ya tambarare.

Kwa upande wake, Rais wa Rotary klabu wilayani humo, Donasian Senzige alikiri kuwapo kwa changamoto kubwa ya tatizo la maji katika kata hizo, ambalo limedumu kwa muda mrefu.

Alisema kukamika kwa ujenzi huo kutaondoa adha hiyo ya kutembea umbali mrefu kutafuta huduma ya maji na kujikita katika uzalishaji na kukuza uchumi wa nchi. Mhandisi wa maji Wilaya ya Mwanga,

Stephano Kariwa, alisema serikali inatambua tatizo la maji linalowakabili wananchi wa wilaya hiyo, ambapo kwa sasa wameanza mradi mkubwa wa maji kutoka nyumba ya Mungu, Mwanga, Same na Korogwe unaotarajiwa kukamilika mwaka 2020.

# Wenye ulemavu waomba ruzuku vifaa vyao

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WALEMAVU mkoani Kilimanjaro, wameomba serikali ianzishwe taasisi itakayoshughulikia upatikanaji wa vifaa vya kujimudu, pia itoe ruzuku kwa vifaa hivyo pamoja na viungo bandia.

Akizungumza jana na wanahabari ofisini kwake, Mweka hazina wa Shirikisho la vyama vya watu wenye ulemavu Tanzania Mkoa wa Kilimanjaro, Pudensiana Kisoka, alisema serikali inapaswa kuangalia upya suala la walemavu.

Alisema watu wenye ulemavu nchini wanakumbana na gharama kubwa za matibabu, viungo bandia na vifaa saidizi ambapo wengi hushindwa kumudu ingawa kuna waraka wa serikali kuhusu huduma za matibabu bure kwa watu wenye ulemavu ambao kiuhalisia hautekelezwi.

"Tunaomba uandaliwe utaratibu ambao utatoa unafuu wa matibabu kwa watu wenye ulemavu, serikali kutoa ruzuku kwa viungo bandia kwa watu wenye ulemavu ili waweze kumudu gharama hizo na kwamba bado sera ya huduma kwa watu wenye ulemavu haijatafsiriwa katika nyaraka za huduma za wizara mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji,"alisema

Kisoka alisema pia mitaala wa elimu haijajumuisha vyema mahitaji ya watu wenye ulemavu, hali hiyo inafanya ushirikishwaji kuwa mgumu huku sera ya watu wenye ulemavu na sheria zao hazijulikani kwa wengi, ikiwamo vyombo vya dola jamii inayowazunguka.

"Uandaliwe utaratibu wa kuwaelimisha watu wenye ulemavu juu ya haki zao na uwepo mfumo wa kuwafikishia nyaraka kama sera na sheria ya watu wenye ulemavu ,"alisema.

Kisoka alisema baadhi ya jamii za watu wenye ulemavu bado hazitambuliki vyema hivyo hazina mfumo wao rasmi wa elimu kwa wenye ulemavu zaidi ya aina moja, aliomba mahitaji muhimu ya watu hao ikiwamo elimu ya utengamao yazingatiwe wakati wa kutayarisha mitaala ya elimu

Mwakilishi kutoka ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Uforo Mariki, alisema serikali inaendelea kufanyia uchambuzi na utatuzi wa masuala yanayowakabili watu wenye uleamvu, ikiwa ni pamoja na kuwa na mwakilishi bungeni ambaye atakuwa anaongealea maswala hayo. "Changamoto zote tumezipokea na zitawashilishwa katika ngazi zote za mkoa hadi taifa kwa kufanyiwa kazi na kuitaka jamii kuthamini watu wenye ulemavu na kuwatoa katika sensa ili kupata takwimu sahihi zitakazotumika katika mipango ya kimaendeleo,"alisema.

ama
ALHAMISI JUNI 13, 2019
AFYA NA MAZINGIRA



**Mazoezi yanayobadili misuli, maumbile yanapoteza uzazi**

Ukurasa 17



BWANA CHANJO MANYARA...

Sura kamili namna anavyomnasua mtoto kutoka janga la maisha yake

Ukurasa 18



Ukurasa 14

## Mkurugenzi Ewura: Mamlaka za maji zinajitanua kwa shida



# Mganga Mkuu Morogoro asimulia wanavyojihami 'hodi' ya dengue

Ukurasa 16



Kinywaji cha Wine. **PICHA: MTANDAO.**

## Wajua unywaji 'wine' una miaka 2000?

**Na Helen Briggs**

HISTORIA inaonyesha kuwa huenda kinywaji aina ya 'wine' kinachopendelewa sana nchini Ufaransa na katika sehemu nyingi duniani, kilikuwapo zaidi ya karne tisa zilizopita.

Hiyo ni kwa mujibu wa vinasaba na historia ya mimea hiyo, huku ikionyesha Wataliano nao wameangukia matumizi hayo, wastani wa miaka 2000 sasa

Wanasayansi wanasema walitengeneza 'wine' mbalimbali kufanikisha matumizi yao, kwani mahitaji mbalimbali yanayotumika kutengenza kinywaji hicho sasa, mimea yake iko tangu zama hizo zilizopita.

Kinachofanyika hivi sasa ni kwamba watafiti wanafanya kazi ya kuoanisha vinasaba kutoka aina 28 za mbegu kutoka zama za chuma katika maeneo ya kihistoria na makumbusho ya Italia na Ufaransa.

Mtaalamu kutoka Chuo Kikuu cha York, Dk. Nathan Wales, anasema wakiwa katikati ya Ufaransa, walipata mbegu zinazooana na vilivyokuwapo zama hizo.

"Ni aina ya mimea ambayo inazalishwa leo nchini Ufaransa, inawiana na kilichokuwapo miaka 900 iliyopita," anasema

Huo ni utafiti uliozama mbali zaidi, kukagua aina ya kinywaji katika Italia ambacho watafiti nacho walikifanyia kazi.

Ni kazi iliyofanywa na timu ya watafiti kutoka nchi za Uingereza, Denmark, Ufaransa, Hispania na Ujerumani walioingia kazini kuusaka ukweli huo wa kihistoria.

MAZINGIRA

# Mkurugenzi Ewura: Mamlaka za maji zinajitanua kwa shida

- Maji yanazidi kupotea njiani
- Nguvu bado zimejikita mijini
- Waziri awadokeza pa kuinukia



Moja ya miradi ya maji iliyozinduliwa katika zama za serikali ya awamu ya nne, katika kijiji cha Ilula, wilayani Kilolo.

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

HUDUMA za majisafi na majitaka mijini na vijiji zimekuwa duni kutokana mengi, ikiwamo uwezo mdogo wa kifedha katika uendelezaji wa sekta hiyo.

Hata inaporejewa historia ya miaka nenda rudi hasa kabla ya mwaka 2000, hali kwa ujumla nchini ilikuwa mbaya maradufu, hasa katika baadhi ya maeneo ya vijijini.

Tatizo hilo limekuwa kubwa kulingana na mahitaji makubwa ya maji kwa maisha ya kila siku ya binadamu. Hatimaye, kupitia mipango ya maendeleo kitaifa, serikali iliamua kulivalia njuga kuhakikisha huduma inaboreshwa kwa haraka.

> **"Hilo linaeleza kwamba kuna uimarikaji uwiano wa wafanyakazi na idadi ya wateja na ufungaji wa mita za maji kwa wateja.**

Katika mipango hiyo, iliongeza bajeti katika maendeleo ya sekta ya maji na kuanzishwa na kuimarishwa kwa mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira.

**Ripoti Ewura**

Moja ya matokeo ya mikakati hiyo, ndiyo ikaanzishwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (Ewura). Lengo ni kuhakikisha huduma husika zinatolewa kwa ubora na viwango vya juu.

Hivi karibuni, Ewura ilizindua ripoti za utendaji za Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira nchini katika mwaka wa fedha 2017/18, inayoonyesha tathmini ya utendaji wa mamlaka hizo.

Kaimu Mkurugenzi wa Ewura, Nzinyagwa Mchany anasema ripoti ya mamlaka zinazohudumia miji ya makao makuu ya wilaya na miji midogo, imetoa uchambuzi wa utendaji wa mamlaka za maji na usafi wa mazingira 82; kwa maana ya mamlaka 68 za miji mikuu ya wilaya na nne za miji midogo.

Pia, anasema mamlaka 15 hazikufanyiwa tathmini kwa kushindwa kuwasilisha taarifa za utendaji na mamlaka 13 kati ya hizo zilikuwa hazijaanza kutoa huduma ya maji, kwa sababu ya kukosa menejimenti na bodi za wakurugenzi.

**Mikoa & Miradi**

Anasema, tathmini ya utendaji wa mamlaka zinazohudumia miji mikuu ya mikoa na miradi ya kitaifa, inaonyesha utendaji wa mamlaka hizo umeimarika, kama vile kuongezeka kiwango cha maji yaliyozalishwa na ubora wake, wanaopata maji, wateja wa maji na mtandao wa majitaka.

Mchany anataja maboresho mengine ni wastani wa muda wa upatikanaji maji kwa siku, kuimarika uwiano wa wafanyakazi na idadi ya wateja.

Nyingine kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo wa Ewura, ni kuongezeka makusanyo na ufanisi katika ukusanyaji maduhuli na idadi ya mamlaka za maji za mikoa zinazofanya vizuri kwa mujibu wa vigezo vilivyowekwa na Ewura.

Kiongozi huyo anasifu utendaji wa mamlaka zinazohudumia makao makuu ya miji, wilaya na miji midogo kwamba kumeimarika katika nyanja tofauti.

Anataja maboresho hayo ni kuongezeka muda wa upatikanaji maji, kupungua kiasi cha maji kinachopotea, kuongezeka makusanyo na kiwango cha ufanisi cha ukusanyaji maduhuli ya maji.

Hilo linaeleza kwamba kuna uimarikaji uwiano wa wafanyakazi na idadi ya wateja na ufungaji wa mita za maji kwa wateja.

Wigo changamoto

Mchany anasema, ni mafanikio yanayokabiliwa na changamoto zinazohitaji ufumbuzi kwa kushindwa kukidhi mahitaji stahiki.

Anarejea mwaka wa fedha 2017/18, kiasi cha maji kilichozalishwa na mamlaka za maji na usafi wa mazingira katika makao makuu ya mikoa ni mita za ujazo 307, mil-

**Inaendelea Uk. 15**



Bomba l

MAZINGIRA

# Mkurugenzi Ewura: Mamlaka za maji zinajitanua kwa shida



Ndivyo ilivyokuwa shida ya maji wilayani Kisarawe. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Inatoka Uk. 14**

ioni ikilinganisha na mita za ujazo 276 milioni kwa mwaka wa fedha 2016/17.

"Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 11.2. Hata hivyo, kiwango hicho cha maji kilichozalishwa ni asilimia 67.9 ya mahitaji ya maji ambayo ni mita za ujazo 452 milioni kwa mwaka wa fedha 2017/18.

"Wastani wa upatikanaji huduma ya maji ni saa 18 kwa siku, wakati kiwango kinachotakiwa cha upatikanaji wa huduma ya maji ni saa 24 kwa siku," anasema.

Katika miradi ya kitaifa, anasema kiasi cha maji yaliyozalishwa ni mita za ujazo 23.7 milioni mwaka wa fedha 2017/18, ikilinganishwa na mita za ujazo 24.5 milioni kwa mwaka wa fedha 2016/17.

Mchany anasema maji yalizalishwa kupitia miradi ya kitaifa na yamepungua kwa asilimia tatu, hoja ni kwamba inatokana na kupungua uzalishaji maji katika miradi minne kitaifa: Maswa, Makonde, Mugango - Kiabakari na Manawasa.

Ufafanuzi wake ni kwamba, kinachohudumiwa sasa ni asilimia 51.2 tu ya mahitaji halisi, huku miradi ya kitaifa katika mwaka wa fedha 2017/18, ilihudumia wastani wa saa 14 kwa siku.

Anasema, katika mwaka wa fedha 2017/18, mamlaka za majisafi na mazingira za makao makuu ya mikoa, zilihudumia ongezeko la asilimia 9.2, dhidi ya mwaka wa fedha uliotangulia.

Kati ya wateja waliofungiwa dira za maji, ni asilimia 97 waliopatikana kulipia katika mwaka wa fedha 2017/18, kama ilivyokuwa mwaka uliotangulia

Mkurugenzi huyo anasema, ufungaji dira za maji za wateja umeongezeka kutoka asilimia 79 kwa mwaka wa fedha 2016/17 hadi kufikia asilimia 82 kwa mwaka wa fedha 2017/18.

**Kulivyo mijini**

Mchany anabainisha, mamlaka za miji mikuu ya mikoa ziliongeza mapato kwa asilimia 24.7 katika mwaka wa fedha 2017/18, kulinganisha mwaka uliotangulia.

Vivyo hivyo, katika miradi ya kitaifa ukusanyaji wa mapato uliongezeka kutoka Sh. 13.43 bilioni katika mwaka wa fedha 2016/17 hadi kufikia Sh. bilioni 17.46 katika mwaka wa fedha 2017/18 sawa na ongezeko la asilimia 30.

Anaeleza, kupitia mamlaka za maji miji na mikoa, kiwango cha ufanisi wa kukusanya mapato kimeongezeka kutoka asilimia 91.2 kwa mwaka wa fedha 2016/17 hadi asilimia 93.6 mwaka 2017/18.

Katika mamlaka za maji za miradi ya kitaifa, anasema ukusanyaji mapato umeongezeka kutoka asilimia 75.6 kwa mwaka wa fedha 2016/17 hadi asilimia 102.5 kwa mwaka wa fedha 2017/18, kuligana na malengo yaliyowekwa.

Lingine analolieleza ni kwamba, katika mwaka wa fedha 2017/18, maji yaliyozalishwa ni mita za ujazo 33.7 milioni, ikilinganishwa na mita za ujazo 33.8 milioni kwa mwaka wa fedha 2016/17.

"Hii ni sawa na kupungua kwa asilimia 0.3. Kupungua maji yanayozalishwa kunatokana na kutojumuishwa kwa Mamlaka za Vwawa na Mlowo (Mbozi, Mkoa wa Songwe ) kwa mwaka wa 2017/18," anasema Mchany

Anafafanua sababu ni mamlaka hizo za maji kuunganishwa na kuunda Mamlaka ya Maji Vwawa- Mlowo, zinazotoa maji katika makao makuu ya mkoa mpya, Songwe.

Anasema mamlaka za Maji Vwawa na Mlowo zilichangia asilimia 2.4 ya maji yaliyozalishwa na mamlaka za maji za wilaya na miji midogo mwaka wa fedha 2016/17.

Pia, wastani wa upatikanaji maji umeongezeka kutoka saa 9.1 kwa siku kwa mwaka wa fedha wa 2016/17 hadi kufikia wastani wa saa 11.4 kwa siku kwa mwaka wa fedha wa 2017/18.

Hata hivyo, bosi huyo wa Ewura, anakitaja kiwango hicho ni kigodo, ikilinganishwa na kinachotakiwa kuhudumia maji kwa saa 24.

Sura nyingine ya maendeleo ni kwamba, wateja waliofungiwa mita za maji walifikia asilimia 79 kwa mwaka 2017/18, ikilinganishwa na asilimia 72 mwaka wa fedha 2016/17, hali inayotoa picha haja ya kuwapo jitihada za huduma hiyo kuwafikia wateja wote.

Sura ya maendeleo katika makusanyo ni kwamba, kiasi cha maduhuli yatokanayo na huduma za majisafi yaliongezeka kutoka Sh. bilioni 11.89 kwa mwaka wa fedha 2016/17 hadi Sh. bilioni 13.20 kwa mwaka wa fedha 2017/18.

**Upotevu wa maji**

Anasema bado kuna kiwango kikubwa cha upotevu wa maji, kwenye mamlaka nyingi za miji mikuu ya mikoa. Tathmini inaonyesha, upotevu umeongezeka kutoka asilimia 38.4 kwa mwaka wa fedha 2016/17 hadi kufikia asilimia 40.5, mwaka 2017/18.

> **Mkurugenzi huyo anasema, ufungaji dira za maji za wateja umeongezeka kutoka asilimia 79 kwa mwaka wa fedha 2016/17 hadi kufikia asilimia 82 kwa mwaka wa fedha 2017/18.**

Kimyume chake, Mchany anasema katika mamlaka za maji za miradi ya kitaifa katika kipindi hicho, kiwango cha upotevu wa maji kimepungua kutoka asilimia 33.1 hadi kufikia aslimia 26.8.

Hadi sasa inaelezwa mtandao wa usambazaji majisafi unakidhi asilimia 74 kwenye miji ya makao makuu ya mikoa na asilimia 55 kwa miradi ya kitaifa,

Tafsiri kutokana na ripoti ya takwimu hizo ni kwamba, sehemu kubwa za maeneo yanayopaswa kuwa na huduma ta maji safi, hayafikiwi.

Waziri wa Maji

Waziri wa Maji Profesa Makame Mbarawa, maelekezo yake kwa Ewura, ni kwamba kusimamia mamlaka za maji zidhibiti upotevu huo wa maji, unaopanda katika maeneo husika .

Profesa Mbarawa, anaagiza Ewura kuzilea na kusimamia mamlaka hizo kuzalisha maji na kuhakikisha yanawafikia wananchi.

"Pia fanyeni semina na kutoa elimu kwa wakurugenzi na wenyeviti wa mamlaka za maji namna ya uendeshaji wake, ili kujua namna ya kupunguza gharama za uendeshaji zikiwamo za matumizi makubwa kununua dawa ya kutibu maji na za umeme," anasema.

Anahimiza kuwa, pamoja na kuzalisha na kusambaza maji, mamlaka inatakiwa kubaini gharama za maji inayozalisha hasa vijijini ni kubwa kuliko mijini, hivyo mamlaka hizo zinapaswa kuweka viwango sawa vya kudhibiti ubora, kuwa na takwimu sahihi za huduma za maji kila wakati.



a maji katika moja ya miradi mikubwa nchini.

AFYA

# Mganga Mkuu Morogoro asimulia wanavyojihami 'hodi' ya dengue

## ▪ Ofisa Afya atumia fimbo ya bajeti ▪ Matabibu katika njia kuu utaalamu



Mganga Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Dk. Frank Jacob, akizungumza na Mtafiti Dk. Angelo Nyamtema. Wanaofuatia ni Dk. Abdallah Abdallah (anayetabasamu), bingwa wa magonjwa ya kinamama na uzazi, Dk Hassan Njete na wa mwisho, Dk. Sister Nathalia Makunja, bingwa wa magonjwa ya kinamama na uzazi, kutoka Hospitali ya Mtakatifu Fransisko, Ifakara. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Na Christina Haule, Morogoro**

"...Kufukia madimbwi ya maji, kufyeka nyasi au vichaka, kumwaga maji yaliyomo kwenye makopo na vifuu, kuvaa nguo ndefu, kufunika mashimo ya maji taka kwa mifuniko imara, kutumia vyandarua wakati wa kulala na kuweka nyavu madirishani na milangoni...

"...Mafuta ya nazi na papai na vidonge, vilivyoanza kutangazwa vinatumika kuzuia mbu wa dengue asiweze kumuuma mtu na kumuambukiza jambo ambalo, halina ukweli kamili...

"...Sekta ya afya imetoa maelekezo ya tahadhari kwa halmashauri zote tisa hadi kufikia ngazi ya vituo vya kutoa huduma kwamba zitoe tiba pindi mgonjwa atakapojitokeza mahali alipo..."

Katika jiji la Dar es Salaam na maeneo mengi ya nchini, mada na hofu kuhusu ugonjwa unaosambazwa na mbu jike aina ya Aedes, uitwao dengue uko kila mahali. Kwa ujumla hali si nzuri,

Hivi sasa, Mamlaka ya Chakula, Dawa na Vipodozi Tanzania (TFDA) ina ushauri kwamba kuna dawa muhimu mbadala wa kujikinga, mafuta mengine yasiyothibishwa yanayoweza kuleta madhara katika ngozi zinazopatikana katika maduka ya dawa muhimu

> **"...Sekta ya afya imetoa maelekezo ya tahadhari kwa halmashauri zote tisa hadi kufikia ngazi ya vituo vya kutoa huduma kwamba zitoe tiba pindi mgonjwa atakapojitokeza mahali alipo..."**

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Dk. Jackob Frank, ameiambia Nipashe ofisini kwake, kuwa zipo aina nyingi za dawa za kujikinga na mbu waenezao magonjwa yatokanayo na mbu, ikiwamo malaria zilizothibitishwa na TFDA.

Anataja aina ya dawa mafuta ya nazi na papai na vidonge, vilivyoanza kutangazwa vinatumika kuzuia mbu wa dengue asiweze kumuuma mtu na kumuambukiza jambo ambalo, halina ukweli kamili.

Anasema, ni vyema jamii ikazingatia ushauri wa kitaalamu unaotolewa na wataalamu wa Afya badala ya kutumia nyinginezo zisizithibitishwa.

Tiba yake ikoje? Dk. Frank anasema, kimsingi hakuna matibabu maalum ya ugonjwa huo, bali inategemea dalili anazokuwa nazo mgonjwa kutokana na ugonjwa wenyewe kuwa na dalili zinazoshabiliana na malaria.

Huku akitaja njia mojawapo ni kumpatia mgonjwa dripu ya maji pale anapogundulika kuwa na upungufu, Dk, Frank anaainisha dalili kuwa ni: Homa kali; maumivu ya kichwa, misuli na viungo; kichechefu; kuvimba tezi.

Pia, anasema kuna wakati mgonjwa anatokwa damu katika sehemu zenye uwazi mwilini kama masikioni na sehemu za haja kubwa na ndogo.

**Chanzo & tahadhari**

Dk. Frank anasema chanzo cha dengue ni virusi wanaoenezwa na mbu aina ya Aedes wenye rangi nyeusi na mabaka meupe, ambao huonekana zaidi asubuhi na jioni.





Picha ya hospitali ambayo ni moja ya msaada kwa vita ya Dengue, Morogoro.

Daktari huyo anafafanua kuwa, mbu huyo anaambukiza baada ya kutoka kumuuma mgonjwa na kisha akamuuma mtu mwingine. Hivyo, daktari huyo anaitaka jamii kuzingatia maelekezo ya wataalamu wa afya kuhusu namna ya kujikinga na maambukizi.

Moja ya njia anazozitaja ni kufukia madimbwi ya maji, kufyeka nyasi au vichaka, kumwaga maji yaliyomo kwenye makopo na vifuu, kuvaa nguo ndefu, kufunika mashimo ya maji taka kwa mifuniko imara,kutumia vyandarua wakati wa kulala na kuweka nyavu madirishani na milangoni.

Dk. Frank anasema taarifa za Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ya Aprili 2 mwaka huu, inaonyesha kati ya watu 470 walipima ugonjwa nchini, 307 walithibitika kuugua.

**Hofu Moro**

Anaainisha orodha hiyo kwamba wagonjwa 252 ni kutoka jijini Dar es salaam na wengine 55 ni kutoka jijini Tanga, huku Dk. Frank akitia shaka ya kuingia mkoani kwake.

Anasema vigezo vya tahadhari hiyo, ni ukaribu wa Morogoro na Dar es Salaam, usafiri rahisi na mwingiliano kubwa wa kibiashara na kijamii, baina ya mikoa hiyo jirani.

Dk. Frank anasema, sekta ya afya mkoani kwake imetoa maelekezo ya tahadhari kwa halmashauri zote tisa hadi kufikia ngazi ya vituo vya kutoa huduma kwamba zitoe tiba pindi mgonjwa atakapojitokeza mahali alipo.

"Hakuna sababu ya 'kumrifaa' (kuhamishia hospitali kubwa) akitokea mgonjwa wa dengue, bali wataalamu wa afya watumie utaalamu waliopewa kuwahudumia wagonjwa pale wanapotokea" anasema Dk. Frank.

Pia, anawaelekeza watalaamu wa afya wa wilaya zote mkoani Morogoro waendelee kuhamasisha jamiii kujikinga dhidi ya maambukizi ya ugonjwa huo.

Kuhusu umwagaji dawa katika madimbwi, Dk. Frank ana ufafanuzi kwamba halmashauri zote kupitia agizo la serikali ina utaratibu wake wa kumwaga dawa katika madimbwi ya wazi ya maji.

Anasema ni kutokana na agizo la Rais Dk. John Magufuli, kwamba kila halmashauri itenge fedha za kununua dawa hizo katika kiwanda cha dawa za kuua wadudu kilichopo Kibaha mkoani Pwani kuzimwaga katika makazi ya wananchi.

Mganga huyo, anasema umefika wakati muafaka kwa halmashauri za mkoa wa Morogoro kutenga fedha kununua dawa hizo, ili kujikinga na dengue kwa kuua mazalia yake unaweza kutokomezwa.



Mganga Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Dk. Frank Jacob (aliyesimama), akizungumza jambo na wenzake.

**Ofisa Afya**

Kaimu Ofisa Afya wa Manispaa ya Morogoro, Prisca Gallet, anasema Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, imetenga sh. milioni 11.5 katika bajeti ya fedha ya mwaka uliopo wa fedha kwa ajili ya kununua dawa za kuua mazalia ya mbu katika Manispaa ya Morogoro.

> **"Hakuna sababu ya 'kumrifaa' (kuhamishia hospitali kubwa) akitokea mgonjwa wa dengue, bali wataalamu wa afya watumie utaalamu waliopewa kuwahudumia wagonjwa pale wanapotokea" anasema Dk. Frank.**

Anasema, katika bajeti iliyopita, halmashauri ilitenga sh. milioni l 6.5 na kufanikiwa kununua dawa zinazomwagwa katika maeneo yenye madimbwi na mashimo yenye maji yaliyotuama, kuzuia mazalia ya mbu, kujiepusha na malaria na dengue.

Hivyo Gallet aliihasa jamii kuwa mstari wa mbele katika kusafisha mazingira huku wakihakikisha wanatumia dawa za mbu za kufukiza na kupuliza kwenye majumba yao ili kuzuia mbu wa aina zote.

"Mtu akilala mchana, anatakiwa atumie chandarua ili asiweze kung'atwa na mbu, avae nguo ndefu na kupaka mafuta ya ku-

INAENDELEA UK.20

# Mazoezi yanayobadili misuli, maumbile yanapoteza uzazi

WANASAYANSI wamegundua kuwa baadhi ya wanaume hupunguza uwezo wao wa kupata watoto kutokana na jitihada zao za kutengeneza miili ya kuvutia.

Mazoezi ya kutunisha misuli au kutumia dawa za kuzuia kupata vipara vinatajwa ni sumu inayoharibu mfumo wa uzazi kwa wanadamu.

Wataalamu wanasema kwamba, mwanaume anayetumia dawa au anayefanya mazoezi ya kutunisha misuli, anaweza kuwa anapata maumivu ya kichwa wakati wa tendo la ndoa na mbegu zake kushindwa kuwa na uwezo wa kuzalisha.

"Nimegundua kuwa baadhi ya wanaume ambao wanakuja kwa ajili ya vipimo miili yao huwa ni mikubwa," anasema Dk. James Mossman, kutoka chuo cha Brown kilichopo Marekani.

Daktari huyo anafafanua: "Wanaume wanajaribu kutaka kuwa na mwonekano mkubwa, huku wanajisababishia madhara ya afya ya uzazi"

"Licha ya kuwa wanajitengeneza wenyewe maumbile yasiyokuwa na uhalisia, lakini wanashindwa kuelewa kuwa wanajiondolea uwezo wao kuwa na mbegu za kuzalisha."

Miongoni mwa madhara yanayowapata, ni homoni zao kushindwa kufanya tendo la kujamiiana kiufasaha, kutokana na mazoea yao ya kutengeneza mwonekano wa miili yao kuwa chanzo kikuu.

Profesa Allan Pacey, kutoka chuo cha Sheffield anaongeza:"Inashangaza kuona wanaume wanaenda kwenye mazoezi ili kuwa na muonekano mzuri. Mara nyingi, lengo ni kuwavutia wanawake na bila kuelewa kuwa wanapunguza uwezo wao wa kuzaa."

Hata hivyo, watafiti wanasema kwamba dhana inayofanana na hiyo ya wanaume kutumia dawa ili kutengeneza maumbile yao, ina madhara yanayofanana.



Aina ya maumbile, ambayo kuna wakati inaleta tabu kiafya. **PICHA: MTANDAO.**

Mtaalamu huyo anasema, dawa zinazotengeneza maumbile yao na kuzuia nywele zote, husababisha madhara katika mfumo wa uzazi.

"Ninaweza kusema kuwa kuna wanaume wengi zaidi ya unavyofikiria ambao wanaweza kupata maradha, inaweza kuwa asilimia 90 hivi. Mazoezi hayo yanaweza kuongeza tatizo linalofanana kuendelea."

Dk. Mossman anasema, ni dawa hizo zinazoweza kumfanya mtu kuwa na mwonekano mzuri wa kuvutia, lakini ikakusababishia madhara katika uzazi.

Anaweka mtazamo wake kwamba, kuna baadhi ya wanaohisi kwamba wanawavutia jinsia nyingine huku wanauwa uwezo wao wa kuzalisha. Ujumbe mkubwa wa hapo ni idadi ya vijana wadogo kuwa wahanga wa kuzalisha bado changamoto.BBC

AFYA

BWANA CHANJO MANYARA...

# Sura kamili namna anavy mtoto kutoka janga la ma

Na Jaliwason Jasson, Babati

- Simulizi 'ugonjwa baada ya ugonjwa'
- Aweka sawa ilikojikita vita ya polio
- Wanaokimbia kliniki wafunguka yao



Kinamama wakiwa na watoto wao katika Hospitali ya Mrara, Manyara, wakisubiri kuchanjwa. **PICHA ZOTE: JALIWASON JASSON**

INAKUBALIKA wazazi wengi nchini wanawapeleka watoto wao kupata chanjo. Kampeni na mwamko wake umepiga hatua sasa, kwani si dhana ngeni na katika huduma kuanzia zahanati na vituo vya afya 'si bidhaa adimu.'

Vivyo hivyo, kinachofanyika hapo ni mwendelezo wa utekelezaji wa yaliyoaza muda mrefu na sasa ni sehemu ya Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) nchini, yenye kipindi cha muongo mmoja sasa.

Lakini, bado inaelezwa kwamba kuna wachache katika vikundi vya kijamii, ambao bado wanasuasua kutohudhuria huduma hizo za chanjo, kwa baadhi ya sababu kama vile kuhofu 'kuwagombeza.'

Kuna wazazi wanaowapeleka watoto hospitali kupata chanjo, lakini hawazimalizii chanjo hizo.

Ushauri uliopo ni kwamba, wazazi wanapaswa kuzingatia mahudhurio ya mtoto kadri wanavyopata ushauri unaoelekezwa na wataalam wa afya, vijana wasipate madhara.

**WAZAZI WAONGEA**

Wazazi wengi waliozungumza na Nipashe kuhusu chanjo, wanakiri kuwa ni kinga ya magonjwa kwa mtoto, ila wengine wanashindwa kuzimaliza kwa kuogopa wanachodai 'ukorofi' na 'kauli mbaya' kutoka kwa wauguzi.

Mkazi wa eneo la Nakwa, Fatma Juma, anasema kinachowafanya wazazi washindwe kumaliza chanjo na hatimaye kuwasababishia maradhi watoto, ni kukosekana elimu kuhusiana na dhana ya chanjo.

Anasema, elimu ikitolewa na wauguzi huwa haiwaingii vizuri, maana wauguzi wengi wanatumia anachokitaja 'lugha chafu' Fatma anaongeza:

"Mfano siku ya chanjo idadi ya watoto ikiwa kubwa wapo manesi wanaotukana baada ya kuwa wamechoka hivyo kina mama ambao wanapeleka watoto kliniki huchukia na kuacha kuhudhuria siku za chanjo,"

Mkazi mwingine wa kitongoji cha Dareda, Rozalia Joseph, anaungana na wataalamu kuwapatia chanjo watoto, kunawasaidia kuwakinga na magonjwa ya polio na pepopunda.

Anasema wanawake wengi wanashindwa kumaliza chanjo, kwa sababu ya umbali wa zahanati na vituo vya afya vilipo, hivyo wengine hutokomea baada ya kujifungua.

> **"Mfano siku ya chanjo idadi ya watoto ikiwa kubwa wapo manesi wanaotukana baada ya kuwa wamechoka hivyo...**

Halima Ramadhan, mkazi wa Maisaka, anasema yeye amewapeleka watoto wake kliniki na wamepata chanjo zote, akiwa mhudhuriaji mzuri wa kliniki kwa miaka mitano sasa.

Ameiambia Nipashe akirejea uzoefu wake, kwamba watoto wake wamepata chanjo zote za afya na kwamba amefaidika na afya zao ni nzuri sasa, kutokana na watoto kupata chanjo zinazowakinga na magonjwa kama polio, pepopunda na magonjwa mengine nyemelezi.

Bahati Cosmas, anakiri umuhimu wa chanjo kwa watoto, maana inachagia kuwakinga na maradhi kama surua na anawashauri wanaume kutenga muda wa kuwasindikiza wake zao, kuwawezesha kuhudhuria chanjo zote kwa watoto.

**MRATIBU CHANJO**

Mratibu wa Chanjo na Ofisa Afya wa Halmashauri ya Mji wa Babati mkoani Manyara, Grace Ngoo, anasema chanjo anayoiita kitaalamu ya BCG, ndiyo mtoto anapatiwa mara tu baada ya kuzaliwa. Kimsingi huwa anapatiwa muda ndani ya siku 14.

"Mtoto akizaliwa akaikosa chanjo ya BCG, madhara yake anakuwa katika 'risk' (hatari) ya kupata kifua kikuu. Kuchanjwa anatakiwa apate kovu ndani ya miezi mitatu na kama hajapata kovu, tunakuwa na shaka mpaka arudiwe," anaeleza Ngoo

Mtaalamu huyo wa chanjo anazitaja faida za chanjo kuwa inamuepusha mtoto na hatari zinazomnyemelea mkosa chanjo. Hivyo, aliyechanjwa anakuwa mbali na hatari ya kuathirika, hata kukiepuka kifo.

Ngoo anaeleza katika hilo, kuwa lengo kitaifa hivi sasa kwa chanjo liko juu, kwa wastani kati ya asilimia 90 na asilimia 95, ingawaje kuna wilaya ziko katika mafanikio ya kuvuka kiwango hicho.

**HATARI YA KUKOSA**

Mtoto anayeikosa chanjo ya BCG madhara yake ni yapi? Ngoo anasema huwa hujitokeza mara moja kulingana na mazingira halisi.

Anafafanua kwamba, chanjo nyingine muhimu ni ya tiba ya maradhi 'Polio 0' ambayo mtoto hawezi kuipata muda mwingine wowote isipokuwa ni mara tu baada ya kuzaliwa. Ni mahsusi, kwa ajili ya kumuweka salama zaidi, dhidi ya ugonjwa polio.

Anafafanua kuwapo aina tatu zinazofahamika akizitaja "By Polio1;

AFYA

# yomnasua
# aisha yake



By Polio 2; By Polio3" anazodai mtoto anapata dozi nne kwa wakati mmoja.

"Polio zingine anapata mtoto anapotimiza wiki sita, yaani mwezi mmoja na nusu na 'By Polio 2' anaipata anapotimiza wiki 10 na 'By Polio3' anaipata akiwa na wiki 14," anafafanua

Kwa mujibu wa mratibu huyo wa chanjo, faida za chanjo hiyo ni kumkinga mtoto dhidi ya ugonjwa wa kupooza, anajihakikishia kinga ya mwili na mbali na hatari zinginezo.

Mratibu huyo wa chanjo, anasema faida nyingine ya chanjo ni mtoto kuwa na afya bora, mzazi anapunguziwa muda wa kwenda kumuuguza mtoto hospitali, dhidi ya magonjwa hatari ambayo yana sura ya nyemelezi na chanzo ni upungufu ya kinga mwilini.

Ngoo anashauri watoto wawahishwe kwenye chanjo, hata inapotokea mzazi amejifungulia nyumbani, bado wana jukumu la kuwapeleka watoto kwenye chanjo, kumuweka salama kiafya.

VITA POLIO

Mratibu huyo anaitaja chanjo nyingine anayoiita 'IPV' anayoieleza ni mpya, kwamba ilianza Aprili mwaka jana, ikiwa mahsusi kukomesha ugonjwa wa polio nchini, ambao uko katika hatua ya kuthibitishwa kutoweka.

Anasema, lengo la serikali hivi sasa ni kukomesha ugonjwa huo kutoweka kabisa nchini ifikapo mwaka 2020 na wataalamu wako katika ufuatiliaji wa karibu dhidi ya ungojwa huo.

Mtaalamu huyo anasema, polio inafanyiwa ufuatiliaji wa karibu, huku akizitaja dalili zake za ghafla ni kwamba, mtoto anashindwa kushika kitu, anashindwa kutembea au kushika jambo na wengine wanatikisika vichwa.

Rai yake kwa umma, ni kwamba wazazi kuwa makini wakati wa kuwatawaza watoto, ili wasipate virusi vinavyosabisha na ugonjwa huo, maana virusi mara nyingi vinapatikana kwenye kinyesi na kunapokuwapo dalili wanazotilia shaka wawapeleke hospitali na si vinginevyo.

Ngoo anapinga vikali watoto kupelekwa kwa waganga wa kienyeji, kwamba hakuna tiba sahihi itakayopatikana huko, kutokana na njia potofu, pia uelewa duni wa uhalisia wa maradhi.

"Huwa tunachukua sampuli za kinyesi na kuzituma Muhimbili (hospitali), wanapima na zinawahi kurudi majibu yake, maana wanatutumia kwa barua pepe. Kila Ijumaa ya wiki na tunawapatia waliopima, ila hatujawahi kumpata mgonjwa wa polio," anasema mtaalamu huyo

> "Hii chanjo inayokinga magonjwa matano siyo anachanjwa sindano tano, bali anachanjwa moja ndiyo inamkinga haya yote na mtoto anachanjwa 'combined' (nyingi kwa pamoja) kwa wakati mmoja," anasema Ngoo.



Kinamama wakipata elimu juu ya chanjo na watoto wao wenye umri chini ya miaka mitano kutoka kwa muuguzi wa Hospitali ya Mrara, Manyara.

Aina nyingine ya chanjo anaitaja ni 'PCV13' anayoieleza kuwa ni chanjo inayomkinga mtoto na maradhi Niumonia, ambayo mtoto anapatiwa pindi anafikisha umri wa wiki sita.

Ni ugonjwa unaodaiwa kuambukizwa kwa njia ya hewa na mapafu, maana unachangiwa na baridi. Ushauri wake watoto waendelee kuvalishwa sweta, kuwakinga na hali hiyo ya hewa hata kama wameshapata chanjo.

**CHANJO MAGONJWA 5**

Kingine anachokitaja Mratibu Ngoo, ni chanjo aliyoipa jina la 'DPT-HePB-HIB' ambayo chanjo inakinga wengi na magonjwa yenye madhara matano:Donda Koo, kifaduro, pepopunda.

Pia, inamkinga mtoto anapotenganishwa na mama baada ya kuzaliwa ugonjwa mwingine, ambayo mazingira yake ni sawa na 'HIV - Ukimwi,' UTI wa vichomi vidogo mgongoni.

"Hii chanjo inayokinga magonjwa matano siyo anachanjwa sindano tano, bali anachanjwa moja ndiyo inamkinga haya yote na mtoto anachanjwa 'combined' (nyingi kwa pamoja) kwa wakati mmoja," anasema Ngoo.

Chanjo nyingine anaitaja kuwakinga watoto dhidi ya kuharisha, kwani katika kipindi cha nyuma watoto wengi walikuwa wanaharisha sana. Anafafanua:"Ile Hali ya kuharisha pasipo sababu ya msingi kumepungua kwa kiasi kikubwa maana tumetoa chanjo hii kwa watoto."

**SURUA**

Ngoo anataja chanjo nyingine ni dhidi ya maradhi ya surua na rubella, akisema ni magonjwa mawili, ambayo dalili zake mtoto anakuwa na homa na vipele vidogo. Ni maradhi yasiyoangalia umri, wadogo kwa wakubwa.

Mtaalamu anasema, mtoto anapofika umri wa miezi tisa anachomwa sindano na anapotimiza miezi 18, kwa maana ya umri mwaka mmoja na nusu hadi miezi 23 anachoma nyingine.

Anataja changamoto kwenye chanjo hiyo, ni kwamba wazazi wengi wanafahamu mtoto anapotimiza miezi tisa anatakiwa apate chanjo ya kujikigha na maradhi ya surua.

"Lakini chanjo ya 'MR2' (surua) imeanza mwaka 2014 mwishoni, hivyo inasababisha wazazi kutokufahamu hii chanjo ya mwaka mmoja na nusu, hivyo wazazi wanaona watoto wamekuwa wengi wanaacha au kupuuza kupeleka watoto kliniki, hujui chanjo ni mpya ya muda mrefu," anafafanua.

Anatoa mfano wa baadhi ya kinamama, ana mimba na anaona aibu ya kuja na mwanawe mdogo, ambayo haiendani na kanuni za uzazi, hivyo anaishia kuikosa haki yake ya chanjo iwe kwake au kupitia mwanawe.

**KITOKA SERIKALINI**

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, bungeni, alipowasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yake kwa mwaka wa fedha 2017/2018 , anasema kati ya Januari na Desemba ya mwaka huo 2017, asilimia 101.2 ya watoto waliolengwa nchini, walipatiwa chanjo zote muhimu za kuwakinga na magonjwa.

Waziri Ummy anasema kuwa Tanzania imefanya vizuri katika kipindi hicho na kupongezwa na Shirika la Afya Duniani (WHO), kwa kufanya vizuri kwenye eneo la chanjo zilizolengwa.

Waziri alirejea katika nchi za Afrika, kwamba ilishika nafasi ya tatu ikiwa na asilimia 97 za kufanikisha chanjo ikitanguliwa na Zambia yenye asilimia 99 na ya pili Rwanda, yenye asilimia 98.

Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (Unicef) katika ripoti yake ya mwaka 2016, inasema karibu nusu ya watoto dunia wenye umri chini ya miaka mitano, wamefikishiwa dozi bilioni 2.5 za chanjo zilizotolewa na Umoja wa Mataifa.

Aidha, Unicef inasema bado kuna zaidi ya watoto milioni 19 duniani kote wasiopata chanjo kila mwaka, huku zaidi ya watoto milioni moja wakipoteza maisha kwa magonjwa yanayozuilika kwa chanjo.

Huku ikielezwa vifo vingi vinatokea katika nchi maskini, ripoti hiyo inazitaja nchi zilizoongoza kupewa dozi kubwa ya chanjo ni Msumbiji, Nigeria, Pakistan na Afghanistan.

AFYA

# Wafamasia ‘wajao’ wakuna vichwa kukabili matumizi holela ya dawa

## Wawajibu madaktari kero ya dawa sugu




Duka la dawa lililofungwa kwa amri ya serikali. **PICHA: MTANDAO.**

**NA VERONICA MREMA**

NI jambo linaloonekana kugeuzwa utamaduni ndani ya jamii, watu wanajiamulia ununuzi wa dawa, hasa za kutuliza maumivu, kisha wanajitibu.


Uelewa mdogo wa jamii juu kuhusu athari za wanachokifanya, ikiwamo kuweka miili yao kwenye hatari ya kutengeneza usugu wa dawa dhidi ya magonjwa mbalimbali. Ni sababu inayotajwa kuchangia hali hiyo.

Usugu wa vimelea vya magonjwa, ni kati ya athari zinazosababishwa na matumizi holela ya dawa, kwa mujibu wa wataalamu wa afya. Hivi sasa inaelezwa ni janga linalokabili dunia.

Tafiti zinaonyesha nchini hali nayo si nzuri. Tatizo la matumizi holela ya dawa hasa za kundi liitwalo ‘antimicrobial’ ambazo zaidi zinatumiwa na wataalamu watiba ama kuua au kuzuia ukuaji wa vimelea vinavyosababisha magonjwa ya kuambukiza, kwa binadamu na wanyama.

Ni kundi linalojumuisha dawa za kutibu magonjwa yanayosababishwa na bakteria ambazo ni antibaiotiki; zinazoua fangasi, kitaalamu inaitwa ‘antifungal’ vinavyoua virusi (antivirals); na parasaiti (antiparasitic) kama vile dawa za kutibu malaria.

Wataalamu wanasisistiza dawa aina za ‘antimicrobial’ ni muhimu kutibu magonjwa mbalimbali iwapo zitatumika ipasavyo, lakini matumizi yasiyo sahihi inavifanya vimelea hivyo kuwa sugu na kushindwa kutibu magonjwa yanayokusudiwa.




### Picha halisi

Tafiti za kimataifa zinaonyesha ongezeko kubwa la matumizi ya dawa hizo, kati ya mwaka 2000 na 2010, kwani yaliongezeka kwa kiwango kinachofikia asilimia 30.

Pia, takwimu hizo za Shirika la Afya Duniani (WHO) zinaonyesha katika cha mwaka 2010 pekee, kuna tani 63,200 za ‘antibaiotiki’ zilihudumia mifugo. Angalizo ni kwamba, kuna makadirio kati ya asilimia 20 na 50 ya antibiotiki hizo zinatumika isivyo sahihi na kila mwaka kuna wastani wa watu 700,000 wanaofariki dunia, kutokana na usugu wa magonjwa yanayowakabili. Utafiti unaonyesha, ikiwa hatua hazitachukuliwa dhidi ya hali hii, huenda idadi ya vifo itaongezeka duniani kufikia milioni 10 ifikapo 2050.

Athari ya mojawapo ambayo iko moja kwa moja ni kwamba, kuna hatari Pato la Taifa la kila nchi, huenda likashuka kati ya asilimia mbili hadi 3.5 kutokana na changamoto hiyo. Nini kifanyike? Kila nchi inatakiwa kuchukua hatua kupambana na matumizi holela ya antibaiotiki

Utafiti uliofanyika katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) unatoa picha kwamba dawa ya sindano ya ‘gentamycin’ ambayo imtumika kutibu UTI, ikionyesha kuongezeka usugu.

Kiwango cha usugu mwaka 2003, inaelezwa kilikuwa asilimia 6.9 ya watumiaji kwa mwaka, sasa imepanda mwaka 2011, ilipanda kufikia 44.

Katika Hospitali ya Rufani Bugando, kumeripotiwa ongezeko la usugu wa dawa ya sindano ya ‘ceftriaxone’ kutoka asilimia 14 ya mwaka 2009, hadi asilimia 29.4 mwaka 201, katika kutibu tatizo la mkojo mchafu (kutibu UTI).

Aidha, katika kutibu kifua kikuu ilionyesha usugu wa dawa kwa wagonjwa wapya asilimia 1.1 na kwa wagonjwa wanaorudia dawa baada ya kupona kuwa na usugu wa asilimia 3.9.

### Kwanini usugu?

Watafiti wanasema matumizi mabaya ya antibaiotiki ni moja ya sababu zinazochangia usugu huo, mfano hai ukitolewa pindi mtu anapoandikiwa au anapopatiwa dawa bila ya kufanyiwa uchunguzi wa kina.

Namna ya uchunguzi huo unavyofanywa, mahsusi ni kupitia maabara, kutotumia dozi sahihi ya antibiotiki wa muda alioelekezwa na mtaalamu wa afya.

Katibu wa Chama cha Wanafunzi Wafamasia Tanzania (TAPSA), Gloria Kajuna, anaiambia Nipashe kwamba sehemu kubwa ya wagonjwa huwa hawamalizi dozi wanazopewa, hali inayotoa mwanya vijidudu vilivyoko kubadilisha muundo wao, kugeuka sugu

“Kimsingi, kila mtu ana dozi yake na kila dozi ina uwezo wake wa kutibu, lakini unakuta mtu anachukua dozi iliyoachwa na mtu mwingine, anaitumia akiamini atapona ugonjwa unaomsumbua. Ni kosa!” anasema.

### Kampeni iliyopo

Gloria anasema, kutokana na hali iliyopo sasa, chama hicho cha wanafunzi kimeanzisha kampeni ya kuelimisha jamii kupitia shule za msingi, sekondari na vyuo kuhusu matumizi sahihi ya dawa.

“Tulipita pia katika hospitali mbalimbali nchini, kuelimisha kuhusu matumizi sahihi ya dawa, elimu ipo chini mno, watu hawaelewi athari ya matumizi holela ya dawa.

“Tulibaini wengi wanadhani kumeza kwa mfano zile za mara tatu kwa siku, maana yake asubuhi, mchana na jioni jambo ambalo si sahihi. Kimsingi, dawa zinapaswa kumezwa kila baada ya saa nane si vinginevyo.

“Kitendo cha kumeza dawa pasipo ushauri wa daktari ni hatari kiafya. Unaweza kuzidisha dozi, hatimaye kifo. Kitendo cha kutomaliza dozi nacho ni hatari,” anasema na kufafanua:

“Kwani hali hiyo huweza kusababisha vimelea vya magonjwa kutengeneza usugu wa dawa, mtu anajipata anatibiwa haponi, hatimaye kifo.”

### Mwelekeo ulivyo

Glory anataja athari mojawapo inayochangia ongezeko la gharama za matibabu kwa mgonjwa husika, ikiwamo fedha na muda mrefu kutumika katika matibabu, huku akihimiza:

“Angezingatia matumizi sahihi, angetibiwa, angepona na kuendelea na shughuli za kumuingizia kipato chake. Familia yake na taifa kwa ujumla, kwa maana hiyo hata taifa linapata hasara. “Ili kuongeza nguvu katika mapambano dhidi ya matumizi yasiyo sahihi ya dawa, tunakusudia kuwa na mjadala mpana katika Mkutano Mkuu wa Kada ya Wafamasia (waliopo vyuoni) nchini.”

Glory anaeleza, wanatarajia Wafamasia kati ya 350 na 500 watahudhuria mkutano huo kuchangia mada, pia namna wanavyoweza kuisaidia nchi kukabiliana na changamoto hiyo. “Tutajikita kuangazia Lengo Namba Tatu la Dunia (SDGs) ambalo linazungumza kuhusu afya. Tunataka kujua namna gani tutaweza kusaidia nchi kufikia afya bora kwa wote,” anabainisha.

Glory anaendelea: “Kwa sababu tuna jukumu kubwa kuhakikisha wananchi wanapata uelewa wa kutosha juu ya matumizi sahihi ya dawa, kwa umoja wetu tumeona tunaweza kufanya kitu kwa jamii.

“Pamoja na hili la matumizi sahihi ya dawa, tunaelimisha pia jamii kuhusu usafi wa mazingira na vijana kujitambua na kuepukana na matumizi ya dawa za kulevya.”

Rais wa TAPSA, Issaya Mbwilo, anasema kongamano hilo linatarajiwa kufanyika kati ya Juni 14 hadi 16 (kesho hadi Jumamosi) mwaka huu. Litashirikisha vyuo 16 vinavyotoa mafunzo kwa ngazi ya stashahada na shahada katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## Mganga Mkuu Morogoro asimulia wanavyojihami ‘hodi’ ya dengue

**INATOKA UK.17**

zuia mbu,” anasema.

Mkazi Moro

Mkazi wa Kata ya Lukobe, Manispaa ya Morogoro, Getruda Raphael, anasema amejiandaa kujikinga na ugonjwa wa dengue, kwa kutumia chandarua wakati anapotaka kulala huku akifunga mlango wa chumbani mwake kuzuia mbu wasiingie.

Raphael anakiri kufuata masharti kwamba hivi sasa huwa anavaa nguo ndefu kujikinga na mbu wasimng’ate kukwepa maambukizi.

Anasema, suala la usafi wa kila mwisho wa mwezi linabeba mtazamo wa agizo la serikali linalozingatiwa, licha ya kwamba bado madimbwi yamejaa mazalia ya mbu na hajawahi kushuhudia mamlaka za kiserikali zikipita kumwaga dawa katika makazi yake.

Getruda ana wito kwa serikali kwamba hivi sasa inapaswa kujitahidi kumwaga dawa kwenye madimbwi ya maji yaliyotuama, kama ilivyokuwa zamani tena katika mtazamo unaogusa anachokitaja ‘nyumba kwa nyumba’ kuzuia mazalia ya wadudu wanaoruka na kutambaa.





## Jamii yahimizwa elimu ya watoto

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

JAMII imeshauriwa kuwapa watoto wao elimu ili waweze kuondokana na adui ujinga, na kuachana na dhana potofu ya kuruhusu watumikishwe katika ajira mbaya.

Ajira hizo ni za migodini, hotelini na majumbani, ambako huambulia mateso na manyanyaso.

Wito huo ulitolewa jana na mwimbaji wa nyimbo za injili, nchini Anna George, alipokuwa akizungumza na Nipashe kuhusu maadhimisho ya Mtoto wa Afrika ambayo hufanyika kila mwaka Juni 16.

Anna alisema waimbaji wa nyimbo za injili nchini wamekuwa mstari wa mbele kukemea vitendo vya unyanyasaji kwa watoto kupitia nyimbo zao na kwamba wengine wamekuwa wakiandaa mikutano kupinga vitendo vya ukatili wa watoto.

Mwimbaji huyo ambaye ni mwanaharakati wa kupinga vitendo vya ukatili kwa watoto wenye ualbino na utumikishwaji wa watoto, amekuwa akitoa elimu ya kupinga vitendo hivyo kupitia nyimbo zake.

“Natumia karama yangu ya uimbaji kufikisha ujumbe kwa jamii kuhusiana na vitendo vya unyanyasaji kwa watoto wenye ualbino na watoto wengine mpaka sasa nimetoa albamu mbili zote zikizungumzia madhira wanayokumbana nayo watoto na kuiasa jamii kuachana na vitendo vya kuwanyanyasa na kuwatumikisha watoto,” alisema Anna.

Alisema taifa lolote haliwezi kutengeneza kizazi kizuri cha baadae kama hawatengenezewa msingi mzuri wa malezi bora na elimu na ili hilo lifanikiwe watu waache kuwaajiri watoto majumbani au migodini.

Aliongeza kuwa kauli mbiu ya mwaka huu ya siku ya Mtoto wa Afrika inayosema ‘Mtoto ni Msingi wa Taifa Endelevu, Tumtunze, Tumlinde na Kumuendeleza’ inaikumbusha jamii kuachana na dhana potofu za kuwatumikisha watoto katika miradi yao na kuwanyanya kingono badala yake itoe nafasi ya kumpa elimu bora ambayo ndio mkombozi wake.

Aliisisitiza jamii kutunga sheria ndogo ambazo zitaendelea kumlinda mtoto katika maeneo husika ukiwamo ulinzi wa mtoto na kupata elimu na kwamba atakayekiuka achukuliwe hatua.

# Msako mafundi wasiopitia Veta mwakani

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

SERIKALI imesema kufikia mwaka 2020 itaanza msako maalum wa kuwabaini mafundi wanaofanya kazi za ufundi bila kuwa na mafunzo kutoka Chuo cha Mamlaka ya Ufundi Stadi (VETA) ili kudhibiti mafundi wasio na sifa ambao wanachangia kutengeneza vitu visivyo na ubora.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, wakati wa kikao cha pamoja na watumishi wa Chuo cha Veta jijini Mbeya, ambapo alisema mafundi wengi wanatumia uzoefu kufanya kazi zao hali inayosababisha kutengeneza vitu visivyokuwa na ubora.

Alisema oparesheni ya kukagua mafundi ifikapo mwaka 2020 itakuwa na tija kwa kuwa itawasaidia mafundi wasio na ujuzi kuongeza maarifa zaidi na kutengeneza vitu vyenye ubora.

“Vyuo vya ufundi nchini vina mchango mkubwa wa kuliletea taifa maendeleo kwa sababu linazalisha vijana wenye ujuzi nitahakikisha kufikia mwaka 2020 kila fundi huko mitaani atatakiwa kuwa na cheti kutoka Veta na ambaye hatakuwanacho, lazima akasome,” alisema Chalamila.

Alisisitiza wananchi kuacha tabia ya kuwatumia mafundi wasiokuwa na ujuzi kujenga au kutengeneza vitu vyao kwa sababu ya gharama nafuu badala yake wawatumie mafundi wenye ujuzi ambao wanatengeneza vitu vyenye ubora. “Mtu unailipua nyumba kwa sababu ya kumtumia fundi mwenye gharama nafuu ambaye atakununulia vifaa feki na hii tabia inaendekezwa na wananchi wenyewe kwani wanapenda kuwatumia mafundi wa mitaani wanawaogopa mafundi wa Veta,” alisema Chalamila.

Mkurugenzi Chuo cha Ufundi Veta Kanda ya Kusini Magharibi, Justine Rutta, alisema oparesheni hiyo itakuwa ni ya mfano mkoani Mbeya na kwamba Chuo kipo tayari kupokea vijana hao.

Alisema kupitia oparesheni hiyo Chuo cha Veta kitaendelea kuzalisha vijana wengi ambao tayari wana uzoefu na ujuzi wa kile wanachokifanya.



Katibu Tawala wa Wilaya ya Sumbawanga, Christina Mzena, akikata utepe kuashiria uzinduzi rasmi wa mnara wa 4G wa Tigo, wilayani humo, mkoani Rukwa jana. Wanaoshangilia ni baadhi ya wafanyakazi wa Tigo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watoto wenye ulemavu waomba baiskeli

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

WATOTO zaidi ya 57 wenye ulemavu wa viungo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, wameiomba Serikali na wadau kuwasaidia kupata baiskeli maalumu ambazo zitawawezesha kufika maeneo mbalimbali ikiwamo shuleni.


Akizungumza jana kwa niaba ya watoto wenzake, Faraja Msigwa (12), alisema wanakabiliwa na changamoto mbalimbali kutokana na ulemavu walionao, lakini kwa sasa wanahitaji baiskeli ili ziwasaidie kufika shuleni na maeneo mengine kiurahisi. Alisema ukosefu wa vifaa kama baiskeli imekuwa ni changamoto kubwa kwao na kuwafanya wajihisi wanyonge wakidai jamii inawaona kama watoto wasio kuwa na haki ya kupata elimu kama watoto wengine.

“Tunaomba Serikali na wadau watusaidie baiskeli, tunapata adha kubwa tunapokuwa njiani kwenda shuleni ukilinganisha na watoto wengine...tunachelewa vipindi vya masomo darasani hali inayosababisha kushindwa kufanya vizuri kwenye mitihani tunaomba wadau watusaidie,” alisema Faraja.

Mkurugenzi wa Shirika lisilokuwa la kiserikali la Child Of Tanzania, Dafroza Mbota, alisema kutokana na watoto wenye ulemavu wa viungo kukabiliana na changamoto mbalimbali, waliamua kuanzisha Shirika hilo kwa lengo la kuwawezesha watoto wenye ulemavu kupelekwa shuleni na kupata huduma nyingine za msingi. Dafroza alisema licha ya Shirika h

ilo kuendelea kutoa elimu kwa jamii na kuwakusanya watoto wenye ulemavu kukaa sehemu moja bado kinakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo ya baiskeli za walemavu na usafiri wa gari wa kuwafikisha kituoni kusoma.

Alisema kutokana na umuhimu wa kuhakikisha watoto wenye ulemavu wanapata haki ya elimu, wazazi na walezi wanatakiwa kuwapeleka watoto wenye ulemavu katika vituo vya kulelea yatima ili wapate mahitaji kuliko kuwaficha ndani na kuachana na imani potofu kuwa kuzaa watoto wenye ulemavu ni mkosi.





# Mikataba yote ujenzi kupitiwa Julai

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imesema hadi kufikia Julai mwaka huu, itakuwa imepitia upya mikataba yote ya miradi ya ujenzi ili kuwawezesha makandarasi wazawa kushirikishwa katika miradi hiyo.

Aidha, serikali imesema hadi kufikia muda huo, miradi yote itakuwa inaonyesha kazi zipi zitakazokuwa zinafanywa na makandarasi wazawa na wa nje. Hayo yalibainishwa jana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi anayeshughulikia Ujenzi, Elius Mwakalinga, katika mkutano na makandarasi kutoka mikoa mbalimbali uliofanyika jijini Dodoma. Mwakalinga alisema kutokana na hilo, imeunda menejimenti ambayo imejumuisha wataalamu waliobobea katika sekta hiyo wakiwamo wastaafu ili kupitia kwa ufasaha sheria zilizomo ndani ya miradi husika.

Alisema lengo la kufanya hivyo ni pamoja na kutaka kuona wapi ina upungufu ambao unaweza kurekebishwa ili makandarasi wazawa wanufaike nayo pale inapoanza kutumika katika maeneo mbalimbali.

Alisema upitiaji utafanyika kwa haraka chini ya menejimenti iliyo undwa ambapo wao wanaamini itafanya vizuri ili kulegeza masharti ambayo makandarasi wazawa wamekuwa wakiyalalamikia kila uchao ambayo yanawabana wao na kushindwa kufanya kazi za miradi.

"Kuanzia Julai miradi yote itakuwa imejulikana kazi ipi itakuwa ya mkandarasi mzawa na ipi itakuwa inafanywa na mkandarasi wa nje" alisema Mwakalinga.

Alisema jambo la msingi ni wote kuwa wakweli katika suala zima la miradi hiyo na sio kuzungukana katika kazi ambazo serikali imezipanga kufanya kupitia makandarasi wake na wao kuleta majungu ili kuhujumu miradi isisonge mbele.

Hata hivyo, alisema moja ya mikakati ya Serikali iliowekwa ni kuhakikisha mtaalamu atakayewekwa hakuna kutolewa labda itokee amepata tatizo au afariki lakini sio kuondoka kwa majungu.

"Hakuna mtaalamu atakayeondoka baada ya kupitia miradi nimesikia kunashida ya kukwazana ili mtaalamu aondoke na mkandarasi kuleta mtu anayemtaka yeye," alisema Mwakalinga.

Alisema kuanzia sasa anaamini shughuli ya kubadilisha wataalamu haitakuwapo na badala yake mtaalamu ambaye atakuwa kaletwa na Tanroads atafanya kazi hadi mwisho labda itokee dharura ya kubadilishwa na wahusika wenyewe au kifo.

Mbali na hilo, alisema mkakati mwingine ambao Serikali imeweka ni kuwajengea uwezo ikiwamo kuwapatia vifaa ili wawe na ushindani, lakini pia wanatakiwa kuwa na uhakika na kile wanachokifanya.

Alisema taasisi hizo zinatakiwa ziwe zimelenga utendaji kazi ambapo kazi ya Serikali ni kuwekeza katika mitambo, mtaji na umahili wa kufanya kazi ikiwamo elimu itolewe kwa watu ambao wanafanya kazi.

Alisema vijijini ambako miradi hiyo inapelekwa watu wafanyiwe usaili na makandarasi kuchagua watu wanaotaka ambao watapatiwa mafunzo ili kwenda sambamba na kile wanachohitaji.

Akizungumzia changamoto zinazowakabili makandarasi wazawa, alisema watazifanyia kazi ikiwamo kuangalia masharti magumu ya upandishwaji wa viwango vya kampuni za makandarasi.

Hata hivyo, alisema pamoja na hayo anaamini kupitia mikakati iliowekwa hakuna kitakachoharibika unyanyapaa katika taasisi za umma hautakuwapo tena.

Akizungumzia suala la rushwa alisema jambo hilo ni la wote, kwa sababu linapaswa kupigwa vita na kila mmoja.

Wakizungumzia changamoto zinazo wakabili, mkandarasi toka Mbeya, Kulwa Mayuma, alisema rushwa nyingi imetawala katika kazi za miradi zinazofanywa jambo ambalo makandarasi wengi wanashindwa kupata kazi za kufanya ilhali wana uwezo wa kuzifanya.



Wafanyakazi wa kampuni ya usafi ya Green West, wakizoa taka katika eneo la Uhindini, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Watakiwa kutengeneza mifuko yenye ubora

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAJASIRIAMALI wanaojihusisha na utengenezaji mifuko mbadala wakiwamo wanawake na vijana, wametakiwa kutengeneza yenye viwango na ubora ili kuingia kwenye ushindani wa masoko. Ushauri huo umetolea na Katibu wa Ushirika wa Mama Wakristo (UMAKI) wa Kanisa Anglikana Tanzania, Margereth Massawa, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa. Alisema utengenezaji wa mifuko katika viwango vya ubora utawawezesha wajasiriamali kupata faida na kujiongezea uchumi, kulinda afya pamoja na kuhifadhi mazingira. Aidha, aliiomba serikali upatikanaji wa malighafi kuwa wa urahisi ikiwa ni pamoja na bei rafiki kwa wajasiriamali walio wengi itakayowezesha kumudu bei.

Alisema upatikanaji wa malighafi umekuwa ni changamoto kwa wajasiriamali wa ngazi ya chini, hali inayowafanya kushindwa kufikia malengo ya kiuchumi na hata kwenye upande wa masoko.

Aidha, ameiomba serikali na taasisi mbalimbali kutoa mafunzo kwa wajasiriamali jinsi utengenezaji wa viwango vinavyokubalika kwa kutumia mashirika yao kama vile Shirika la Viwanda Vidogo (SIDO).

Alisema changamoto kubwa iliyopo kwa wajasiriamali wengi hawapati mafunzo ya elimu na kutambua faida inayotokana na ujasiriamali huo.

## Siku 18 ujenzi kituo cha afya

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

UONGOZI wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, umepewa siku 18 kuhakikisha unakamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya Mkonze kwa asilimia 100.

Agizo hilo lilitolewa jana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa kituo hicho.

Kituo hicho ni moja ya vituo vya kutolea huduma za afya 352 vinavyojengwa nchini na vipo katika Mpango wa Kuboresha Huduma za Afya katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Akizungumza katika ziara hiyo, Waziri Jafo alisema mpango huo unalenga kujenga majengo sita kwenye kila kituo cha afya ambayo ni chumba cha upasuaji, wodi ya mama na mtoto, maabara, nyumba ya mganga, chumba cha kufulia na kuchomea taka

Alibainisha kuwa Juni 26, mwaka jana, Serikali ilitoa Sh. Milioni 400 kwa ajili ya Kituo cha Mkonze ambacho ilitakiwa kukamilika mwisho wa mwaka jana, na waliongeza muda hadi Aprili mwaka huu.

" Nimekuja Mkonze nikitarajia nitakuta kituo kimekamilika, lakini bahati mbaya nimekuta kituo hakijamilika," alisema.

Alisema hajaridhishwa na kazi iliyofanyika kwenye kituo hicho kwa kuwa fedha zilizotolewa kwenye vituo vingine wamekamilisha.

Jafo alisema juzi alitembelea vituo vya afya kadhaa Mkoa wa Lindi, vituo ambavyo walivipa fedha sawa na hicho cha Mkonze, lakini vimekamilisha ujenzi.

"Nimetoa maelekezo ifikapo Juni 30, mwaka huu kituo kile kiwe kimekamilika kwa asilimia 100 nataka siku hizi chache zilizobakia Jiji la Dodoma lihakikishe linakamilisha na nitarudi tena kuangalia," alisisitiza.


Mkurugenzi wa Jiji hilo, Godwin Kunambi, alisema walipatiwa Sh. milioni 400 kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho lakini jiji liliamua kujenga kituo chenye hadhi ya Sh. milioni 500.

Kuhusu maagizo, aliahidi kuwa kituo cha afya cha Mkonze kitakamilika kama alivyoagiza kwasababu fedha ipo tayari.

"Mimi na Mkuu wa Wilaya (Patrobas Katambi) tutafanya kazi usiku na mchana chini ya usimamizi wa Mkuu wa Mkoa,"alisema.

Wakati huo huo, Waziri Jafo ameridhishwa na maendeleo ya ujenzi wa barabara ya Kikuyu-Chidachi-Kinyambwe-Itega yenye urefu wa kilomita 6 inayojengwa kwa lami kwa thamani ya Sh. bilioni 9 na Kampuni ya STECLO.

Kwa upande wa barabara ya urefu wa kilimita 1.85 ya Martin Luther-Swaswa inajoyengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 1.3, Jafo alimuagiza mkandarasi kuhakikisha anapeleka vifaa vingine ili kazi ya barabara ikamilike.





Mbunge wa Jimbo la Morogoro Mjini (CCM), AbdulAziz Abood (kushoto kwa aliyevaa kofia), akiwasikiliza baadhi ya wapigadebe wa stendi ya mabasi yaendayo mikaoni ya Msamvu iliyopo Manispaa ya Morogoro, baada ya kumsimamisha alipopita eneo hilo ili kumpa kero zao, **PICHA NA ASHTON BALAIGWA**

# SMZ kununua boti tano za kisasa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi, wameipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kwa kutangaza nia ya kununua boti za kisasa za kutoa huduma ya usafiri kwa wananchi wa visiwa vya Unguja na Pemba.

Mwakilishi wa Jimbo la Kisiwani Pemba, Mussa Foum Mussa alitoa pongezi hizo wakati akichangia bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji iliyowasilishwa na Waziri wa Wizara hiyo, Dk.Sira Umbwa Mamboya.

Mussa alimpongeza Rais wa Zanzibar Dk.Ali Mohamed Shein, kwa nia yake ya kununuwa boti tano kwa ajili ya kutoa huduma za usafiri kwa wananchi wanaoishi katika sehemu ya visiwa.

Alisema nia hiyo ilitangazwa na Rais Shein wakati alipokuwa akitangaza sera na kunadi Ilani ya uchaguzi katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

"Nampongeza kwa dhati kabisa Rais Shein kwa kutekeleza nia yake ya kununuwa boti tano za huduma ya usafiri kwa wananchi wanaoishi katika visiwa vidogo vya Unguja na Pemba,"alisema.

Hata hivyo, Mussa alitaka apewe ufafanuzi kwa nini kisiwa cha Shamiani kilichopo Pemba hakimo katika orodha ya visiwa vitakavyopatiwa boti ya usafiri wakati kisiwa hicho kinaishi watu.

"Mheshimiwa Spika, namuomba Waziri aniambie kwa nini kisiwa cha Shamiani Pemba hakimo katika orodha ya visiwa vitakavyopata boti,"alisema.

Mwakilishi wa Jimbo la Chake Chake Pemba, Suleiman Sarhani, alisema katika kipindi cha uongozi wa Rais Shein, kisiwa cha Pemba kimepata neema kubwa katika sekta mbali mbali ikiwamo mawasiliano na nishati ya umeme.

Alisema utekelezaji wa lengo hilo kwa kiasi kikubwa utasaidia kuimarisha usafiri wa wananchi pamoja na kuwapo kwa usalama wa maisha ya wananchi.

"Mheshimiwa Spika sisi wawakilishi kutoka Pemba tunampongeza kwa dhati Rais Shein kwa nia yake ya kununua boti ambazo zitatoa huduma za usafiri kwa wananchi wanaoishi katika visiwa vidogo vidogo,"alisema.

Aidha, Mwakilishi wa Viti Maalumu, Viwe Khamis, alisema uamuzi wa kununua boti za kutoa huduma za usafiri kwa wananchi wanaoishi katika visiwa vidogo vidogo utasaidia sana kuokoa maisha ya wanawake na watoto kuwa salama.

"Tumefurahishwa na uamuzi wa Rais Shein kutangaza kununuwa boti tano zitakazotoa huduma katika visiwa vidogo vidogo vilivyopo Unguja na Pemba na hivyo kuwahakikishia usalama wanawake na watoto,"alisema.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji imepanga kununua boti tano zitakazotoa huduma za usafiri katika visiwa vidogo vidogo vilivyopo Unguja na Pemba.

Visiwa hivyo ni Fundo, Kisiwa Panza, Makoongwe pamoja na Kojani kwa upande wa Pemba na Unguja ni Tumbatu.

# Usafirishaji watoto wakithiri Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, Mauldline Cyrus Castico, amesema kumekuwa na wimbi kubwa la usafirishaji haramu wa watoto ambapo watoto hao hutolewa Tanzania Bara na kuletwa Zanzibar kufanya kazi za ndani.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu siku ya kupambana na ajira za watoto, Castico alisema kuwa watoto hao wengi wao hutelekezwa bandarini Zanzibar.

"Watoto hao hutolewa mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara huagizwa wapande basi wakifika Dar es Salaam wapande boti ya kuja Zanzibar na wakishafika Zanzibar wengi wao hutelekezwa kwa sababu ni wageni na hawajui wanapokwenda,"alisema.

Alieleza kuwa Serikali imeshawarejesha watoto wengi wa namna hiyo ambao hutelekezwa bandarini na wanapohojiwa hueleza kuwa wamekuja kufanya kazi za ndani lakini mwenyeji wao hawajaonana.

Alisema kuwa watoto hao huletwa na mawakala ambao wamekuwa wakifanya kazi ya kuwasafirisha watoto kinyume na Sheria. Waziri Castiko aliwataka wazazi na walezi kutowaruhusu watoto wao kufanya kazi za majumbani wakiwa bado hawajafikia umri wa miaka 18 kwani wengi wao huwa wanadhalilishwa. Aidha, alisema jumla ya watoto 25,803 wako katika ajira Zanzibar na wengi wao ni chini ya miaka 18.

Alieleza kuwa, watoto hao hufanya kazi za uvuvi, uvunjaji kokoto na biashara ndogo ndogo hali ambayo inawakosesha haki yao ya msingi ya kupata elimu.

Alisema SMZ imechukuwa hatua mbalimbali katika kukabiliana na suala la ajira za watoto ikiwa ni pamoja na kuanzisha Sheria ya Ajira Namba 11 ya Mwaka 2005, Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2011 pamoja na mikakati ya kuwawezesha wananchi kiuchumi.

Hata hivyo, alisema serikali kupitia wizara yake imefanya juhudi kuelimisha jamii kuhusu madhara yatokayo na ajira za watoto na kutumia mbinu mbalimbali za kuepukana na ajira hizo ikiwamo kuzitembelea sehemu zinazoaminika kuwa kuna ajira hizo pamoja na kuwatoa watoto katika ajira.

Kila ifikapo Juni 12 dunia huadhimisha siku ya kupambana na ajira za watoto ambapo kauli mbiu kwa mwaka huu ni "Watoto wasifanye kazi kivitendo bali wafanye kazi kwenye ndoto".

# Kesi udhalilishaji kijinsia zafutwa kwa kukosa mashahidi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

LICHA ya Sheria ya Ushahidi kufanyiwa marekebisho lakini bado sheria hiyo ina upungufu hasa kwa kesi za udhalilishaji wa kijinsia.

Hayo yalisemwa jana na Suleiman Jaku Juma kutoka Dawati la Jinsia mkokotoni, ambaye alisema Sheria hiyo haijamlazimisha shahidi ambaye anakataa kwenda kutoa ushahidi mahakamani na ndiyo maana kesi nyingi zinashindwa kupatiwa hukumu kutokana na kukosa ushahidi.

Alisema kuwa wanaofanya vitendo hivyo ni watu wa karibu katika familia hivyo jamii huamua kusuluhishana wenyewe ikiwemo kuwafungisha ndoa mtuhumiwa wa udhalilishaji na mwathiriwa aliyedhalilishwa.

Alisema ni vigumu mke kumtolea ushahidi mume mahakamani kwani jamii hukimbilia kufungisha ndoa ili kesi hiyo isiweze kusonga mbele na haki kuweza kupatikana.

Alieleza kuwa jumla ya kesi 88 za udhalilishaji wa kijinsia zimeripotiwa kwa mwaka 2018 katika Wilaya ya Kaskazini A Unguja huku kesi 20 zikiwa zimeripotiwa kuanzia Januari hadi Mei mwaka huu.

Alisema kwa kesi hizo za mwaka 2018 kesi 11 zinaendelea kusikilizwa mahakamani, mbili zimepata hatia, mbili zimeondolewa mahakamani ,49 zimefungwa na saba zipo kwa Mkurugenzi wa Mashtaka na kesi mbili zinasubiri uchunguzi wa vinasaba yaani DNA.

"Kesi nyingi zimefungwa kutokana na kukosa mashahidi mahakamani na hivi sasa wananchi wamekuwa na uelewa katika kuyaripoti matukio ya udhalilishaji lakini wamekuwa wagumu kwenda mahakamani kutoa ushahidi,"alisema.

Naye Kanuni Vuai Khamis, ambaye ni mwanaharakati wa kupinga vitendo vya udhalilishaji kutoka wilaya hiyo, alisema kuwa mashekhe wanaofungisha ndoa kwa watuhumiwa wa kesi hizo nao wanachangia kuendelea kuwapo kwa vitendo vya udhalilishaji.

Alishauri kuwa ni vyema mashekhe wakatae kufungisha ndoa kwa wale watuhumiwa wanaowadhalilisha wanawake na watoto ili kesi hizo ziweze kupatiwa hukumu mahakamani.

Kwa upande wake, Bakari Faki Mcha, Mwenyekiti wa Masheha wa wilaya hiyo, alisema jamii imekuwa na uelewa kuhusu udhalilishaji na ndiyo maana wamekuwa wakiyaripoti matukio hayo lakini changamoto kubwa iliyopo ni rushwa katika kesi hizo.

# TTB yabuni mkakati mpya wa kutangaza vivutio vya utalii

**Na Beatrice Philemon**

BODI ya Utalii Tanzania (TTB), inatarajia kufungua ofisi mpya katika Uwanja wa Kimataifa wa Ndege wa Julius Nyerere (JNIA) (Terminal 3) ili kutangaza vivutio vya utalii.

Aidha, lengo ni kusaidia watalii watakapopata tatizo pamoja na kuwapa taarifa sahihi kuhusu vivutio vya utalii wanavyotaka kutembelea wakiwa nchini.

Akizungumza na Nipashe, Mwenyekiti wa TTB, Jaji mstaafu Thomas Mihayo, alisema kuwa kupitia ofisi hiyo itakuwa rahisi kwa Tanzania kutangaza vivutio vyake vya utalii kwa sababu wageni watakaokuwa wakija nchini kwa ajili ya mikutano ya Kimataifa watapewa vipeperushi vinavyoelezea utalii wa Tanzania.

"Hivi sasa itakuwa rahisi kwa watalii kupata msaada wa haraka kwa sababu miaka ya nyuma kuna baadhi ya wakala wa usafirishaji watalii alileta watalii wanne nchini na watalii hao walipofika uwanja wa ndege hawakumuona mwenyeji wao, na fedha walikuwa wameshalipa na sisi kama bodi hatutaki watalii wanaokuja hapa nchini wapate changamoto hizo," alisema.

Alisema JNIA kutakuwa na matangazo yanayoelezea utalii wa Tanzania kwa ujumla na jinsi ya kutembelea maeneo hayo.

Katika hatua nyingine, TTB imeingia makubaliano na Benki ya NMB ili watalii wakifika uwanja wa ndege iwe rahisi kubadilisha fedha zao.

Jaji Mihayo alisema lengo kuu ni kutangaza vivutio vya utalii wa Tanzania na kusaidia watalii kupata huduma nzuri na kwa muda mwafaka wanapowasili nchini.

Vilevile, alisema katika mwaka ujao wa fedha 2019/2020 TTB itaendelea kufungua masoko mapya ya utalii katika nchi za Thailand, Malaysia, India, Korea Kusini, Russia pamoja na nchi nyingine za mashariki ya mbali na Skandinavia.

Ili kutimiza lengo hilo, Serikali imeipatia TTB jumla ya Sh. bilioni 10.2 kwa ajili ya shughuli zote za mishahara na utangazaji wa utalii kwa mwaka ujao wa fedha wa 2019/2020.

"Mwaka huu tutakwenda kufungua masoko mapya ya utalii ili kuvutia watalii wengi zaidi kuja kutembelea vivutio vya utalii nchini," alisema

Ingawa alisema fedha walizopata hazitoshelezi kutekeleza shughuli zote zilizopangwa kwa ajili ya kutangaza utalii, Bodi itahakikisha inatumia fedha hizo kutangaza vivutio vya utalii ili kuongeza idadi ya watalii na kuiwezesha Tanzania kujulikana zaidi ulimwenguni kwa vivutio vizuri ilivyonavyo.

Aidha, TTB itashirikiana na mabalozi wanaoiwakilisha Tanzania nje kutangaza vivutio vya utalii.



Mkuu wa Wilaya ya Uyui mkoani Tabora, Gift Msuya na Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya JTI Leaf Services, John Gauna (wa pili kushoto), wakizindua madarasa mapya yaliyokabidhiwa kwa Shule ya Msingi ya Chali kupitia programu ya JTI Leaf ijulikanayo kama ARISE. Wengine kutoka kushoto ni Mkuu wa Shule ya Msingi ya Chali, Bwire Mbuya na Diwani wa Kata ya Ndono, Haruna Ruwambo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mapato Bandari ya Kigoma yaongezeka

**Na Mary Geofrey,** KIGOMA

IDADI ya meli zinazohudumiwa katika Bandari ya Kigoma zimeongezeka katika kipindi cha miaka mitano kutoka 296 mwaka 2013/14 hadi 434 mwaka 2017/18. Kadhalika shehena inayohudumiwa katika bandari hiyo imeongezeka kutoka tani 88,390 mwaka 2013/14 hadi 196,844 mwaka 2017/18.

Meneja wa Bandari ya Ziwa Tanganyika, Ajuaye Msese, aliyaeleza hayo jana, mkoani hapo, wakati akizungumza na waandishi wa habari waliotembelea bandari hiyo kwa ajili ya kushuhudia miradi ya maendeleo inayotelekezwa na Mamlaka ya Bandari (TPA) katika ziwa hilo.

Alisema shehena wanazohudumia katika Bandari ya Kigoma ni mchanganyiko wa mafuta na makasha yanayotoka na kuelekea katika nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo na Burundi. "Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita kuanzia mwaka 2013 hadi 2018, idadi ya meli tunazohudumia katika bandari hii imeongezeka, pamoja na idadi ya shehena tunayohudumia jambo lililosababisha bandari kukusanya Sh. milioni 18.446 sawa na ongezeko la asilimia 29.2 katika kipindi hicho," alieleza Msese.

Kuhusu mapato hayo alisema mwaka 2013/14 walikusanya Sh. milioni 2.793 hadi Sh. milioni 6.752 mwaka 2017/18.

Alisema bandari hiyo iliyodumu kwa miaka 100 inategemea reli ya kati na inahudumia nchi nne za Zambia, Congo, Burundi na Rwanda. "Aidha, kwa mwaka wa fedha 2019/20 mamlaka imepanga kununua 'forklift' mbili kwa ajili ya Bandari ya Kipili na 'Terminal Tractor' yenye uwezo wa kubeba tani 40.

# Mtandao 4G waunganisha wateja Tigo Sumbawanga

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Tigo imezindua mtandao wenye kasi wa 4G mjini Sumbawanga, utakaowawezesha wateja wake kupata huduma bora ya intanet, kupiga na kupokea simu, pamoja na ujumbe mfupi wa maneno (SMS).

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa Mnara wa 4G mjini Sumbawanga, Meneja Tigo wa Kanda ya KusinI, Ladislaus Karlo, alisema mnara huo ulioongezwa ufanisi kutoka 3G kwenda 4G umeimarishwa ili kuweza kupitisha mfumo wa data kwa haraka zaidi, hivyo kuwezesha miamala ya fedha na huduma ya intanet kuwa ya kasi zaidi.

"Kama mnavyofahamu, Sumbawanga ni makao makuu ya mkoa wa Rukwa, hivyo kupelekea mji huu kuwa kiungo muhimu wa shughuli za kiuchumi...hapa ndipo faida ya mtandao huu wa 4G unapoweza kudhihirika, katika kuwezesha biashara na kurahisisha upatikanaji wa taarifa na habari kwa kasi zaidi," alisema Karlo wakati wa uzinduzi wa mnara huo mpya wa 4G.

Karlo alisisitiza pia kwamba wateja wa Tigo sasa wataweza kutumia mtandao ulioi mara, usiokuwa na vikwazo, ambao utawawezesha kufanya shughuli zinazotumia kiwango kikubwa cha intanet, kama kutazama video, kusikiliza muziki, na kutuma na kupokea habari mtandaoni bila wasiwasi wowote.

"Wateja wetu wa hapa Sumbawanga ambao watahudumiwa katika eneo la mnara huu wa 4G watapata ofa maalum, watazawadiwa GB 4 za intanet bure pale wanapobadilisha laini zao za simu kuingia 4G. Wateja wataweza kutumia kifurushi hichi cha intanet kwa muda wa siku 7," alisema Karlo. Karlo pia aliwakumbusha wateja wa Tigo Sumbawanga kuwa wanaweza wakapata ofa mpya ya 'Saizi Yako' ambayo inamwezesha kila mteja kupata ofa bora ya kupiga, kupokea simu, intanet na SMS iliyo mahususi na kuendana na mahitaji yao binafsi. Kujiunga na ofa hiyo, piga *147*00# au *148*00#."

"Kipaumbele chetu ni kuhakikisha kwamba wateja wetu wanapata huduma za teknolojia za kisasa kama vile mtandao wa 4G. Pia ni muhimu kutambua kwamba, teknolojia ya 4G imeongeza idadi kubwa ya watu kuunganishwa na intanet kupitia simu na pia imefungulia jamii zilizopo vijijini kuweza kupata huduma za kielektroniki katika nyanja za kibiashara, afya, elimu na serikali ambazo walishindwa kupata huko nyuma," alisema Karlo.

Mnara wa Sumbawanga ni wa nne kuzinduliwa baada ya uzinduzi wa minara iliyopo Mpanda, Katavi; Kilolo, Iringa na Bariadi. Jumla ya minara 52 itazinduliwa katika kampeni hii ya nchi nzima kwenye maeneo mbali mbali ikiwa ni pamoja na kanda ya Ziwa, Kaskazini, Pwani na Kusini.

# Apigwa risasi kwa kuingia Ikulu

**NAIROBI, Kenya**

MWANAFUNZI wa Chuo Kikuu cha Kilimo na Teknolojia cha Jomo Kenyatta (JKUAT) nchini Kenya, Brian Bera, amepigwa risasi na polisi baada ya kuingia Ikulu ya Nairobi kinyume cha sheria.

Bera (25) amelazwa katika Hospitali ya Kitaifa ya Kenyatta, alifikwa na mkasa huo baada ya kupanda geti mojawapo la Ikulu.

Alipigwa risasi na kujeruhiwa bega la kushoto na maofisa wa polisi waliokuwa doria kwenye lango hilo baada ya kuchomoa kisu alipoagizwa asimame.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa siku ya Jumapili Jioni, Kibet aliandika katika mtandao wa kijamii wa Facebook kuwa atain-gia Ikulu.

Kwa mujibu wa msemaji wa Ikulu, Kanze Dena-Mararo, Kisa hicho kilitokea Jumatatu na mshukiwa alipelekwa katika Kituo cha Polisi cha Kileleshwa na kusajiliwa katika Kitabu cha Matukio nambari 39 kabla ya kupelekwa katika Hospitali ya Kitaifa ya Kenyatta kwa matibabu.

"Tunachukua fursa hii kukumbusha umma kwamba Ikulu ni mahali palipotengwa kuwa chini ya ulinzi mkali kwa mujibu wa Sheria ya Maeneo yanayolindwa. Kwa sababu hiyo, hakuna mtu yeyote anayeruhusiwa kuingia Ikulu pasipo na ruhusa ya mamlaka yenye jukumu hilo." alisema Kanze.

Aliongeza kuwa uchunguzi unaendelea kubaini nia ya mshukiwa huyo kuingia Ikulu kinyume cha sheria na hatua kali zitachukuliwa dhidi yake baada ya uchunguzi kukamilika.

Tukio hilo limezua mjadala mkali katika mitandao ya kijamii nchini Kenya huku baadhi ya watu wakihoji kwanini mwanafunzi huyo aliamua kuchukua hatua hiyo.

Wengi wameeleza kuwa huenda alichukua hatua hiyo baada ya kutumia kileo fulani kwa sababu mtu aliye na akili timamu hawezi kudhubutu kufanya hivyo.

Hata hivyo, baadhi ya watu kwenye mtandao wa kijamii wa Twitter walimpongeza kijana huyo kwa kufanya kitendo hicho.

Danvas Nyabasa alieleza kuwa: "Kibet sio mwendawazimu bali ana hasira kama mtu mwingine yeyote anaehisi kunyanyasika kutokana na hali ngumu ya maisha".

Nyabasa: "Rais atarajie wageni zaidi ikiwa hataingilia kati kuwasaidia Wakenya wanaoozongwa na umasikini na kutoa wito kwa mamlaka kuingilia kati suala hilo"

*BBC*

# Mke amtetea mume aliyeua watoto wake watano

**WASHINGTON, Marekani**

MWANAMKE mmoja nchini Marekani ameliomba jopo la majaji linalosikiliza kesi ya mauaji inayomkabili mume wake, kutomwekea hukumu ya kifo.

Mama huyo aliyefahamika kwa jina la Amber Kyzer, alimtetea mume wake kutohukumiwa kifo, baada ya kukutwa na hatia ya kuua watoto wake watano.

Kyzer aliiambia mahakama moja huko Carolina ya kusini, nchini Marekani kwamba mumewe (Tim Jones Jr) hakuwaonea huruma watoto wake wakati akitekeleza mauaji hayo licha ya watoto kumpenda.

Tim Jones Jr mwenye umri wa miaka 37 alikutwa na hatia kwa kosa la kuwauwa watoto wake watano wenye umri kati ya mwaka mmoja hadi nane nyumbani kwake karibu na Lexington Agosti 29, 2014.

Hata hivyo, jopo la majaji bado linajadiliana iwapo Jones anastahiri kupewa kifungo cha maisha ama kunyongwa.

Kyzer aliliambia jopo hilo kwamba amekuwa akipinga hukumu ya kifo kwa kipindi chote cha maisha yake.

Alisema licha ya kutamani sheria imuhukumu mumewe lakini hatapenda kumchangulia hukumu ya kifo.

''Hakuwaonyesha watoto wangu huruma yoyote, Lakini watoto wangu walimpenda na iwapo ninazungumza kwa niaba yangu na watoto wangu basi hilo ndio tamko langu," alisema Kyzer.

Kyzer alisema kwamba ataheshimu chochote kitakachotolewa na jopo hilo la majaji.

Wanandoa hao walifunga ndoa wiki sita baada ya kukutana mwaka 2004 wakati walipokuwa wakifanya kazi katika bustani ya watoto ya kucheza katika eneo la Chicago.

Kyzer alitoa ushahidi Mei, mwaka huu kwamba ndoa yao ilikuwa imekumbwa na matatizo kwa kuwa alikuwa anapewa masharti mengi.

Wawili hao walipotengana baada ya miaka tisa alimpatia watoto aishi nao kwa sababu alikuwa akifanya kazi iliokuwa ikimpatia pato la dola za Marekani 80,000 kwa mwaka, ambapo Kyzer alikuwa akiwaona watoto wake kila Jumamosi katika mgahawa mmoja.

Akisimulia mkasa wa kuuawa kwa watoto wake, Kyzer alisema Jones alikasirika alipomuona mtoto mwenye wake mwenye umri wa miaka sita, Nahtan akichezea umeme nyumbani.

Alisema amuua mtoto huyo na baadaye kuwanyonga watoto wengine wanne-Elaine, Gabriel, Elias na Mera.

"Jones baadaye aliifunga miili yao katika mfuko wa plastiki, na kuiweka ndani ya gari moja na kuondoka kwa siku tisa kabla ya kuacha mabaki hayo katika jimbo la Alabama," alisema Kyzer.

Jones alikamatwa katika kituo kimoja cha trafiki mjini Missisipi wakati maofisa wa polisi walipotambua harufu iliokuwa ikitoka ndani ya gari hilo.

Hata hivyo, Jones alikana kuhusika na mauaji ya watoto hao alipofikishwa mahakamani.

*BBC*



Mfanyakazi wa Wizara ya Afya nchini Uganda, akimpima joto mwanamke aliyekuwa anaingia nchini humo akitokea Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) ikiwa ni sehemu ya kudhibiti kusambaa kwa ugonjwa huo. **PICHA: AP**

# Mtoto aliyeambukizwa Ebola Uganda afariki

**KAMPALA, Uganda**

WIZARA ya Afya nchini Uganda imesema mtoto ambaye aliripotiwa kuwa na virusi vya ugonjwa wa Ebola nchini Uganda amefariki dunia.

Wizara ya Afya imetoa taarifa hiyo wakati wazazi wake wakiwa wamethibitishwa kuwa na virusi vya ugonjwa huo kutoka nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC).

Shirika la Afya Duniani (WHO) limethibitisha kupitia ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Twitter ikieleza kuwa nchi ya Uganda imerekodi kesi tatu za Ebola, ikiwa ni maambukizi ya kwanza kuripotiwa nchini Uganda tangu ugonjwa huo uripotiwe nchini DRC.

Wizara ya Afya ya Uganda jana ilisema kuwa mwanamke mmoja mwenye asili ya DRC ambaye ameolewa na raia wa Uganda, walikuwa wameenda na mtoto wao pamoja na wanafamilia wengine wanne nchini DRC kumuhudumia baba yao ambaye baadae alifariki kutokana na Ebola.

Katika taarifa yake kupitia WHO imeeleza kuwa mtu aliyegundulika kuwa na virusi hivyo ni mtoto wa miaka mitano ambaye alikuwa anasafiri akitoka DRC na wazazi wake Juni 9 mwaka huu.

Imesema mtoto huyo na familia yake waliingia nchini Uganda kupitia mpaka wa Bwera ambapo baada ya kuingia waliomba kupata matibabu kwenye kituo cha afya na kuchukuliwa sampuli ya damu.

Wizara ya Afya ya Uganda imethibitisha kuwapo kwa mgonjwa huyo ambapo imesema baada ya mtoto huyo kuchukuliwa sampuli ya damu, ilibainika kuwa na maambukizi ya virusi vya Ebola.

Tayari wizara ya afya nchini humo na WHO wametuma wataalamu wake kwenda kusaidia wataalamu walioko eneo la magharibi mwa Uganda kuwatibu na kutoa chanjo ya majaribio inayoendelea kutolewa pia mashariki mwa DRC.

Nchi ya Uganda imekuwa kwenye hali ya tahadhari tangu kuripotiwa kwa mlipuko wa virusi vya Ebola mashariki mwa DRC, ambako watu zaidi ya 1,300 wameripotiwa kupoteza maisha.

*RFI*

# Polisi yanasa wanaodaiwa kupora bastola ya wakili

**Na Romana Mallya**

WACHIMBAJI madini wawili wakazi wa Mirerani, jijini Arusha, Mwaluka Jumanne (24) na Ali Hatibu (34), wanashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani humo kwa kwa tuhuma za kukutwa wamejificha nyumba ya kulala wageni baada ya kumwibia bastola wakili wa kujitegemea.

Kamanda wa Polisi mkoani humo, Jonathan Shana, aliliambia Nipashe jana kuwa watuhumiwa hao wawili walikutwa Jumatatu kwenye nyumba ya kulala wageni Songambele iliyopo mji mdogo Mirerani wakiwa wamejificha baada ya tukio hilo la wizi. Akisimulia kuhusu tukio hilo, Kamanda Shana alisema Mei 19 mwaka huu, walipokea taarifa kutoka kwa Wakili wa Kujitegemea Dancan Pola (52) mkazi wa JR Mbauda kuwa ameibiwa bastola yake aina ya Brown nyumbani kwake.

"Baada ya kupokea taarifa hii, kikosi kazi kiliingia kazini kupitia taarifa za kiintelijensia na kufanya operesheni na kuwakamata watuhumiwa hao waliokuwa wamejificha nyumba ya wageni wakiwa na bastola hiyo," alisema.

Kamanda Shana alisema watuhumiwa hao ambao wanaendelea kushikiliwa na kuhojiwa ili kubaini mtandano wa kihalifu.

"Watu hawa wamewataja washirika wao na upelelezi ukikamilika watafikishwa mahakamani, Jeshi la Polisi linawataka washiriki wote waliotajwa na hawa, wajisalimishe polisi wenyewe," alisema.



Sehemu ya wanachama wapya 886 wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wa Kata ya Naberera, mkoani Manyara, waliohama Chadema na kumfuata Mbunge wa Jimbo la Simanjiro, James Ole Millya (kushoto), wakila kiapo cha uhaminifu juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mbinu mpya ya majangili yatajwa

**Na Salome Kitomari**

UJANGILI wa nyumbu, pundamilia, twiga na kakakuona unashamiri nchini, baada ya udhibiti wa biashara ya meno ya tembo na pembe ya faru.

Akizungumza jana na waandishi wa habari katika mahojiano maalum, Mkurugenzi Msaidizi wa Kuzuia Ujangili, Robert Mande, alisema ujangili huo unashamiri kwa kasi kwa watu kusafirisha nyama nje ya nchi.

Alisema ujangili wa wanyamapori umeongezeka maeneo ya mpakani mwa Serengeti na Kenya kwa majangili wanafadhiliwa na watu wenye fedha ambao ndiyo wanunuzi.

"Watu wameelekea kwenye uhalifu wa kuua wanyama kwa ajili ya kitoweo cha biashara, wanajua ukiua tembo utakamatwa wakakimbilia uhalifu mwingine," alisema. Alisema katika eneo la Mugumu na Bunda Serengeti majangili huwavizia wanyama nyumbu wakati wa kuhama kutoka Hifadhi ya Serengeti kwenda Masai, Mara nchini Kenya kwa kutegesha nyaya.

"Kwa sababu wanahama kwa wingi mtu anaenda ndani ya pori anaweka kambi mwezi mzima anatega wanyama kwa kutumia nyaya, anatega mitego zaidi ya 100 alafu wanaua wanyama hadi 1,000 alafu nyama zinasafirishwa kwenda nje ya nchi," alisema.

Mande ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kikosi kazi cha Taifa cha Kuzuia Ujangili, alisema walibaini kuna watu wanawapa fedha nyingi, nyaya na vifaa vingine ili waweze kukusanya nyama kwa wingi.

"Hii ni biashara haramu ya wanyamapori, wanakamata nyumbu wanaohama kwa wingi, mtu akiweka nyaya 500 anakamata nyumbu 200, nyama yake inakaushwa inaitwa vimolo na kusafirishwa tani kwa tani kwenda Kenya ambako kuna soko," alisema.

Alisema maeneo mengine yenye ujangili huo ni Selous na wanyama wanaokamatwa zaidi ni nyumbu, nyati na pundamilia ndiyo wanyama wanaolengwa na huu ujangili mpya.

Aidha, alisema mkoani Arusha kuna ujangili wa twiga na kwamba majangili huangalia thamani na ukubwa wa mnyama kabla ya kumuua.

Mkurugenzi huyo alisema ni rahisi mtu kushawishiwa na kuingia kwenye uhalifu bila kujulikana kutokana na nafasi yake serikalini au kwenye taasisi.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, mwaka juzi walikamata mtandao wa watu kutoka Tanzania, Uganda, Guinea na Rwanda wakiwa na tani sita za magamba ya kakakuona ambazo zilikusanywa sehemu mbalimbali.

"Kumekuwa na biashara kubwa sana ya magamba ya kakakuona. Mwaka jana walikamata watu maeneo ya Kondoa, Dodoma, si biashara ya Tanzania pekee bali duniani, kwa nchini watu wanne walikamatwa na kesi zinaendelea mahakamani," alibainisha.

Katika kukabiliana na jambo hilo, Mande alisema wameunda vikosi kazi 10 nchi nzima ambavyo ni kwenye kanda zote, na kuanzisha kikosi maalum chenye vyombo vyote za ulinzi na usalama kwa kushirikiana na taasisi za wanyamapori chini ya uratibu wa kikosi kazi taifa.

"Kwa msukumo tunaoupata kwa Rais John Magufuli juu ya kupambana na ujangili tunaona matunda, sheria namba 3 ya kulinda rasilimali za nchi na kuhakikisha wananchi wananufaika imetoa uwanja mpana wa kulinda mali za taifa," alifafanua.

"Baada ya kudhibiti ujangili wa Tembo na Faru sasa wamehamia kwenye kakakuona, na mbaya zaidi hatuna idadi yao na tunatakiwa kuchukua hatua ikiwamo kujua takwimu zao," alisema.

# Mpango kuvuna watalii wa China

**Na Beatrice Moses**

BODI ya Tanzania (TTB) imejipanga kufanya ziara ya utangazaji wa utalii China ikiwa ni hatua ya kuhakikisha inavuna watalii kutoka nchini humo, hivyo kujiimarisha katika soko la utalii.

Mwenyekiti wa Bodi ya TTB, Jaji Mstaafu Thomas Mihayo, ameyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, ambapo alibainisha kuwa kiongozi wa msafara atakuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Aloyce Nzuki.

Alisema ziara hiyo ya wiki moja inaanza Juni 19 hadi 26 katika miji minne ya China ambayo ni Beijing, Shangha, Nanjig, Changsha, lengo likiwa ni kuhakikisha Tanzania inaongeza sehemu ya umiliki wa soko kwenye soko la utalii China.

" Kwa kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo, fursa za uwekezaji na safari mpya za ndege za ATCL kwenda China," alisema.

Alisema katika ziara hiyo TTB itaambatana na wadau mbalimbali kutoka sekta binafsi na ya umma ikiwamo TANAPA, NCAA, Wakala wa Huduma za Misitu, Makumbusho ya Taifa Idara ya Mambo ya Kale Mamlaka ya Usimamizi wa wanyamapori na Wizara ya Maliasili na Utalii.

Jaji Mihayo alisema Shirika la Utalii Dunia (UNWTO) na vyanzo vingine mbalimbali duniani vimebainisha kuwa soko la watalii kutoka China linaendelea kuongoza kwa kuwa na idadi kubwa zaidi ya watalii na mchango katika uchumi wa dunia.

"Kwa sababu hii TTB na wadau tuliona fursa kubwa ya kuongeza jitihada za kuwavutia watalii zaidi kutika katika nchi hiyo, mwezi Novemba 2018 iliratibu ziara kubwa ya kutangaza vivutio vya utalii vya Tanzania," alisema Jaji Mihayo.

**" Kwa kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo, fursa za uwekezaji na safari mpya za ndege za ATCL kwenda China," alisema.**

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### MAGARI NA VIPURI

**CRANE FUSO FOR SALE,**

(1.) Fighter 2002, SAKAI_340,3 stages, New in TZ,
2. Magnum 1991, TADANO_290, 2 Stages, 3 years in TZ.


**"Dalali Hatakiwi" Simu 0692 469 669**

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz ,au piga simu: 0767 223311


### CHETI KIMEPOTEA



115271002

**ELIZABETH ONYANGO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0333-0223** kilichotolewa na MWANZA SEKONDARI mwaka 1997. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/STA/57566/2019.**


### CHETI KIMEPOTEA



115270802

**NSAJIGWA MWAKALIKAMO MPOKI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1407-0074** kilichotolewa na ARCH BISHOP KAHURANANGA SEKONDARI mwaka 2011. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **SI/B.I/27/VOL.IX/296.**

### CHETI KIMEPOTEA



115270902

**GEOFREY SALAMBA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0717/0029** kilichotolewa na LAELA SEKONDARI mwaka 1999. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **SU/RB/1247/2005.**

### KUPOTEA KWA CHETI



215269802

**Pendo Katutu** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato nne chenye index namba **S0404-027** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1993 katika shule ya sekondari Tunduru .Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **TUK/RB/2283/2008**

### CHETI KIMEPOTEA



215270302

**ANSELMINA REGNARD MAHUYI** anatangaza kupotelewa na cheti cha KIDATO CHA NNE chenye no **P0377-0008** kilichotolewa na NECTA TANZANIA mwaka 1998 Shule ya Lugalo High school. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/56866/2019**

### GOROFA INAUZWA



**BOKO KAMWANGA STR LOW DENSITY AREA BLOC "C", PLOT NO. 65**

**SIMU**: 0754 226 687 / 0756 410 345.

115258902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA MOROGORO.**

**MAOMBI NA.57 YA MWAKA 2019.**

**NURU RASHIDI...............MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**PAULO EDWARD.............MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA PAULO EDWARD............MJIBU MAOMBI**

Popote Ulipo Unaarifiwa Ufike ktk baraza la ardhi na Nyumba la wilaya ya Morogoro tarehe 19/06/2019 mwenyewe binafsi au mwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa.Endapo hautaudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.

Imetolewa kwa mkono wangu leo tarehe 11 Mwezi June,2019.

215270402

### KUPOTEA KWA KADI

**Tenta Trading Limited** anatangaza kupote kwa kadi ya gari yenye usajili wa namba **T528 CUW**, aina ya MITSUBISH PAJERO iliyotolewa na TRA. Taarifa imetolewa kituo cha Polisi kwa Kumb. Na. **MS/RB/4822/2019**

115270502

### TANGAZO LA KUPOTEA KWA OFA YA KIWANJA

**COLEETA GIGWA MKAZI WA NDALA MANISPAA YA SHINYANGA**

ANATANGAZA KUPOTELEWA NA OFA YAKE YA KIWANJA NAMBA 205 BLOK HD NDALA AMBAYO ILIPOTEA TANGU MWAKA 2017 MAENEO YA SHINYANGA

KWA YEYOTE ATAKAE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU AU AWASILIANE NA COLEETA GINGWA KWA SIMU NAMBA **0752883903. RB NAMBA SHY/RB 3455/2019**

215270202

### KUPOTEA KWA KADI

**Riziwani Adamu Kijazi** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye usajili wa namba **T243 DCA** aina ya **TOYOTA HILUX,** yenye chasis namba **JTFD56262000036473.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DAR/OST/RB/538/2019**

115270602

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA

### TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **ALHAMIS** tarehe 13/06/2019 kampuni ya **DOW ELEF INTERNATIONAL TANZANIA LIMITED** itasafirisha Mizigo yake yenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM** kuelekea MTWARA kupitia **NANGURUKURU,** gari hizo zenye namba za usajili zenye vipimo vyake:

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | T 164 DNL/ T 653 CAE | UREFU 19.0 | UPANA 3.5 | KIMO 5.0 |
| 2. | T 181 DNL/ T 865 DKM | UREFU 19.0 | UPANA 3.5 | KIMO 5.0 |
| 3. | T 505 DNJ / T 863 DKM | UREFU 19.0 | UPANA 3.5 | KIMO 5.0 |
| 4. | T 167 DNL / T 403 BLW | UREFU 19.0 | UPANA 2.88 | KIMO 5.0 |

2. Gari hizo zinatoka **DAR ES SALAAM** kuelekea **MTWARA** kupitia **NANGURUKURU.** ***Gari zitasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni).***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

115271402

**Uza, Chenye Thamani Kubwa**

**Kwa Kutangaza**

**Nasi Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0767 223 311**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# GIGGS AKIRI BALE AMEPOROMOKA

**Budapest, Hungary**

RYAN Giggs amekiri kwamba amekutana na wakati mgumu wa utimamu wa kimwili wakati akijaribu kupata nafasi nzuri kiufanisi kwa Gareth Bale katika kikosi cha Wales baada ya kumtazama mshambuliaji huyo wa Real Madrid akihaha wakati wakichezea kichapo cha bao 1-0 kwenye mechi ya kuwania kufuzu michuano ya Euro 2020 dhidi ya Hungary.

Bale alikosa nafasi muhimu kwa Wales katika mechi hiyo, kwa kushindwa kuzamisha mpira wavuni mwa kipa wa Hungary, Peter Gulacsi wakati mpira ulipotua miguuni mwake akiwa umbali wa maguu 12 ya mtu mzima kutoka golini, na kisha Mate Patkai akawaadhibu kwa uzembe wao wa kushindwa kuziona nyavu mapema baada ya kuifungia timu yake bao la ushindi zikiwa zimebaki dakika 10 mechi kumalizika.

Baada ya kuamua kumchezesha Dan James kama mshambuliaji wa kati wakati Bale akianzishwa winga ya kushoto, Giggs alisema maadili ya mshambuliaji huyo si tatizo wakati wa mazoezi licha ya kupitia wakati mgumu msimu huu akiwa La Liga.


"Amekatishwa tamaa kama sisi sote kwa michezo miwili," Giggs aliwaambia wanahabari wakati alipoulizwa kuhusu Bale.


"Nilishasema kabla, katika kambi ya mazoezi alikuwa mzuri, kuhusu nafasi amekuwa mzuri. Shida ni kuwa fiti vizuri kwa kutocheza muda mrefu.

"Namna alivyocheza pia, wale walio na kiwango cha juu. Ni vigumu. Lakini amekuwa mzuri karibu na nafasi, hakuna tatizo.

"Daima ni kitendo kidogo cha ujuzi kimwili kujaribu kutafuta sehemu ambayo Gareth anaweza kuwa na ufanisi. Tuna wachezaji wengi ambao wanaweza kucheza kulia ama namba 10.

"Gareth ameonyesha zaidi ya miaka michache anaweza kucheza mbele, namba 10, pembeni kulia. Ni kazi yangu kujaribu na kupata nafasi sahihi na kupata wachezaji wengine katika nafasi nzuri pia."





# MADRID
## WAANZISHA MCHAKATO WA POGBA

**MADRID,Hispania**

KLABU ya Real Madrid sasa imeamua kuanzisha mazungumzo rasmi na Manchester United kwa ajili ya kumsajili kiungo wake mshambuliaji, Paul Pogba.

Imeelezwa, maofisa wa Real Madrid walikutana na wale wa Man United mapema mwishoni mwa wiki kwa ajili ya kuangalia uwezekano wa kumsajili Pogba.

Maofisa hao walikutana jijini London wakati wakiwa kwenye harakati za kukamilisha uhamisho wa nyota wa Chelsea, Eden Hazard ambaye wamekwishamtangaza kuwa ni mchezaji wao.

Hata hivyo, United inataka faida huku ikitaka kumuuza kiungo huyo wa kimataifa wa Ufaransa kwa dau la pauni milioni 150, wakati wao walikuwa wamemsajili kwa pauni milioni 89.

Kocha wa Real Madrid, Zinedine Zidane anamtaka Pogba ambaye ni Mfaransa mwenzake na Machi mwaka huu aliweka wazi kwamba anavutiwa na kiwango cha Pogba huku mwenyewe akikiri ndoto yake ni kucheza Real Madrid siku moja.

Uwezekano wa Pogba kukipiga Madrid umezidi kuonekana kutokana na kudorora kwa uhusiano na kocha wake wa sasa, Ole Gunnar Solskjaer baada ya awali kutokuwa na uhusiano mzuri na kocha aliyepita, Jose Mourinho.

Pogba pia alikwaruzana na mashabiki wa United katika pambano la mwisho la msimu dhidi ya Cardiff City paled Old Trafford baada ya United kuchapwa mabao 2-0 na mashabiki walimwambia Kocha Solskjaer amuuze kama kuna uwezekano huo.

# Solskjaer amfungia kazi Wan-Bissaka



**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, ameongeza nguvu kwenye kuiwania saini ya beki wa kulia Aaron Wan-Bissaka wa Klabu ya Crystal Palace.

Licha ya beki huyo wa kulia kuwekwa sokoni kwa pauni milioni 50, kocha huyo amepania kumsajili katika kipindi hiki cha majira ya joto.

Awali klabu ya Palace ilikataa ofa ya pauni milioni 40 iliyowekwa mezani na Man United.

Solskjaer ana kiu ya kufanya kazi na Wan-Bissaka baada ya kucheza kwa kiwango bora katika mashindano ya msimu uliopita.

Kocha huyo anataka beki wa kulia kuziba pengo la wachezaji wakongwe akiwamo nahodha Antonio Valencia na Ashley Young. Kinda huyo wa timu ya Taifa ya vijana ya England chini ya miaka 21, amekuwa na msimu mzuri Palace.

## HABARI MICHEZO

# LAMPARD
## AJIPA MATUMAINI KUELEKEA KUINOA CHELSEA

**LONDON, England**

FRANK Lampard anajiamini kwamba anaweza kupata nafasi ya kuwa kocha wa Chelsea kipindi hiki cha majira ya joto, wakati Maurizio Sarri akiwa njiani kuondoka hapo Stamford Bridge.

Lampard alianza kazi ya ukocha msimu uliopita kwa timu ya daraja la chini ya Derby County baada ya kumaliza kipindi chake cha kucheza Chelsea, ambako alicheza mechi 400 katika kipindi cha miaka 13.

Lampard mwenye umri wa miaka 40 ambaye aliiongoza Derby kwenye mchezo wa mwisho wa mchujo 'play-off' kuwania kufuzu Ligi Kuu, aliikosa nafasi hiyo baada ya kufungwa na Aston Villa mabao 2-1 katika dimba la Wembley.

Goal.com imeripoti kwamba, Lampard alikutana na maofisa wa Chelsea Jumanne kwa ajili ya kujadiliana uwezekano wa kupewa nafasi hiyo.

Kama mpango huo utakamilika, atachukua nafasi ya Sarri, ambaye anakwenda kujiunga na Juventus baada ya kufukuzwa kwa Massimiliano Allegri.

Uwezekano wa Sarri kuondoka ni mkubwa na sasa Chelsea imekuwa katika mchakato wa kutafuta mrithi wake na Lampard ndiye anaonekana kama mtu anayeweza kuchukua nafasi hiyo.

Pia, Rafael Benitez amekuwa akitajwa kupewa nafasi hiyo baada ya kukaa pale Newcastle na kuibakiza kwenye Ligi Kuu ya England.





# MBAPPE
## AFUNGA BAO LA 100 TAIFA UFARANSA

**PARIS, Ufaransa**

UFARANSA ilipata ushindi wa mabao 4-0 ugenini dhidi ya Andorra Jumanne na kurudi kileleni mwa Kundi H katika michuano ya kuwania kufuzu kwa Euro 2020, huku mchezaji wake, Kylian Mbappe akifikisha mabao 100 kwa kikosi hicho.

Mbappe mshindi wa Kombe la Dunia alifunga bao katika dakika ya 11 na kumfanya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 kufikisha mabao 100 katika kipindi chake cha kuichezea nchi hiyo.

Wissam Ben Yedder na Florian Thauvin nao walifunga kwenye ushindi huo, huki beki Kurt Zouma akifunga bao la nne.

Mbappe kwa umri wake sasa anaweza kufikisha mabao mengi zaidi kwa kuifungia Ufaransa na huenda akaifikia rekodi iliyowekwa na Thierry Henry.

Ufaransa iliingia kwenye mchezo huo, ikitokea kwenye maumivu ya kufungwa mabao 2-0 na Uturuki katika michuano hiyo.

Ushindi huo sasa umeiweka Ufaransa kileleni mwa msimamo wakitofautiana mabao na Uturuki.

# Barca kuingiza euro mil. 60 kabla ya Juni 30

**BARCELONA, Hispania**

KLABU ya Barcelona ina matumaini ya kuingiza kiasi cha euro milioni 60 kabla ya Juni 30, mwaka huu kwa ajili ya kukiimarisha kikosi chake kwa msimu ujao, kwa mujibu wa ESPN FC.

Kocha Ernesto Valverde angependa kuongeza wachezaji watatu au wanne kwenye kikosi chake kipindi cha majira ya joto, lakini alionywa kwamba anatakiwa kuingiza fedha kwa kuuza kwanza wachezaji.

Kwa mujibu wa ESPN FC baada ya mabingwa hao wa Hispania kufungwa na Liverpool hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, wanapanga kumuuza mchezaji waliyemsajili kwa ada iliyoweka rekodi, Philippe Coutinho.

Barca inapanga kumuuza mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil kwa kiasi cha euro milioni 100.

Ivan Rakitic na Samuel Umtiti pia wanatajwa kwamba watauzwa na kwa ujumla wake kiasi chao kinatajwa kuwa ni euro milioni 300, ingawa wote wawili wameonyesha nia ya kutaka kubakia klabuni hapo.

Lakini chanzo kingine kimeliambia ESPN FC kwamba, klabu hiyo inataka kukiboresha zaidi kikosi hicho kwa kuhakikisha kinawauza wachezaji ambao hawakuwa na msimu bora mwishoni mwa mwezi huu.

Miamba hao wa Hispania tayari wameshakubali kulipa ada ya awali ya euro milioni 75 kwa ajili ya kiungo wa Ajax, Frenkie de Jong.

Pia, wanataka kumsajili Antoine Griezmann ambaye aliwaambia Atletico Madrid mpango wake wa kuondoka mwishoni mwa msimu huu na ada yake ni euro milioni 120, huku pia wakiwa kwenye harakati za kumsajili Matthijs de Ligt wa Ajax.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI AONGOZA KWA KULIPWA ZAIDI DUNIANI

**NEW YORK, Marekani**

MSHAMBULIAJI wa Barcelona na timu ya Taifa ya Argentina, Lionel Messi, ndiye mwanamichezo anayelipwa malipo ya juu zaidi kuliko wachezaji wote duniani, akiwa analipwa dola milioni 127 katika kipindi cha miezi 12 iliyopita, kwa mujibu wa orodha ya Jarida la Forbes ya wachezaji 100 wanaolipwa vizuri.

Mshambuliaji wa Juventus, Mreno Cristiano Ronaldo anashikilia nafasi ya pili akilipwa dola milioni 109, huku mshambuliaji wa Paris St-Germain, Neymar ambaye ni raia wa Brazil akiwa katika nafasi ya tatu kwa malipo ya dola milioni 105.

Mwaka jana mwanamichezo aliyekuwa akilipwa kuliko wote duniani alikuwa ni mwanamasumbwi, Floyd Mayweather, lakini sasa ameshuka katika orodha hiyo.

Mchezaji tenesi, Serena Williams ni mwanamke pekee katika watu 100, wanaolipwa vizuri na kwa mujibu wa Forbes analipwa dola milioni 29.2.

Mshindi mara tano wa mashindano ya dunia ya magari ya Formula 1, Lewis Hamilton na mshindi wa zamani wa masumbwi uzani wa juu, Anthony Joshua ndio wanariadha wanaolipwa vizuri zaidi nchini Uingereza , wakichukua namba 13 na malipo ya dola milioni 55.

Jarida hilo la Marekani lilikokotoa malipo ya wanariadha kwa kujumlisha fedha za malipo ya tuzo, mishahara na nembo walizoidhinisha kati ya Juni 2018 na Juni 2019.

Messi ndiye mchezaji pekee wa pili wa soka kuwa juu katika viwango baada ya Ronaldo na ndiye mwanamichezo wa nane pekee miongoni mwa wachezaji soka tofauti kuchukua namba moja tangu orodha hiyo ilipoanza kutolewa mnamo mwaka 1990.

Ni mara ya kwanza kwa mchezaji wa mpira wa miguu kuwekwa miongoni mwa watu watatu wanaolipwa vizuri kwa kucheza.

Messi ni miongoni mwa wanamichezo 38 wasio raia wa Marekani kwenye orodha hiyo, huku wanamichezo nyota 62 wa Marekani wakishikilia nafasi za kwanza katika orodha ya watu 100.

Shirikisho la Mchezo wa Kikapu la Marekani (NBA), ndilo lililoongoza kwa kuwa na wachezaji wengi kwenye orodha hiyo, likiwa na wachezaji 35, huku LeBron James wa LA Lakers akiwa ndiye mchezaji anayelipwa zaidi ambapo anashikilia nafasi ya nane akilipwa dola milioni 89.

**Orodha ya 10 bora:**
1. Lionel Messi - Dola mil. 127
2. Cristiano Ronaldo - Dola mil. 109
3. Neymar- Dola mil. 105
4. Canelo Alvarez- Dola mil. 94
5. Roger Federer- Dola mil. 93.4
6. Russell Wilson- Dola mil. 89.5
7. Aaron Rodgers- Dola mil. 89.3
8. LeBron James- Dola mil. 89
9. Stephen Curry- Dola mil. 79.8
10, Kevin Durant- Dola mil. 65.4

## KWA UFUPI

**UBINGWA UEFA KUMSTAAFISHA GUARDIOLA**
KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, atafikiria kupumzika kazi ya ukocha mwishoni mwa msimu ujao kama atatwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Star)***

**RAKITIC APIGIWA HESABU UNITED**
MANCHESTER United imefanya mawasiliano na Barcelona kuhusu uwezekano wa kumsajili kiungo Mcroatia Ivan Rakitic, 31. ***(Sport - in Spanish)***

**CHAMBERLAIN KUJIFUNGA TENA LIVER**
KIUNGO Muingereza, Alex Oxlade-Chamberlain, 25, anajiandaa kuongeza mkataba wake wa sasa hapo Liverpool hadi mwaka 2023. ***(Mail)***

**FELIX AITAKA ATLETICO MADRID**
MSHAMBULIAJI wa Benfica, Mreno Joao Felix, 19, anavutiwa na kujiunga na Atletico Madrid. ***(AS - in Spanish)***

**MAGUIRE, BISSAKA KUWEKA REKODI UTD**
MANCHESTER United itapaswa kuvunja rekodi yake ya usajili wa mabeki mara mbili kama itafanikiwa kuwasajili Aaron Wan-Bissaka, 21, kutoka Crystal Palace na Harry Maguire, 26, kutoka Leicester kwa ada ya jumla ya pauni milioni 130. ***(Standard)***

**DE LIGT KUAMUA AKIWA LIKIZO**
BEKI wa Ajax, Mholanzi Matthijs de Ligt, 19, anasema "hajui nini moyo wangu unasema" lakini ataamua mustakabali wake wa baadaye wakati akiwa likizo. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

**CHELSEA YAMTAFUTIA SARRI MBADALA**
CHELSEA inataka mbadala wa kocha wa sasa Maurizio Sarri kuwa tayari kabla ya Mtaliano huyo kuthibitisha kuondoka Juventus baadaye wiki hii. ***(Mirror)***

**ARSENAL YATUA KWA PELLEGRINI**
ARSENAL inavutiwa na kumsajili kiungo wa Roma, Mtaliano Lorenzo Pellegrini, 22, ambaye anaruhusiwa kuununua mkataba wake kwa pauni milioni 27, lakini inakabiliwa na ushindani kutoka Tottenham, AC Milan na Inter Milan. ***(Mirror)***

**BUFFON KUMRITHI CASILLAS PORTO**
KIPA wa zamani wa Italia Gianluigi Buffon, 41, anaweza kujiunga na Porto baada ya kuondoka Paris St-Germain, ili kuziba pengo la Mhispania Iker Casillas, 38. ***(Tuttosport - in Italian)***

**LAMPARD, CHELSEA WATETA**
CHELSEA imefungua meza ya mazungumzo na kocha wa Derby, Frank Lampard kuhusu kiungo wao huyo wa zamani kurejea Stamford Bridge kuinoa. ***(Mail)***

**POGBA APANIWA KUTUA MADRID**
REAL Madrid itafanya kila liwezekanalo kumsajili kiungo wa Manchester United, Mfaransa Paul Pogba, 26, kwa kuwa ni chaguo la kwanza la Zinedine Zidane. ***(Marca)***

**HUDSON-ODOI ATOA MASHARTI**
WINGA wa Chelsea, Callum Hudson-Odoi, 18, anataka kuhakikishiwa kuwa sehemu ya kikosi cha kwanza kabla ya kusaini mkataba mpya na klabu hiyo. Nyota huyo wa kimataifa wa England amebakiza mwaka mmoja katika mkataba wake wa sasa na klabu hiyo. ***(Sun)***

**BARCA KUINGIZA EURO MILIONI 60**
BARCELONA inatumai kuingiza takriban euro milioni 60 kwa kuwauza wachezaji wake kabla ya Juni 30, lengo likiwa ni kutafuta uwiano mzuri wa akaunti yake kwa msimu wa 2018-19. ***(ESPN)***



# MWAMEJA AMFUNDA MANULA AFCON 2019

**Na Somoe Ng'itu**

KIPA chaguo la kwanza wa zamani wa timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Mohammed Mwameja, amemtaka golikipa wa timu hiyo, Aishi Manula, kuongeza umakini kwenye fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019 ili waweze kufanya vema katika mashindano hayo.

Mwameja, alisema hayo jana muda mfupi baada ya uzinduzi wa jezi mpya za Taifa Stars ambazo zitaanza kuvaliwa katika mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Misri itakayochezwa leo mjini Alexandria.

Kipa huyo alisema golikipa ndiye nguzo ya timu na kazi yake kubwa ni kurekebisha makosa ambayo yamefanywa na wachezaji wenzake katika kila mchezo.

Alisema anaamini Manula akiongeza utulivu, anaweza kuisaidia sana timu hiyo ambayo ilikuwa haijashiriki fainali hizo kwa miaka 39.

"Ushauri wangu kwa Manula ni kuwa anatakiwa kuongeza umakini, utulivu na kucheza kwa kiwango cha juu, yeye ndiye nguzo na mhimili muhimu wa timu, ninamwamini na nchi pia imemwamini, tunawatakia kila la kheri," alisema Mwameja.

Kipa huyo wa zamani wa Simba aliwataka wachezaji wote walioko katika timu hiyo kuongeza bidii na kuhakikisha wanapeperusha vema bendera ya Tanzania katika mashindano hayo.

"Wanatakiwa kupambana na kujivunia kuwa kwenye kikosi hicho, ni historia, wafahamu wanatakiwa waweke rekodi nzuri ya ushiriki wao, tupo nyuma yao katika maombi, tunaamini watatuwakilisha vizuri," Mwameja alisema.

Naye Keneth Mkapa, nyota wa zamani wa Yanga na Stars, alisema kikosi hicho kinatakiwa kuendeleza pale walipoishia katika mechi za kusaka tiketi za kushiriki fainali hizo.

"Moto na kasi waliyoionyesha katika mechi ya mwisho, inatakiwa iendelee, wakifanya hivyo, tutapata matokeo ya kufurahisha huko Misri," alisema Mkapa.

Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), jana liliwakabidhi jezi mpya kila mchezaji wa zamani aliyefika katika uzinduzi huo ambao ulihudhuriwa pia na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda.




Msanii wa muziki wa Kizazi Kipya, Khalid Ramadhani maarufu kama Tunda Man (kushoto), akikabidhiwa mfano wa hundi ya Sh. milioni 40.5 na Meneja Uhusiano wa Kampuni ya SportPesa, Sabrina Msuya, kufuatia kupatia kwa usahihi ubashiri wa mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot ya wiki iliyopita. **PICHA: SPORTPESA**

# Tunda Man mkali wa kubeti, ashinda mil. 40/- SportPesa

**Na Mwandishi Wetu**

MWANAMUZIKI nguli wa Bongo Flava, Khalid Ramadhani maarufu kama 'Tunda Man' ameonyesha kwamba si mkali tu katika kutunga na kuimba mashairi, bali pia anatisha pindi anapotulia na kuchanga karata zake katika kubashiri matokeo ya mechi.

Tunda Man amethibitisha umakini huo baada ya kupatia mechi 12 kati ya 13 katika Jackpot ya SportPesa hivyo kujinyakulia bonasi ya Sh. milioni 40.5 katika ubashiri wa wiki iliyopita.

Staa huyo anayefahamika kwa vibao vyake maarufu kama vile 'Mwanamke gani na Bosi hanuniwi' amejinyakulia kitita hicho ambacho kinazidi kuongezeka kila wiki wakati huu thamani ya Jackpot ikiwa ni Sh milioni 6.98.

Tunda Man ambaye ni mkongwe wa muziki nchini, ameweka wazi kuwa ameshawishika kuanza kubashiri baada ya kuona washikaji zake wakishinda.

"Mwanzo nilikuwa naona watu tu wanacheza wakawa wananiuliza hadi mimi nikawa nawajibia tu wao wanapata hela.

"Ikafika kipindi nikaona kwa nini na mimi nisipate hela, kwa hiyo ndio nikaanza kucheza na nikawa nashinda kidogo kidogo ila kibunda cha leo ndio kimekuwa cha maana hivi," alisema Tunda Man.

Akizungumza katika makao makuu ya SportPesa muda mfupi kabla ya kukabidhiwa hundi ya kitita chake, Tunda Man ambaye anafanya muziki chini ya lebo maarufu ya 'Tip Top Connection', ameelezea sababu zinazomfanya apendelee kubeti kupitia SportPesa nyingi na za kuvutia.

"Sportpesa wana 'option' nyingi sana yaani mpaka kadi, kona kuliko kampuni nyingine na kingine unaweza kubet hata mechi moja," alisema.

Tofauti na watu wanavyoweza kudhani kuwa wanamuziki wengi hawafuatilii mpira wa miguu, lakini kwa Tunda Man ni tofauti kidogo kutokana na kueleza kuwa siri yake ya ushindi ni kuujua mpira vilivyo.

"Mimi kabla ya kuwa mwanamuziki nilikuwa mchezaji wa mpira hivyo mimi ni mpenzi wa mpira kweli kweli.

"Nina ujuzi mkubwa kujua timu gani inashinda au haishindi nikawa napata pata hizi hela ndogo ndogo laki saba, laki nane milioni moja ila leo ndo nimepata kibunda kikubwa," alitilia mkazo.

Akizungumza na SportPesa News, baada ya kukabidhiwa mfano wa hundi, Tunda Man ameorodhesha baadhi ya vitu ambavyo atafanya baada ya kushinda kitita hicho.

"Hela haikosekani cha kufanyia ila sasa hivi sitategemea tena kibunda cha muziki.

"Nitarekebisha vitu fulani pale nyumbani, nimnunulie 'wife' ndinga mpya, lakini pia nina timu ya U-17 nilikuwa naiendesha kinja ninja ila sasa nimepata hela ya kusimamia timu yangu," alihitimisha Tunda Man.

## Milambo afutwa kazi Serengeti Boys

**Na Mwandishi Wetu**

BENCHI la Ufundi la timu ya Soka ya Taifa ya Vijana wa umri chini ya miaka 17 (Serengeti Boys), lililokuwa chini ya Kocha Mkuu, Oscar Milambo, limevunjwa.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia, alisema kuwa wamefikia uamuzi huo kutokana na matokeo mabaya ambayo timu hiyo iliyapata katika fainali za Vijana za Afrika (Afcon U-17), zilizofanyika nchini Aprili mwaka huu.

Karia alisema TFF itatafuta kocha mwingine mpya atakayeanza kuinoa timu hiyo huku tayari wakianza kutumia walimu kuangalia wachezaji wenye vipaji katika mashindano ya vijana ya umri chini ya miaka 15 yanayoendelea jijini Dar es Salaam na Kibaha mkoani Pwani.

"Napenda kuwaambia kuwa jopo la U-17 lililokuwa chini ya Oscar Milambo limevunjwa rasmi, kuna vitu mbalimbali tumevibaini na tunapanga kuvirekebisha katika kuanza kuunda timu mpya, hivyo tutatangaza kocha mpya ambaye naye ataanza na watoto kuanzia chini," alisema Karia.

Aliongeza kuwa shirikisho hilo linaendelea kujipanga kuendesha mashindano mbalimbali ya vijana kwa sababu ndiyo yanayozalisha wachezaji ambao baadaye wanakuwa tegemeo kwenye kikosi cha Stars.

## Ninje aachia ngazi TFF

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI wa Ufundi wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Ammy Ninje, ameachia ngazi katika nafasi hiyo kutokana na kubanwa na majukumu ya kifamilia, imeelezwa.

Rais wa TFF, Wallace Karia, alisema jana kuwa Ninje, ameshindwa kuendelea na majukumu yake kutokana na kubanwa na familia yake ambayo inaishi London, England na hivyo watalazimika kutafuta mkurugenzi mpya.

Karia alisema kuwa licha ya kurejea England, Ninje ataendelea kushirikiana na TFF katika mambo mbalimbali ya kiufundi kwa sababu bado ana nia ya kushiriki katika kuendeleza kiwango cha soka hapa nchini.

"Tunawatangazia rasmi kuwa Ammy Ninje si Mkurugenzi wa Ufundi tena wa TFF, ni kutokana na changamoto ya vikwazo vya kifamilia, anarejea UK, atakuwa kule muda mrefu," alisema Karia.

Kabla ya Ninje kuwa Mkurugenzi wa Ufundi, alikuwa Kocha Mkuu wa Tanzania Bara (Kilimanjaro Stars) ambayo iliishia katika hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la Chalenji kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati yaliyofanyika mwaka juzi nchini Kenya.

# Michezo

Alhamisi Juni 13, 2019

Nipashe




Messi aongoza kwa kulipwa zaidi duniani

HABARI UK 30

UZI MPYA...



Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda (kulia), wakionyesha jezi mpya za timu ya soka ya Taifa 'Taifa Stars' baada ya uzinduzi uliofanywa jana jijini. Jezi ya bluu ni ya nyumbani na njano ya ugenini. MPIGAPICHA WETU

# KICHUYA, BANDA WATEMWA STARS

**Makonda awaonya wanaoibeza Tanzania Afcon, Amunike afunguka ubora wao wakiivaa Misri leo huku...**

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), ikitarajia kushuka dimbani leo kuwavaa Misri katika mchezo wa kirafiki mjini Alexandria, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Emmanuel Amunike, ametangaza kuwatema nyota tisa akiwamo Shiza Kichuya na Abdi Banda.

Wachezaji wengine walioachwa katika kikosi cha mwisho ni Claryo Boniphace, Selemani Salula, David Mwantika, Fred Tangalu, Miraji Athumani, Shaban Chilunda na chipukizi, Kelvin John.

Akizungumza jana baada ya kutangaza kikosi chake nchini Misri, Amunike alisema anaamini mchezo wa leo utasaidia kubaini makosa yaliyobaki kikosini na kuyafanyia kazi kabla ya kuanza kwa fainali hizo.

"Mechi hii ya kwanza dhidi ya Misri itatupa nafasi ya kuona idara tulizoimarika na zenye mapungufu, itatusaidia kujitathimini na itatuweka tayari kuanza kwa mashindano kabla ya kucheza mchezo mwingine dhidi ya Zimbabwe," alisema Amunike.

Kikosi kamili cha Stars kitakachoshiriki Afcon kinaundwa na Aishi Manula, Metacha Mnata, Aron Chalambo, Hassan Kessy, Gadiel Michael, Mohammed Hussein 'Zimbwe Jr", Himid Mao, Feila Salum "Feitoto", Frank Domayo, Yahya Zayd, Aggrey Moris, Kelvin Yondani, Mudathir Yahya, Ally Mtoni, John Bocco, Thomas Ulimwengu, Farid Mussa, Simon Msuva, Rashid Mandawa, Abdillahie Mussa, Vicent Philipo, Erasto Nyoni na Mbwana Samatta.

**MAKONDA AFUNGUKA**

Katika hatua nyingine, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, amewataka wadau wa michezo nchini kuacha kuibeza Taifa Stars ambayo inatarajia kushiriki fainali za Kombe la Mataifa Afrika (Afcon) 2019, zinazotarajiwa kuanza Juni 21 hadi Julai 19 nchini Misri.

Akizungumza katika uzinduzi rasmi wa jezi za Taifa Stars, Makonda, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ushindi ya timu hiyo, alisema kufanya hivyo kunawakatisha moyo wachezaji ambao wamepewa dhamana ya kupeperusha bendera ya nchi kwenye mashindano hayo makubwa barani Afrika.

Makonda alisema huu si wakati wa kuwakatisha tamaa wachezaji wa timu hiyo na badala yake wadau wanatakiwa kuwaunga mkono ili waweze kufanya vizuri katika mashindano hayo yanayoshirikisha nchi 24.

"Tuache kuwabeza, tusiwakatishe tamaa wachezaji wetu, wametoka Simba, Yanga, Azam, Lipuli, Kagera Sugar, tuheshimu mchango wao, hiki ni kipindi cha kuonyesha mahaba kwa timu na kwa taifa, tuangalie mazuri, tuyakuze, tuache kuongea mapungufu, tuongee vitu chanya kuhusiana na timu yetu, na taifa letu," alisema Makonda.

Alisema anafahamu timu hiyo iliondoka kinyonge, lakini hilo lilitokana na ratiba iliyobana ila yeye na kamati yake wanaendelea kukusanya ahadi kutoka kwa kampuni zaidi ya 40, ambayo kila moja litatoa kiasi cha Sh. milioni 10 ili kuwahamasisha wachezaji wa timu hiyo wafanye vizuri.

Kiongozi huyo alisema kuwa ili kuonyesha mapenzi kwa Stars, amewataka mashabiki wa soka nchini kununua jezi hizo katika maduka rasmi na kuwatahadharisha wale watakaodurufu jezi hizo, watachukuliwa hatua kali.

"Ni historia mpya, jezi hizi zitaonyesha umoja wetu, mapenzi yetu kwa Stars, uzalendo wetu, itaonyesha kielelezo cha Utanzania wetu kuanzia mtaani hadi kimataifa," alisema Makonda huku pia akitangaza kununua jezi 100 na kuwapatia wajumbe wake walioshiriki katika mchakato wa kuhakikisha timu hiyo inakata tiketi ya kucheza fainali hizo za Afcon.

## Nyoni, Manula wajifunga Simba

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI bado utata wa mkataba upi ni halali wa mshambuliaji, John Bocco, ukiendelea kuwa gumzo, mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, wameweka wazi kwamba wamewapa mikataba mipya wachezaji wake wawili ambao ni golikipa, Aishi Manula na beki, Erasto Nyoni.

Manula na Nyoni, ambao walitokea kwa mabingwa wa Kombe la Kagame na FA, Azam FC, kila mmoja amesaini mkataba wa miaka miwili, lakini picha zikionyesha kuwa walisaini kabla ya kujiunga na kambi ya timu ya Taifa (Taifa Stars) ambayo sasa iko Misri ikijifua kujiandaa na fainali za Kombe la Mataifa Afrika (Afcon) 2019.

"Tutaendelea kudondosha moja moja," alisema kwa kifupi, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara.

Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, Salim Abdallah 'Try Again' alisema jana kuwa Bocco ni mchezaji halali wa klabu yao na Polokwane City ya Afrika Kusini haikufuata taratibu katika kumsajili mshambuliaji huyo.

"Wamepotea, Bocco ni mali ya Simba, mkataba wake ni halali na wala hakuna kilichotengenezwa," alisema kiongozi huyo.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042